# Nipashe

Alhamisi Agosti 22, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 05780003

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Wabunge wadaiwa sugu wa nyumba za TBA watimuliwa

UKURASA 3




UKURASA 13

# Tatizo ajira vijana sasa lapata suluhu

UKURASA 2



Daktari Bingwa wa Upasuaji Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Edwin Mrema, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa Hospitali hiyo, Aminiel Aligaesha. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mtaalamu ataja sababu majeruhi moto kufariki

**WATATU** zaidi wapoteza maisha Muhimbili, sasa wafikia 100...*Endelea ukurasa wa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**KABUDI AKIRI UPINZANI MKALI KISWAHILI SADC**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi...

**UKURASA WA 3**

**BALOZI SEIF AWATAKA WAKAZI KAHAMA KUZALIANA KWA WINGI**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka wakazi wa Wilaya ya Kahama mkoani...

**UKURASA WA 4**

**KORTINI TUHUMA KUENDESHA UPATU, UTAKATISHAJI WA FEDHA**

WAFANYABIASHARA Magdalena Uhwello na Halima Nsubuga, wamefikishwa...


## Mkoa wakosa umeme siku 3

UKURASA 3


**MICHEZO** KMC YAMWAGIWA BILIONI, YAITANGAZIA VITA AS KIGALI UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Mwarobaini kutatua ukosefu ajira waja

**Na Gwamaka Alipipi**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kimesema kuna haja kwa serikali kuipa msukumo mpya falsafa na sera ya elimu ya kujitegemea katika mfumo wa elimu, kwa kuwa ndiyo itakayolikomboa taifa katika tatizo la ajira kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu.

Kimesema katika mazingira ya sasa, sera hiyo ina umuhimu mkubwa kuliko wakati mwingine wowote wa uhai wa taifa.

Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya ujasiriamali kwa wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu yaliyoandaliwa na chuo hicho.

"Ukiisoma vizuri na makini utagundua kuwa sera hii ambayo iliasisiwa mwaka 1967 na chama cha Tanu chini ya uongozi wa (hayati) Mwalimu Julius Nyerere, ndiyo itakayotukomboa kutoka kwenye kongwa la kufikiri kuwa ajira ziko ofisini. Sera hii inasisitiza sana umuhimu wa elimu yetu kuwafanya wahitimu katika ngazi mbalimbali za elimu kufikiria kujiajiri badala ya kuajiriwa," alisema.

"Wahitimu wetu watatengeneza ajira badala ya kusubiri kuajiriwa. Kwa upekee naomba hii iwe changamoto kwa wadau wa elimu katika ngazi mbalimbali za elimu hususani taasisi zetu zinazoandaa mitaala inayotumika shuleni, vyuo vya kati na vikuu," aliongeza.

Kuhusu mafunzo hayo, Prof. Anangisye alisema UDSM itawafikia zaidi ya wahitimu wa elimu ya juu 2,000 kutoka mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Lindi, Kaskazini Pemba, Katavi, Mbeya, Mwanza na Unguja Kusini, kwa kuwafundisha ujasiriamali bure.

Alisema wazo la kuandaa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana waliomaliza masomo katika vyuo vya elimu ya juu, limetokana na utafiti walioufanya na kugundua kuwa vijana wengi wanaomaliza elimu ya juu wanahangaika kutafuta kazi za kuajiriwa serikalini au mashirika binafsi.

"Sote tunafahamu, siku hizi ajira ni adimu na wakati mwingine huchukua muda mrefu mpaka kupatikana na hivyo kuwaathiri vijana wengi, hivyo tukabuni wazo la kuwazesha vijana kutambua changamoto za kijamii zilizopo na kujaribu kuzibadili kuwa fursa," alisema Prof. Anangisye.

Alisema mafunzo hayo yaliyoanza Agosti na yatamalizika Septemba, ni mkakati wa uongozi kudhihirisha UDSM kwa wananchi pamoja na kuchangia katika utekelezaji wa mikakati ya serikali kukabiliana na changamoto za ajira kwa vijana, hususani wahitimu wa vyuo vya elimu ya juu nchini.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Walemavu, Jenista Mhagama, aliyemwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alitaka mafunzo hayo kujikita katika kutoa elimu, ujuzi, kujitegemea na kuwa ya vitendo kuliko kukaa darasani.

"Nataka asilimia 40 ya mafunzo yafanyike darasani na asilimia 60 yawe ya vitendo. Mafunzo haya ni muhimu katika kuifikisha nchi kufikia uchumi wa viwanda," alisema Mhagama.

Aliwataka wakuu wa mikoa nchini kutenga eneo la uwekezaji kwa ajili ya vijana watakaokuwa na mawazo mazuri ya kibiashara.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Balozi wa Afrika Kusini, Thamasanqa Dennis Mseleku, ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana, alipokwenda kwa ajili ya kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa kufanya kazi nchini. Habari Uk. 4. **PICHA: OWM.**

# Kabudi akiri upinzani Kiswahili SADC

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, amesema Tanzania ilipata upinzani mkubwa katika jitihada zake kuishawishi Jumuiya ya Maendeleo kwa Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kukifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha nne rasmi za shughuli za jumuiya hiyo.

Mkutano wa 39 wa wakuu wa nchi za SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, ulikipitisha Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne ya shughuli zake. Awali jumuiya hiyo ilikuwa inatumia Kiingereza, Kifaransa na Kireno.

Hata hivyo, katika mkutano wake na wahariri na waandishi wa habari jijini jana, Prof. Kabudi alisema haikuwa rahisi kwa Tanzania kuishawishi jumuiya hiyo iridhie Kiswahili kutumika katika shughuli zake.

"Tumepata upinzani mkubwa kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne kwenye mikutano na shughuli za SADC. Baadhi ya mataifa yalipinga kwa hoja kwamba ni lugha ya kabila fulani na hatuwezi kuwalaumu," Prof. Kabudi alisema.

Waziri huyo aliwataka Watanzania kutobweteka badala yake watumie fursa hiyo kujipatia ajira.

"Wataalamu wengi wanaofundisha Kiswahili Amerika na Ulaya kwa sasa wanatoka Kenya na Congo. Tuchangamkie fursa hii muhimu, lakini lazima tujifunze lugha nyingine za kigeni hasa Kifaransa na Kireno.

"Mshindani wa Tanzania katika fursa hii ya Kiswahili kusini mwa Afrika ni Congo. Lazima niuseme ukweli huu maana maeneo mengi Congo ni wazungumzaji wakubwa wa Kiswahili na wanaijua vizuri lugha ya Kifaransa," alisema.

Prof. Kabudi pia alisema Tanzania ambayo imepewa uenyekiti wa SADC kwa mwaka mmoja hadi Agosti mwakani, inaunga mkono maombi ya Burundi kujiunga na jumuiya hiyo, akibainisha kuwa nchi hiyo imefuzu vigezo kwa zaidi ya asilimia 70.

"Kuna maeneo mawili ambayo Burundi inapaswa kuyafanyia kazi. Mojawapo ni kuihakikisha jumuiya kwamba itakuwa na uwezo wa kulipa ada ya mwaka ya mwanachama wa SADC," alisema.

Prof. Kabudi ambaye ni mwalimu wa sheria, akifundisha kwa muda mrefu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), pia alisema Tanzania itasimamia kidete uondoaji wa vikwazo dhidi ya Zimbabwe ili kuinua uchumi wa nchi hiyo tajiri wa madini.

Katika mkutano wake huo na wanahabari, Prof. Kabudi alivipongeza vyombo vya habari kwa kazi kubwa viliyoifanya ka-

INAENDELEA UK. 8

# Mtaalamu ataja sababu majeruhi wa mafuta kufariki Muhimbili

**Na Mary Geofrey**

WAKATI idadi ya watu waliopoteza maisha kufuatia ajali ya moto wa lori la mafuta iliyotokea Morogoro ikifika 100, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Edwin Mrema, ametaja sababu za watu ya wanaopoteza maisha kuongezeka kila siku.

Alisema wagonjwa wengi waliungua ndani ya mwili kwa asilimia 70 hadi 100 kutokana na kuathiriwa na moshi wa moto wa mafuta ya Petroli kuanzia kwenye mfumo wa upumuaji, mapafu na figo.

Alisema mbali na kusababisha athari ndani ya mwili, pia majeraha yaliyokuwa nje ya mwili yalikuwa ni kuanzia asilimia 50 hadi 100, hali iliyosababisha baadhi miili yao kuwa wazi kwa asilimia 90.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema kutokana na eneo walilopatia ajali kutokuwa rafiki kupata huduma ya kwanza, walifikishwa Muhimbili wakiwa katika hali mbaya.

"Moto wa wazi ni mbaya ambao unaunguza vitu vingi kama uliotokea kwa wenzetu pale Morogoro. Ni hatari sana kwa sababu mtu anapoungua mwili unaathirika katika ogani zote kuanzia hali ya upumuaji, mapafu na figo kwa sababu ya kuvuta hewa yenye kemikali zinazotokana na vitu vilivyoungua," Dk. Mrema alisema na kuongeza:

"Na kulingana na ulivyoungua mwili unakuwa hauna kinga bali unakuwa wazi kwa asilimia 90 kwa sababu ngozi ni kinga kubwa ya mwili ndicho kilichotekea kwa majeruhi wetu ambao tumetumia jitihada kubwa na mbinu mbalimbali kuokoa maisha yao bila mafaikio."

Alisema kutokana na majeruhi hao kuathirika ndani na nje ya mwili walilazimika kuwawekea mashine za kupumulia ili kuondoa hewa ya sumu waliyovuta aina ya 'Carbonmonoxide Poisoning' na kuwaingizia hewa safi ya Oxygen wakati wakiendelea na kutibu vidonda vya moto.

Alisema ngozi ikiungua inafanya kilicho ndani kisitoke nje na mwili unapoteza maji mengi yenye chumvi na madini mengi ndio sababu mgonjwa anayeungua kwa zaidi ya asilimia 80 uponaji wake unakuwa na shida.

Alisema pia majeraha ya moto yanasababisha mzunguko wa damu kupungua na kushindwa kuingia kwenye mapafu, maini, figo na mwili kupata shoku.

Dk. Mrema alisema moyo nao unaanza kufanya kazi ya ziada kusukuma damu kwenda sehemu nyingine za mwili na mwili kupoteza kinga zote.

"Ajali ya moto dawa yake ni

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Balozi Seif awataka wakazi Kahama kuzaliana kwa wingi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amewataka wakazi wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga kuzaliana kwa wingi kwa kuwa wana rasilimali za kutosha.

Balozi Seif alitoa ushauri huo kutokana na takwimu za Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama kuzalisha wajawazito 40 hadi 50 kwa siku.

Kutokana na hali hiyo, aliwaomba wananchi hao wasichoke kuzaa ili kuijaza nchi kuenzi utamaduni wao wa kuwa na familia yenye watoto wengi.

Mkoa wa Shinyanga ni mkubwa kijogorafia na kuna maeneo makubwa ya kupata chakula cha kutosha, hivyo wananchi hawanabudi kuendelea kuujaza mkoa wao kwa kuzaliana kwa wingi na kuongeza uzalishaji wa chakula.

Balozi Seif aliyasema hayo alipotembelea Hospitali ya Mji wa Kahama na kuzungumza na wazazi waliojifungua pamoja na wauguzi, huku akisisitiza wauguzi wa hospitali hiyo kuwa la lugha nzuri kwa wagonjwa.

Alisema kitendo cha hospitali ya mji kuwa na idadi ya kuzalisha watoto 40 mpaka 50 kwa siku sio suala la kubeza, na kuongeza kuwa watoto hao baadaye wataongeza nguvu kazi katika kuzalisha chakula ambacho kitakuwa msaada katika familia wanazotoka na mkoa mzima.

Akikabidhi msaada wazazi waliojifungua siku hiyo, mke wa Balozi Seif, Asha Suleiman, aliwataka wazazi kuvitumia vyema vifaa hivyo.



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, akizungumza na wamiliki na wakuu wa vyombo vya habari, jijini Dar es Salaam jana, akiwashukuru kwa ushiriki mzuri wa vyombo vya habari, wakati wa Mkutano wa 39 wa SADC, uliomalizika hivi karibuni. Kutoka (kulia) ni aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya mkutano huo, Agnes Kayola, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Damas Ndumbaro na Mwakilishi wa Vyombo vya Habari, Richard Mngazija. **PICHA: JOHN BADI**

# Wadaiwa sugu TBA watimuliwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAKALA wa Majengo nchini (TBA) imeanza kuwaondoa wadaiwa sugu wakiwamo watumishi wa umma, wabunge na baadhi ya taasisi za serikali wanaodaiwa zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kutokana na malimbikizo ya kodi ya muda mrefu.

Wadaiwa hao ni wale wanaoishi kwenye maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma, Mtaa wa Area C na D, jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Meneja wa TBA, Herman Tanguye, alisema operesh

INAENDELEA UK.8

# Kagera yakosa umeme na maji kwa siku tatu

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WILAYA tano kati ya saba mkoani Kagera, jana ziliingia siku ya tatu zikiwa gizani kutokana na kutokuwapo kwa umeme, na kusababisha hasara kwa wafanyabiashara wanaoendesha shughuli zao kwa kutumia umeme.

Wilaya hizo ni Bukoba, Muleba, Missenyi, Karagwe na Kyerwa, ambazo zinategemea umeme kutoka Uganda.

Katizo la umeme katika wilaya hizo lilianza Jumatatu majira ya asubuhi, huku Ngara na Biharamulo pekee ndizo zinazopata huduma hiyo kutokana na kuwa katika gridi ya Taifa.

Kaimu Meneja wa Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) mkoa wa Kagera, Mhandisi Shaban Mashaka, alisema tatizo hilo limesababishwa na hitilafu iliyotokea karibu na mji wa Masaka, Uganda.

Mashaka alisema mafundi wa Uganda wanaendelea kushughulikia tatizo hilo, na kuwa Tanesco Kagera imetuma mafundi wake ili washirikiane kutatua tatizo hilo.

Tatizo hilo pia limesababisha kutokuwapo kwa huduma ya maji inayotolewa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Buwasa), hali inayosabasha wananchi kuhangaika kutafuta maji ya mito na Ziwa Victoria.

Audax Mutasingwa Mafumbo kutoka Manispaa ya Bukoba, alisema pamoja na kulala gizani kwakukosa umeme, pia amekosa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani.

"Namshukuru Mungu leo (jana) mvua imenyesha, nimekinga maji ingawa nimechelewa kwenda kazini, lakini maji kidogo kwa ajili ya matumizi nimepata, ingawa siwezi kufua wala kufanya shughuli nyingine zinazohitaji matumizi makubwa ya maji maana sifa

INAENDELEA UK.8



# Sababu UN kuifagilia Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Mataifa (UN) umeipongeza Tanzania kwa namna inavyotumia vizuri rasilimali zake za ndani, hivyo kuiwezesha kutekeleza shughuli mbalimbali za kimaendeleo sambamba na kupunguza utegemezi kutoka nje.

Pongezi hizo zilitolewa jana na Mratibu Mkazi UN nchini, Alvaro Rodriguez, alipokutana na kufanya mazungumzo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jijini Dar es Salaam.

Rodriguez, ambaye alikwenda kumuaga Waziri Mkuu, alisema Tanzania imeendelea kutumia vizuri mapato yake ya ndani kwa kuimarisha miundombinu na huduma za kijamii kama ujenzi wa hospitali na vituo vya afya.

"Katika kipindi changu cha miaka mitano ambacho nimefanya kazi Tanzania, nimeshuhudia mabadiliko makubwa ya kimaendeleo yanayofanywa na Serikali, ikiwamo kuimarika kwa mahusiano kati ya Serikali na UN na taasisi zake nchini."

Katika hatua nyingine, Rodriguez ameisifu Serikali ya Tanzania kwa namna ilivyoweza kuandaa na kuendesha vizuri mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika wiki iliyopita.

Mbali na kuisifu Serikali, pia kiongozi huyo amevipongeza vyombo vya habari kwa jinsi vilivyoshirikiana na Serikali kuripoti matukio mbalimbali ya mkutano huo. "Nawapongeza wananchi kwa ushirikiano walioutoa kwa Serikali wakati wote wa mkutano wa SADC."

Kwa upande wake, Waziri Mkuu amemshukuru kiongozi kwa pongezi alizozitoa ambazo ni ishara kwamba anatambua jitihada zinazofanywa na Serikali katika kutumia vizuri rasilimali zake.

Waziri Mkuu alisema: "Maelezo yaliyotolewa na Rodriguez yanaakisi kauli za Rais John Magufuli kwamba Tanzania si nchi masikini na inao uwezo wa kutoa misaada kutokana na rasilimali nyingi ilizonazo. Watanzania waendelee kuiunga mkono Serikali yao."

Pia, Waziri Mkuu ametumia fursa hiyo kumpongeza kiongozi huyo kwani alikuwa kiungo kizuri kati ya Serikali ya Tanzania na UN. Pia atakumbukwa sana kutokana na mambo mengi aliyoyafanya kipindi cha utumishi wake nchini.

Awali, Waziri Mkuu alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Afrika Kusini, Thamasanqa Dennis Mseleku, ambaye alikwenda kwa ajili ya kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa kufanya kazi nchini.

Waziri Mkuu alimpongeza Balozi huyo kwa ushirikiano na mchango alioutoa kwa Serikali ya Tanzania katika shughuli mbalimbali za kimaendeleo zikiwamo za kiuchumi, elimu, afya, maendeleo ya jamii pamoja na kuimarisha uhusiano baina ya nchini mbili hizo.

# Kortini kwa tuhuma kuendesha upatu, utakatishaji wa fedha

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA Magdalena Uhwello na Halima Nsubuga, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakikabiliwa na mashtaka saba yakiwamo kuendesha biashara ya upatu isiyo halali na kutakatisha fedha.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao katika mahakama hiyo mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai washtakiwa walitenda makosa hayo kati ya Aprili Mosi na Juni 30, 2017.

Katika shtaka la kwanza, wanadaiwa kuwa Aprili Mosi, 2017 na Juni 30, 2017 maeneo ya jiji la Dar es Salaam washitakiwa hao walikula njama kutenda kosa la kusimamia na kuendesha biashara ya upatu.

Wankyo alidai katika shtaka la pili, tarehe na mahali hapo, washtakiwa walikusanya fedha kutoka kwa watu mbalimbali ambazo walikuwa wakichangisha kwa kuwaahidi kuwapatia faida watakayopata.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha, Simon alidai kuwa Aprili Mosi na Juni 30, 2017 washitakiwa hao walijihusisha na muamala wa Dola za Marekani 394,265 kwenye akaunti ya Magdalena na Halima kupitia Benki ya Equity Tanzania Ltd wakati wakijua kwamba fedha hizo ni zao la kosa la kuendesha biashara ya upatu.

Ilidaiwa kuwa Aprili 22, 2017 maeneo ya jiji la Dar es Salaam, kwa lengo la kuficha chanzo halali cha fedha hizo, walihamisha Dola za Marekani 12,309 kwa Benki ya Equity Uganda kwa jina la Smart Magara.

Aprili 24, 2017 washtakiwa hao wanadaiwa walihamisha Dola za Marekani 29,890 kwenye akaunti ya jina hilo.

Wakili Simon aliendelea kudai kuwa Aprili 25, 2017 maeneo ya jiji la Dar es Salaam, washtakiwa walihamisha Dola za Marekani 58,743 kupitia benki ya Equity Uganda.

Pia ilidaiwa kuwa Aprili 21, 2017 washitakiwa walihamisha Dola za Marekani 83,718 kwenye benki ya Equity Uganda kwa jina la Magara huku wakijua kwamba fedha hizo ni zao la makosa ya kuendesha biashara ya upatu.

Washitakiwa walikana mashitaka hayo na upande wa mashitaka ulidai upelelezi wa shauri hilo bado haujakamilika.

Wakili wa utetezi, Peter Kibatala, aliomba mahakama kupanga tarehe fupi kwa ajili ya kutoa hoja za kisheria kuhusu uhalali wa hati ya mashtaka.

Hakimu Simba alisema kwa mujibu wa sheria ya mashitaka wanayoshtakiwa nayo hayana dhamana kisheria, hivyo aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 30, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa.




Magari yakiwa katika foleni nyakati za asubuhi katika Barabara ya Ali Hassan Mwinyi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI.**

# TBS kufanya ukaguzi wa kushtukiza nchi nzima

**Na Joseph Mwendapole**

BAADA ya kubaini udanganyifu unaofanywa na baadhi ya wazalishaji wa nondo nchini, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limepanga kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye viwanda vyote nchini na kuchukua hatua ya kisheria kwa wazalishaji wasiofuata viwango vya ubora wa nondo.

Shirika hilo lilitangaza uamuzi huo juzi jijini Dar es Salaam kutokana na ukaguzi walioufanya kwenye masoko kubaini kuwapo udanganyifu mkubwa unaofanywa na baadhi ya wazalishaji wa nondo, jambo ambalo ni la hatari.

Akizungumza baada ya kumaliza kufanyika ukaguzi kwenye maduka yanayouza nondo katika maeneo ya Kawe, Buguruni, Mwenge na Tegeta juzi, Mkaguzi wa TBS, Mhandisi Donard Manyama, alisema katika ukaguzi wao wamebaini kuwapo kwa nondo nyingi zisizokidhi viwango kwenye matumizi ya ujenzi.

"Ukaguzi wetu umebaini kuwapo udanganyifu katika uzalishaji wa nondo kuanzia unene, urefu na madaraja vyote hivyo hakuna ukweli jambo hili ni hatari kama litafumbiwa macho," alisema Manyama.

Alisema kiwango halisi cha urefu wa nondo huwa ni ujazo husiopungua futi 40, lakini zilizopo sokoni baadhi zina futi 39 hadi 34, huku unene yaani ujazo wa kipenyo halisi ni mm 18, lakini zilizopo sokoni nyingi ujazo wake ni tisa hadi sita.

Alizungumzia pia kuhusu udanganyifu unaofanywa na wafanyabiasharara kuuza bei moja kati ya nondo za daraja la BS 300 na 500 kwamba kufanya hivyo ni kosa kisheria.

## Waziri Simbachawene atoa maagizo Bonde la Kihansi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, ametaka kuwapo utunzaji endelevu wa ekolojia katika maporomoko ya Bonde la Kihansi kwa faida ya nchi na kizazi cha sasa na baadaye kutokana na umuhimu wake kwa mazingira.

Akizungumza katika ziara yake ya kutembelea bonde la maporomoko ya Mto Kihansi wilayani Kilombero mkoani Morogoro pamoja na kushiriki zoezi la kurejesha vyura wa Kihansi katika maeneo yao ya asili, Simbachawene alisisitiza umuhimu wa kutunzwa kwa ekolojia katika eneo hilo.

"Ekolojia iliyopo katika bonde hili ni muhimu kutunzwa kutokana na upekee wake na kuiletea faida nchi kwa vizazi vijavyo na pia napongeza hatua zinazoendelea kufanywa sasa za uhifadhi," alisema Waziri.

Aliagiza wataalamu waendelee kufanya utafiti juu ya ekolojia iliyopo katika bonde hilo na kuleta mapendekezo serikali yatakayosaidia kutunga sheria ambazo zitalifanya eneo hilo kuwa katika hali ya usalama kimazingira.

"Kihansi ina vitu vingi vya kipekee na pia kuna umuhimu wa kuendelea kulinda bonde hili ikiwamo vyura ambao wanasifa ya kuzaa, vipepeo na kahawa ya kihansi ambavyo vyote vinapatikana Tanzania tu," alisema Simbachawene.

"Kutokana na upekee wa ekolojia iliyopo katika Bonde la Kihansi kila mdau awajibike kwa nafasi yake kuhakikisha mazingira katika bonde hili yanahifadhiwa na kulindwa ili vizazi vijavyo vinufaike kwa kazi itakayofanyika sasa ya kupalinda," alisema.

# Kesi ya Wambura yapigwa tena kalenda



Mshtakiwa Michael Wambura akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kesi ya utakatishaji fedha inayomkabili kutajwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imeahirisha tena kesi inayomkabili Makamu wa Rais wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Michael Wambura, mpaka Septemba 4, mwaka huu, baada ya upande wa Jamhuri kudai kuwa upelelezi bado haujakamilika.

Jana kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina.

Wakili wa Serikali Ester Martin alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Kutokana na ombi hilo, utetezi ulidai kuwa upande wa Jamhuri uliahidi kuipa mahakama taarifa jana ya kuhusu hatua za upelelezi ulipofikia lakini bado unadai bado haujakamilika.

Martin alidai kuwa hajapata taarifa kutoka kwa wakuu wake wa kazi na kwamba wakili anayeendesha kesi hiyo amepata udhuru.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Septamba 4, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, kigogo huyo anakabiliwa na mashtaka 17 likiwamo la kughushi, moja la kutoa na kuwasilisha nyaraka za uongo, mashtaka 13 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na mawili ya kutakatisha fedha haramu.

Katika shtaka la kughushi, mshtakiwa anadaiwa kutenda kosa hilo Julai 6, 2004 sehemu isiyojulikana ndani ya jiji la Dar es Salaam.

Ilidaiwa siku na tarehe za tukio la kwanza, Wambura kwa nia ya kutapeli alitengeneza barua ya kughushi ambayo haina kumbukumbu namba akionyesha imeandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa kampuni ya Jeck System anayedai kurejeshewa malipo ya mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba aliyokuwa amekopesha TFF.

Katika shtaka la kutoa na kuwasilisha nyaraka ya uongo, mshtakiwa anadaiwa alitoa barua iliyokuwa haina kumbukumbu namba ya Julai 6, 2004, akijifanya kwamba ni barua iliyoandikwa na E. Maganga ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Jeck System Ltd, akionyesha kuwa anadai mkopo wa USD 30,000 pamoja na riba waliokopeshwa TFF huku akijua kuwa siyo kweli.

Pia katika mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, Wambura anadaiwa kutenda kosa hilo Juni 17, 2015 katika ofisi za TFF kwa njia ya udanganyifu, alijipatia Sh. milioni 10 kutoka TFF kwa kuonyesha kuwa ni malipo ya USD 30,000 pamoja na riba kutoka kwenye kampuni hiyo ya Jeck jambo ambalo si kweli.


SALAMU ZA PONGEZI

ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified



Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa EWURA,wanampongeza
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli**
kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya SADC kwenye kikao cha 39 cha jumuiya hiyo.

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF Pension Fund, Barabara ya Makole, S.L.P 2857, Dodoma, Tanzania-Simu:+255 26 239002-3,
Nukushi: +255 26 23 9005, Baruapepe: info@ewura.go.tz- Tovuti: www.ewura.go.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mgomo daladala Dodoma ni somo

**KIASI** muda unavyosonga watu wanaendelea kusahau yaliyotokea Morogoro kwenye ajali ya tangi la mafuta lililolipuka na kuua watu takribani 100 huko Msamvu.

Poleni tena majeruhi na wafiwa na Watanzania kwa kuwa idadi ya watu wengi kufa kwa wakati mmoja ni maafa kwa nguvukazi.

Tunaiomba serikali iwe na mikakati ya kudhibiti ajali za milipuko kama kuhakikisha kuwa wanaoishi chini ya nyaya za umeme mkubwa na kufanya biashara chini ya transfoma wanaondolewa na matangazo makubwa kama umeme ni hatari unalipuka yanabandikwa kuanzia sasa.

Hii ni kwa sababu transfoma ni kilipuzi lakini kuna maelfu ya watu 'wanatanua' chini ya mitambo hiyo ya kupoza na kuchochea umeme bila kujali kuwa wanahatarisha maisha yao.

Si hivyo tu serikali inapaswa pia kujifunza kile kilichotokea Dodoma, madereva wa bodaboda waligoma kushinikiza wafanyabiashara wa vyakula kama wachoma nyama, mahindi, chipsi na mamalishe kuondolewa kwenye stendi ya Sabasaba kwani wanahisi ni chanzo cha ajali.

Ni kweli kuwa ni chanzo cha milipuko kwa sababu wanatumia gesi na mkaa na kuni na yote hayo si rafiki wa petroli zilizoko kwenye injini za pikipiki na magari yanayoingia na kutoka kwenye stendi hiyo.

Serikali isipuuze masuala kama hayo yaliyotokea Dodoma maana kuwapo kwa moto na upishi jirani na magari kwenye vituo vya mabasi ni mwanzo wa mlipuko mwingine mkubwa ambao hata kama hautatokea leo unakuja.

Suala la ajali ya Msamvu liiamshe Tanesco iweke ulinzi na kuzizungushia uzio transfoma zake na ikibidi kuandika taarifa za kuonya hata kama inawezekana kuweka ving'ora vinavyotoa sauti za onyo na tahadhari kwa wanaozubaa chini ya mitambo hiyo.

Lakini, si hivyo tu kuwe na mwamko wa kuandika na kuweka lebo zinazoeleweka za kutangaza tahadhari kwenye magari ya mafuta kwa kuwa watu wengi hawafahamu kuwa Petroleum Danger kwenye magari ya mafuta inamaanisha nini.

Ni wakati wa kuandika alama na maneno ya tahadhari kwa lugha inayoeleweka. Magari ya mafuta yaandikwe na kila mmoja aelewe. Pengine alama za kuzuia usiwashe sigara au kuwasha moto hazieleweki kuwe na alama na ujumbe wa Kiswahili usivute sigara wala kuwasha moto karibu na gari la mafuta. Pia waandikiwe likianguka usilisogelee wala kugusa betri.

Kubadilisha alama na njia za mawasiliano ni muhimu nyakati hizi ili kuokoa maisha na kudhibiti yaliyotokea Msavu yasirudie tena.

Kuna baadhi ya watu hawazielewi alama za sumu mfano 'fuvu na mifupa'. Wapo wanaodhani ni alama za 'Freemason' hizo nazo ziandikwe kwa ufasaha na pengine alama hizo zibadilishwe kwani umma hauna uelewa.

Ni wakati wa kukataza mama na babalishe karibu na vituo vya mafuta. Kuzuia pia kuchomelea magari karibu na vituo vya mafuta na hata ndani ya vituo vya mabasi.

Lakini ni vizuri pia kuangalia upya alama na ujumbe wote unaotoa tahadhari ya kuonya kuhusu sumu na milipuko.

Kwa mfano ujumbe unatambulisha taarifa za kuwapo hatari, kuanzia kwenye magari, nyaya za umeme, taka za sumu, dawa zikiwamo viuatilifu na kemikali.

Kwa kudhani ni alama ya 'Freemason' wananchi wanaendelea kutumia madumu na vifungashio vya taka za sumu bila kujua kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Ni kwa kuzingatia kuwa wananchi wengi wana uelewa mdogo, ndiyo maana tunakumbusha mamlaka zinazohusika kusimamia usalama kutafuta njia bora za kuwasiliana na wananchi ili kuepusha hatari na kupoteza maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kujitolea ndiko kusogeza karibu huduma za afya

**KUTEMBEA** umbali mrefu kufuata huduma za afya ni moja ya changamoto, ambayo inazikumbuka baadhi ya wananchi wa mikoa mbalimbali.

Hata hivyo, baada ya serikali kuanzisha mkakati wa kujenga zahanati kila kijiji, baadhi ya vijiji vimeanza kunufaika nao, huku wananchi wakiunga mkono mkakati huo kwa kujitolea kujenga zahanati kwenye maeneo yao.

Miongoni mwa wananchi waliofanikiwa kutimiza azma hiyo ni wakazi wa vijiji vya Wilaya ya Musoma Vijijini mkoani Mara, ambao wamekuwa wakijitolea kwa hali na mali kujenga zahanati ambazo sasa zimefikia 20 na zinaelezwa kuwa zinatoa huduma.

Dokta Vincent Anney ni Mkuu wa Wilaya ya Musoma, ambaye anasema mbali na hizo, zipo nyingine mpya zinazoendelea kujengwa katika vijiji mbalimbali ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati.

Anasema mbali na ujenzi wa zahanati, wananchi hao pia wamekubali kuchangia ujenzi wa hospitali ya wilaya, ambao unaendelea sasa kwenye kitongoji cha Kwikonera katika kijiji cha Suguti.

"Musoma Vijijini ina kata 21, na kwenye kuchangia ujenzi wa hospitali ya wilaya, kila kata imekubali kuchangia Sh. milioni 7.5 na matarajio yetu ni kupata Sh. milioni 157.5," anasema Dk. Anney.

Kadhalika anasema kuwa mchango huo wa wananchi ni kuunga mkono juhudi za serikali kuu, ambayo imetoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, ambayo tayari majengo yake manane yameezekwa.

Suala la wananchi kuchangia ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali ni la muhimu kwani wao ndiyo wanaotarajia kupata huduma pale ujenzi unapokamilika.

Kwa mfano wakazi wa Musoma Vijijini, baadhi ya wananchi wamekuwa wakiuza mifugo yao ikiwamo ng'ombe ili kupata fedha za kuchangia ujenzi wa zahanati, kituo cha afya au hospotali.

**Kwa kawaida, serikali imekuwa ikiunga mkono pale wananchi wanapoonyesha jitihada katika jambo fulani la maendeleo, hivyo ni muhimu wananchi waendelee kuonyesha mfano kama hao wa Musoma Vijijini.**

Wengine wanasomba, mawe, mchanga, maji na kokoto, lengo likiwa ni kufanikisha ujenzi huo ili kusogeza huduma za afya karibu yao na kuondoka na changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Hii inatokana na ukweli kwamba haiwezekani viongozi kwenda kuomba msaada kwa watu wa nje kwa ajili ya kuwajengea zahanati au hospitali wakati wananchi wenyewe wapo na ndio wanufaika wakubwa.

Kwa kawaida, serikali imekuwa ikiunga mkono pale wananchi wanapoonyesha jitihada katika jambo fulani la maendeleo, hivyo ni muhimu wananchi waendelee kuonyesha mfano kama hao wa Musoma Vijijini. Inawezekana wakawapo baadhi ya wananchi, ambao hawataki kusikia habari za kuchangia maendeleo, lakini ninaamini kwamba wanaojitolea wanaweza kuwa chachu kwa watu wa aina hiyo.

Kimsingi ni kwamba utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa zahanati kila kijiji, vituo vya afya kila kata na hospitali kila wilaya ili kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi, hivyo juhudi hizo hazina budi kuungwa mkono.

Hivyo kama kuna baadhi ya wananchi ambao hawajatambua umuhimu wa kuchangia ujenzi huo, basi waendelee kuelekezwa vizuri wataelewa na mwisho wa siku wanaweza kuwa mstari wa mbele kushiriki kikamilifu.

Ikumbukwe kuwa afya maana yake ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwapo kwa maradhi na pia afya bora ni nguzo na raslimali muhimu katika kuchangia mtu na taifa.

Kwa mantiki hii afya inalenga kuwa na ustawi endelevu wa jamii, kwa kuzingatia mchango wa mtu binafsi kulingana na nafasi, uwezo na fursa zilizopo katika kuleta maisha bora.

# BARUA/MJADALA

## *Kwa nini ukere wenzako usafiri wa umma?*

**Habari za majukumu!**

*KIMSINGI nimejitokeza leo katika ukurasa huu wa barua kwa Mhariri unaotupatia fursa sisi wasomaji ya kuelezea changamoto na kero mbalimbali zinazotukabili, katika dhima nzima ya kusukuma gurudumu la maendeleo ya taifa letu mbele.*

*Lakini ukurasa huu hautoi fursa tu ya kuwasilisha changamoto na kero zinazotukabili, bali pia kupongeza inapobidi kwa kazi nzuri inayokuwa imefanyika katika maeneo yetu na hasa kama inalenga tija kwa jamii.*

*Mhariri, leo nimeona nijitokeze kuelezea kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo sana niwapo katika mihangaiko yangu ya kutafuta riziki ya kila siku, kwenda na kurudi nyumbani.*

*Nikiwa ni mkazi wa eneo la Mbagala katika jiji hili la Dar es Salaam, mara nyingi usafiri wangu wa kwenda na kurudi kutoka kwenye mihangaiko yangu huwa ni ule wa umma kwa maana ya daladala.*

*Kero ambayo nimekuwa nikikumbana nayo katika usafiri huu na wengine wenye mtazamo kama wangu, si ile ya kujazana kwenye mabasi hayo na hasa kwetu sisi wakazi wa Mbagala kama inavyojulikana na wengi katika jiji hili.*

*Kimsingi ninazungumzia tabia ya baadhi ya wasafiri wenzetu kuweka hadharani mambo yao ya siri ya kifamilia, mitaani ama kimahusiano kupitia mazungumzo ya simu za mkononi tena kwa sauti kubwa kiasi cha kuwa kero kwa wasafiri wenzao.*

*Unakuta mtu anaongea na shoga yake kwa simu kwenye daladala tena kwa sauti kubwa akimueleza namna pengine alivyomchongea jirani yake kwa mumewe au namna alivyomshushua mbele ya mashoga zake.*

*Kibaya zaidi unaweza ukakuta mtu anajadiliana na anayewasiliana naye mambo ya mahusiano ya kimapenzi, namna gani wakutane, saa ngapi na wapi kwa sauti kubwa bila hata ya kujali kama mazungumzo yake na hata sauti yake inakera wengine.*

*Kupitia kwako Mhariri, ninaomba watu wenye tabia hii waelewe kuwa kuna baadhi ya mazungumzo yasiyostahili kuwekwa wazi hadharani katika vyombo vya usafiri wa umma, ambavyo viko pale kwa ajili ya kusafirisha watu na si vinginevyo.*

**Said Majaliwa- Mbagala**


**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# SADC itufundishe kuviboresha vyombo vya habari nchini

**Na Mashaka Mgeta**

MOJA ya mambo yanayotajwa kuchangia mafanikio ya Mkutano wa 39 wa marais na wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ni ushiriki wa vyombo vya habari.

Vyombo vya habari kupitia watendaji wake, yaani waandishi wa habari na wataalamu wa nyanja nyingine katika tasnia hiyo, waliandaliwa, wakajitolea na kutumia muda mwingi kuielezea, kufafanua na kuelimisha umma kuhusu SADC na manufaa yake.

Rais John Magufuli aliungana na kauli iliyowahi kutolewa na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, akiwapongeza waandishi wa habari kwa namna walivyoweka mbele uzalendo katika kuutangaza mkutano huo.

Kisha mawaziri wengine, wanataaluma na wageni kutoka nje ya mipaka ya nchi, walikaririwa wakielezea namna walivyoridhishwa na ushiriki wa vyombo vya habari vya ndani kuandika na kutangaza kuhusu mkutano huo.

Hakika, kwa kazi iliyofanywa na waandishi wa habari walioripoti matukio ya kuanzia maandalizi ya mkutano, wiki ya maonyesho ya viwanda, vikao vya makatibu wakuu, wataalamu, mawaziri na hatimaye marais na wakuu wa SADC, ni sawa na kusema 'vyombo vya habari vimeutendea haki wajibu wao kwa Taifa'.

Lakini je, kushiriki kuitangaza SADC kwa mafanikio kiasi hicho, inatosha kuwaacha waandishi na vyombo vya habari 'wakiziishi' pongezi kwa kazi waliyoifanya?

Kwangu binafsi, jawabu rahisi kulitoa mara moja ni hapana.

Ninasema hivyo kwa maana matunda yaliyotokana na kazi za waandishi wa habari katika kuandika na kutangaza habari za SADC hayapaswi kuachwa hadi yaoze.

Ikiwa ni hivyo, jamii haitapata matunda mengine kutoka ndani ya nchi, jumuiya za kikanda na hata kimataifa.

Ndio maana katika kulitafakari suala hilo, ninaamini kwamba ipo haja kwa wadau wote kuanzia serikali, kuzidi kutambua kwamba vyombo vya habari vina wajibu mkubwa wa kuwaandaa, kuwaelimisha na kuwaelekeza raia kwa masuala yanayohusu maisha yao ndani na nje ya nchi.

Ufanisi wa hali hiyo unatokana zaidi na mazingira wezeshi na yaliyo rafiki kwa waandishi wa habari na wanataaluma wengine wanaoitumikia tasnia hiyo, kufanya kazi zao kwa weledi, sheria, haki, usawa na kadri ya mikataba na maazimio ya kikanda na kimataifa.

Kwa maana moja ya mafundisho yanayotokana na SADC kwa vyombo vya habari ni kuwa, mafanikio 'yanayozaa matunda mema' yana manufaa makubwa kwa raia wa kawaida.

Kiu ya kutafuta ushiriki wa raia katika uchumi, biashara na uhusiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa itaondoka pale azma hiyo ikifikiwa, na hapo ndipo vyombo vya habari vyenye waandishi weledi na wanaofanya kazi katika mazingira wezeshi na rafiki, watatimiza wajibu huo.

Kwa mfano, mbali na SADC, Tanzania pia ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Umoja wa Afrika (AU) na Umoja wa Mataifa (UN).

Lakini Tanzania imesaini na kuridhia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa, ambayo kwa sehemu kubwa haijafahamika kwa kiasi cha kutosha ama haijulikani kabisa kwa baadhi ya wananchi.

SADC inapofikia mwisho wake, Watanzania wanapaswa kujiuliza, ni namna gani moto huu wa waandishi na vyombo vya habari utaendelezwa katika hamasa ya kuwafanya raia washiriki na kunufaika na fursa za kikanda na kimataifa?

Majawabu yanaweza kuwa mengi, lakini miongoni mwa hayo ni kuchukua mfano kutoka katika mkutano wa SADC, utufundishe kuviboresha vyombo vya habari na kuwajengea waandishi wa habari mazingira wezeshi na rafiki kufanya kazi zao.

Hili likifanyika kwenye ajenda mbalimbali za kimaendeleo zinazogusa taifa, kanda na wananchi wake kwa ujumla litatoa matunda mema kama ilivyoonekana katika mkutano huu wa SADC.

Vyombo vya habari unaitwa mhimili usio rasmi wa dola kimsingi kutokana na wajibu wake kwa umma ambao ni pamoja na kuwapatia wananchi habari sahihi na kamili zinazowawezesha kuwa kwenye nafasi ya kuchukua maamuzi sahihi.

Maamuzi ambayo hatimaye yatajenga ustawi wao na jamii kwa ujumla lakini pia mahusiano yanayowahakikishia wanajamii amani na usalama wa maisha na mali zao kwa ujumla.

**Hongereni waandishi wa habari Tanzania.**
**0754691540**

## KABWELA — NA FADHIL MOHAMMED



HABARI KITAIFA

# Mtaalamu ataja sababu majeruhi wa mafuta kufariki Muhimbili

INATOKA UK 2

kuzuia moto usitokee kwa sababu unapotokea madhara yake ni makubwa. Moto ni kitu kikubwa kinachosababisha mwili kushindwa kufanya kazi kwa asilimia kubwa," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji Bandia, Dk. Laurean Rwanyuma, alisema baada ya kupokea majeruhi hao, jambo la kwanza waliwatenga kulingana na majeraha waliyokuwa nayo ili kuanza kuwapa matibabu.

Alisema jambo la kwanza waliangalia kwanza kama wanaweza kupumua vizuri na kuangalia kama wameungua kwa kiasi gani na kubainia ni kuanzia asilimia 70 hadi 100.

"Lakini pamoja na hayo, wengi walifunikwa na moto na kuvuta hewa yenye moshi wa kemikali iliyounguza mapafu na kuongeza hatari kwenye mapafu.Tulilazimika kuanza kuwatundikia dripu za maji na kuhakikisha hawapati baridi na dawa za maumivu.

Alisema duniani kote hasa katika nchi zilizoendelea, daktari anatakiwa kupigana kwa ajili ya maisha ya wagonjwa na ndicho walichokifanya kwa wagonjwa hao.

"Sisi tunapigana na maisha ya wenzetu haijalishi hali zao zilikuwaje, lakini lazima tujue kuwa wagonjwa waliungua kwa kiasi kikubwa na haijalishi wameathirika kwa kiasi gani,,, wajibu wetu ni kuhakikisha tunaokoa maisha yao ili mradi wawe wanapumua," alisema Dk. Rwanyuma.

Alisema wagonjwa wengine wanawafanyiwa upasuaji ikiwamo kunyoosha baadhi ya viuno na kubandua na kundika ngozi sehemu ambazo zenye majeraha makubwa.

Awali Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano MNH, Aminiel Aligaesha, alisema kati ya majeruhi hao 13 kati ya 15 waliobaki wapo katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) wakiendelea kupatiwa matibabu.

Alisema jumla ya majeruhi 32 wameshapoteza maisha kati ya 47 waliopokelewa Muhimbili kuanzia Agosti 10, mwaka huu.

Aliwataja waliofariki dunia juzi na kufikisha idadi ya majeruhi wote waliofariki 100 ni Mazoya Sahani, Khasim Marjani na Ramadhani Magwila.

Aidha, lisema wameshakusanya chupa 700 za damu kutoka kwa makundi ya watu mbalimbali wanaojitokeza kuchangia kwa ajili ya kuokoa maisha ya majeruhi hao, huku akiwaomba Watanzania kuendelea kuchangia damu kwa sababu majeruhi hao wanahitaji kiwango kikubwa cha damu.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa mifereji ya majitaka katika Mtaa wa Papa Sinza, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Wadaiwa sugu TBA watimuliwa

INATOKA UK. 3

eni ya kuwaondoa wadaiwa sugu ni endelevu na imeanzia jijini Dar es Salaam na kuhamia Dodoma kutokana na sehemu hizo kuwa na madeni makubwa kwenye nyumba nyingi ambazo wamewapangisha watu.

Alisema TBA imefikia hatua hiyo baada ya kutoa kwa wapangaji wengine notisi ya siku 30 kwa wapangaji ambao hawajalipa zaidi ya miaka 10 na kuwataka wajiandae kutolewa kwenye nyumba hizo.

"Hili zoezi si kwa Dodoma pekee bali litaendelea nchi nzima ambapo kuna majengo ya TBA," alisema Tanguye.

Alisema kwa mujibu wa mkataba wa nyumba hizo, wanatakiwa kila baada ya mwaka mmoja kulipa, lakini hawajafanya hivyo.

"Unakuta mtu hajalipa kodi ndani ya miaka kumi kinyume na makubaliano ndani ya mkataba aliopangishwa,"alisema.

Kutokana na hilo, alisema TBA imeamua kuwaondoa wapangaji hao kwa kutumia taratibu stahiki ambazo zinatambulika kisheria na mahakama inatambua.

"Tuliwapa notisi ya siku 30 baadaye tukawaongezea siku 14 wameshindwa kutekeleza ndio maana tumewaondoa," alisema Tanguye.

Naye, Kaimu Meneja Miliki wa TBA, Fredy Mangula, alisema wameshaziondoa familia tatu katika nyumba za eneo la area C na D na operesheni hiyo inaendelea katika nyumba nyingine za eneo hilo.

Alifafanua kuwa uondoaji wa wapangaji hao unafanyika kisheria kwa kushirikiana na kampuni ya Yono Action Mart kutoa vyombo vya wapangaji ambao walishapewa notisi ya kuondoka kutokana na kuwa wadaiwa sugu huku wengine wakimaliza muda wa kuishi maeneo hayo.

"Tunawaondoa wadaiwa sugu kwa kufuata sheria wengi wao walishapewa taarifa ikiwamo notisi na muda wa nyongeza, lakini wamepuuzia agizo hilo," alisema Mangula.

Alisema kinachotakiwa kwa waliopewa notisi za kuondoka, wasibweteke na badala yake watekeleze ndani ya muda waliopewa ili wasije kuondolewa kinguvu na timu inayohusika.

Akitoa ufafanuzi kwa wapangaji wa eneo hilo, alisema wote wanatakiwa kulipa kodi isipokuwa mawaziri ambao wao wanalipiwa kulingana na wadhifa waliokuwa nao.

Alisema, wabunge wanapaswa kulipa kwa wakati ikiwamo kufuata kanuni na taratibu za mkataba wa upangishaji inavyoelekeza.

"TBA tumekuwa wavumilivu sana toka Juni 30 baada ya mwaka wa fedha wa serikali kuisha tuliwapa notisi ikiwamo agizo la utekelezaji wa malipo ya kodi, lakini wengi hawajafanya," alisema Mangula.

Alisema watu wasichukulie mazoea na kuongeza waliopewa agizo wanapaswa kutekeleza.

Alisema lengo ni kukusanya madeni hayo na fedha hizo ni nyingi ambazo zinaweza kufanya kazi ya ujenzi wa nyumba nyingine eneo la Nzuguni ambako kuna hekari 630 kwa ajili ya kujenga nyumba za kupangisha watumishi wanaohamia.

Kwa upande wa wastaafu alisema, wanaondolewa kwa sababu wanaamini tayari wameshakuwa na makazi yao.

"Idadi ya watu wanaohamia makao makuu ni wengi nyumba zilizopo ni chache hivyo ni lazima watu waachie nyumba kama haustahili kukaa," alisema Mangula.

## Kabudi akiri upinzani Kiswahili SADC

INATOKA UK 2

tika Mkutano wa 39 wa SADC.

"Kwa kweli vyombo vya habari vimetekeleza wajibu wake vizuri sana katika mkutano huu. Waliokuwa na shaka na uongozi wa Tanzania katika eneo hili la SADC, vyombo vya habari vimewafanya sasa waamini Tanzania inaweza.

"Vyombo vya habari vilishikamana na serikali katika kipindi chote cha shughuli za SADC. Mkutano umemalizika lakini shughuli ndiyo kwanza zinaanza. Kutakuwa na mikutano zaidi ya 30 ya kisekta itakayofanyika hapa Tanzania.

"Mikutano inalenga kuwa na viwanda endelevu kwa lengo la kuongeza ajira na uzalishaji wa bidhaa bora," Prof. Kabudi alisema.

Waziri huyo aliongeza kuwa wakati wa vikao hivyo vya kisekta, watahakikisha wanasimamia utekelezaji wa uondoaji vikwazo vya kibiashara miongoni mwa nchi za SADC ili kuinua uchumi wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

## Kagera yakosa umeme na maji

INATOKA UK. 3

hamu kama mvua itanyesha tena," alisema.

Kagemuro Rweyemamu, mkazi wa Buyekera, alisema kukosa umeme kunawatesa zaidi kinamama, kwa kuwa ndo wanahangaika mtaani kutafuta maji kwa ajili ya matumizi ya familia.

"Hivi unavyoniona nimetoka kuchota maji Bunena kwenye chanzo cha asili ambako ni mbali na makazi yangu, kwa siku ninaweza kuchota ndoo tatu tu kutokana na msururu mrefu na umbali," alisema.

Mmoja wa wafanyabiashara duka la vifaa vya ofisi, Jasmin Joseph, alisema tangu Jumatatu anafungua ofisi tu, lakini hafanyi shughuli yoyote kutokana na kutokuwa na umeme.

"Hapa nafanya kazi za kutoa kopi, kuchapisha nyaraka, lakini tangu Jumatatu sijafanya kazi yoyote ya kuniingizia kipato, hapa nalipa kodi ina maana nisipofanya biashara ni hasara kubwa kwangu," alisema Jasmin.

Akizungumza kwa njia ya simu kutoka mpakani mwa Tanzania na Uganda eneo la Mtukula, Kalumuna Richard, anayeishi katika eneo hilo, alisema upande wa Uganda umeme upo ila kwa upande wa Tanzania haupo.

"Hapa Mtukula upande wa Tanzania hatuna umeme, lakini upande wa Uganda wana umeme, hatujafahamu kwa nini maana siyo kawaida," alisema Richard.

Hata hivyo baadhi ya wakazi wa manispaa ya Bukoba wenye mashine za kufua umeme (jenereta) akiwamo aliyefahamika kwa jina moja la Manyati, alisema kwa sasa wanachajisha simu kwa gharama ya Sh. 1,000.

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kueleza kuwa liko juu ya uwezo wake, na kuwataka waandishi kuwasiliana na waziri mwenye dhamana.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipopigiwa simu jana, hakupokea, na hata alipotumiwa ujumbe mfupi kuombwa ufafanuzi, hakujibu hadi tunakwenda mitamboni.

Wiki iliyopita, akizungumza mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Mjaliwa, wakati wa kufungua maadhimisho ya wiki ya Kagera yaliyolenga kutangaza fursa za uwekezaji, Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, aliomba serikali kuingiza mkoa huo katika gridi ya Taifa.

"Mheshimiwa Waziri Mkuu (Kassim Majaliwa), naomba mkoa wa Kagera uingizwe katika gridi ya Taifa ili kuepusha tatizo la umeme kukatika mara kwa mara," alisema Bashungwai.

# Wakulima tumbaku watangaziwa neema

**Na Waandishi Wetu,**
KAHAMA

SERIKALI mkoani Shinyanga imewahakikishia wakulima wa tumbaku katika Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama kuwa tumbaku iliyobaki kilo milioni mbili itanunuliwa baada ya kupatikana kwa kampuni mpya ya British America (BAT).

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Tellack, alitangaza neema hiyo wakati alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Ulowa namba tano kwenye ziara ya Makamu wa Pili wa Rais ya Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi.

Alisema, baada ya kampuni iliyokuwa ikinunua awali zao hilo TLTC, kusitisha ununuzi, serikali ilitafuta kampuni nyingine ya Alliance na kuahidi kununua asilimia 10 ya tumbaku iliyobaki na pia kampuni ya British America ambayo iko mbioni kununua tumbaku yote iliyobaki kwa mkulima.

"Najua kuna changamoto tuliyokutanayo kwenye ununuzi wa zao la tumbaku kwenye kata hii ya Ulowa, kampuni ya TLTC ilisitisha ununuzi wa zao hilo na kusababisha kilo milioni mbili kubaki kwa mkulima. Kutokana na serikali kuwa sikivu tumetafuta kampuni nyingine ambazo zitanunua tumbaku yote," alisema.

"Kampuni hii ya British America itaingia mkataba na Chama Kikuu cha Ushirika (KACU), ili kuhakikisha mkulima wa tumbaku anapata fedha zake zote anapouza.

Naye Balozi Iddi aliwatoa wasiwasi wakulima wa mazao ya biashara nchini likiwamo zao la tumbaku na pamba kuwa serikali yao ni sikivu na itahakikisha haiwavunji moyo wakulima bali itaendelea kuwatafutia masoko na mazao yao yatanunuliwa yote.

Hata hivyo, aliwataka wakulima kuacha kuendelea kukata miti ovyo na badala yake wakate matawi ili mvua ziendelee kunyesha kwa wingi na kuendelea kuzalisha chakula cha biashara na kujiinua kiuchumi.

Kwa upande wake mkulima wa tumbaku kutoka Kata ya Ulowa, Hamisi Michael, alipongeza serikali kwa kuwatafutia kampuni nyingine ambayo itanunua zao hilo na kubainisha kuwa mpaka sasa ana tumbaku kilo 1,200 ambayo imekosa soko.

***Imeandikwa na Shaban Njia na Marco Maduhu***




Meneja wa Kiwanda cha TBL cha Ilala, jijini Dar es Salaam, Calvin Martin (wa pili kushoto), akikabidhi msaada wa vipuri vya magari kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Ilala, ASP Nyararo Otuma, kwa ajili ya matengenezo ya magari ya kituo hicho, ili kuimarisha ulinzi, katika hafla iliyofanyika kiwandani hapo jana. Wengine ni maofisa kutoka polisi na TBL. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi waonywa ujenzi, kilimo maeneo mabomba ya gesi, mafuta

**Na Agness Shayo,**
TUDARCO

JAMII imetakiwa kuacha tabia ya kujenga na kufanya shughuli za kilimo katika maeneo yaliyopitishwa mabomba ya mafuta na gesi, ili kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza na kuygharimu maisha yao ikiwamo majanga ya moto.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Masuala ya Jamii kutoka Kampuni inayojishughulisha na kuzalisha umeme kwa kutumia gesi (SONGAS), Nikodemasi Mwakapaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu matumizi bora ya gesi na mafuta.

Alisema baadhi ya wananchi wanayatumia sana maeneo ambayo yamepita mabomba ya mafuta na gesi, jambo ambalo linadaiwa kuwa ni uelewa mdogo kuhusu matumizi ya maeneo hayo, huku wengine wakifanya ukaidi ilhali wanajua madhara yanayoweza kujitokeza katika maeneo hayo kutokana na shughuli za kibinadamu wanazozifanya kikiwamo kilimo.

"Ukiachilia mbali wananchi, pia yapo baadhi ya kampuni ambazo nazo zimekuwa na kawaida ya kujenga katika maeneo hayo, pasipokufikiria hatari ambayo inaweza kutokea na kusababisha madhara kwenye jamii, hivyo tunawaomba wote waache mara moja, na kwa bahati nzuri mpaka sasa tumefanikiwa kudhibiti hali hii kwa asilia 21," alisema Mwakapa.

Aidha, alieleza kuwa kampuni hiyo imekuwa ikinunua maeneo inayopitisha mabomba yake, ili kuzuia watu kuchimba chimba maeneo hayo, lengo likiwa kupunguza uharibifu wa mabomba unaoweza kusababisha uchafuzi wa mazingira.

Aidha, aliwataka wananchi kuachana na matumizi ya kuni na mkaa ili kulinda mazingira yanayowazunguka, badala yake watumie njia mbadala ikiwamo gesi na kuondokana na tatizo la uchafuzi wa mazingira kwa kiasi kikubwa.

# Mkeremy aimwagia sifa TFS

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Brigedia Jenerali Mbaraka Mkeremy, amesema taasisi hiyo inafanya kazi kubwa kuhakikisha inasimamia rasilimali za misitu zilizopo ili ziwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Jenerali Mkeremy aliyasema hayo jana akiwa kwenye Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asili ya Kalambo ikiwa ni sehemu ya ziara yake ya kutembelea maeneo ya hifadhi za misitu na mashamba ya miti ya serikali.

Alisema uamuzi wa serikali kuupandisha hadhi msitu wa Kalambo kuwa msitu wa hifadhi ya mazingira asili ni jitihada za kuhakikisha maporomoko ya mto huo yanahifadhiwa na kusimamiwa ipasavyo.

Mwenyekiti huyo alisema ni wakati sasa kwa Watanzania kuanza kuwa na utamaduni wa kutembelea hifadhi hiyo ili kujionea maajabu ya maporomoko hayo.

"Eneo hili linavutia na zuri kwa utalii. Nitoe wito kwa Watanzania wakiwa katika siku za mapumziko na sikukuu kutembelea na kushuhudia maajabu ya maporomoko haya ambayo yameshatangazwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (Unesco) kuwa ni urithi wa dunia," alisema.

"Niwapongeze TFS kwa ujenzi wa ngazi zenye urefu wa mita 1,277 zinazoshuka hadi kwenye maporomoko haya yanayomwaga maji Ziwa Tanganyika. Nimeambiwa kuwa katika ngazi za kushuka chini kwenye maji kuna "view point" tatu. Ya kwanza unapotoka kwenye maji imepewa jina la "Kigwangala View Point". Napendekeza katika "view point" ya pili ambayo ni ya kwanza unapoteremka ngazi iitwe Dos Santos View Point (Kamishna Mkuu Uhifadhi wa Misitu) na ya tatu inayofuatia iitwe, "Mkeremy View Point," alisema.

Kwa upande wake, Profesa Silayo alisema TFS imeweka mikakati kadhaa katika kuhakikisha misitu yake inaingiza mapato ya kutosha kupitia huduma za utalii sambamba na kuuza mazao ya misitu.

Profesa Silayo alisema miongoni mwa mikakati hiyo ni kuvitangaza vivutio vya utalii ekolojia vilivyoko kwenye misitu ya mazingira asilia iliyo chini ya taasisi hiyo.

"Utalii ekolojia na biashara ya mazao ya misitu ni nyuki ni nguzo ya utendaji kazi wa taasisi yetu, tunafanya kila liwezekanalo kuimarisha maeneo ya maporomoko ya Kalambo ili kutusaidia kuongeza tija katika jukumu letu la ukusanyaji wa maduhuli ya serikali, kuongeza mauzo ya nje na fedha za kigeni kupitia huduma za utalii na uuzaji wa mazao ya nyuki," alisema.

Profesa Silayo aliwashukuru wananchi wa kata ya Mpimbwe kwa kukubali kutoa sehemu ya ardhi yao kwa ajili ya mlima wa Mpimbe ili iwe kiunganishi (corridor) kati ya msitu wa Maporomoko ya Mto Kalambo na Msitu wa Hifadhi wa Kalambo, ambao sasa umeunganishwa na kuwa Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asili.

# Elimu ya maboya vyombo vya usafiri yapewa mkazo

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

WAFANYAKAZI na wenye vyombo vya usafiri wa majini wametakiwa kuzingatia utoaji elimu kwa abiria kuhusu uvaaji na umuhimu wa maboya kabla ya kuanza safari.

Imeelezwa kuwa elimu hiyo iwe maalum kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kutambua namna ya kutumia vifaa hivyo endapo itatokea hitilafu au ajali wawapo majini wakati wakisubiria msaada.

Hayo yalielezwa na Ofisa Mfawidhi wa Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) Mkoa wa Mwanza, Patrick Mipawa, wakati akizungumza na Nipashe, na kusisitiza kuwa suala la uvaaji wa maboya ni jukumu la kila mmoja anayetumia usafiri wa maji ili kuokoa maisha yake.

Aliongeza wafanyakazi na wenye vyombo hivyo wanapaswa kuwaelimisha abiria namna ya kuyatumia kabla ya kuanza safari pamoja na kuwapatia mara tu mtu anapopanda usafiri huo.

"Umuhimu wa maboya ni kwa ajili ya kusaidia 'kusave' maisha ya watumiaji wa vyombo vya majini, vyombo vyetu vimegawanyika katika maeneo makubwa mawili, vyombo vidogo vya majini ambavyo vipo na urefu wa mita 24 kwenda chini ambavyo tunasema vyombo hivyo mtu anatakiwa mara tu anapopanda apewe boya na avae kwa usahihi," alisema Mipawa.

"Isipokuwa kwa meli kubwa ambazo ni zaidi ya mita 24 hizo kwa sababu zinakuwa na vifaa vya kutosha vinanyotoa alama wakati wa dharura zinaweza kutoa ishara na zinakuwa na muda wa kutosha kwa ajili ya maandalizi, wao watafuata maelekezo ya nahodha wa chombo ni wakati gani wavae maboya," alisema Mipawa.

Aidha, Mipawa aliwataka watumiaji wa usafiri wa vyombo vya majini kuzingatia matumizi ya maboya mara tu wanapoingia katika vyombo hivyo ili kuokoa maisha endapo chombo kitapata hitilafu ingali majini.

"Endapo mtumiaji yeyote wa usafiri wa majini hajaelewa namna ya kufunga au kutumia boya hilo ni wajibu wake kuwauliza wafanyakazi wa chombo husika ili waweze kumwelekeza kwani ni haki yake kueleweshwa kwa kupata maelezo sahihi," alisema.

Mipawa alisema Tasac imekuwa ikitoa elimu ya uvaaji maboya kupitia mikutano ya hadhara pamoja na mtu mmoja mmoja hasa maeneo ya visiwani.

Mkuu wa Kitengo cha Polisi Wanamaji Mkoa wa Mwanza, Inspekta Wenceslaus Muchunguzi, alisema Tasac na Polisi wamepewa jukumu la kusimamia masuala ya usafiri majini ikiwamo kudhibithi utumiaji wa maboya, hivyo kabla ya kuingiza chombo ziwani lazima wakague kama wana vifaa hivyo.

"Jeshi la Polisi jukumu lake kubwa ni kulinda mali na usalama wa raia, hivyo katika masuala ya usafiri wa majini tunashirikiana na Tasac kuelimisha watu hususan wavuvi namna ya uvaaji maboya na umuhimu wake ambao ni kusaidia, kuokoa uhai panapotokea ajali, kwa siku tatu tulikuwa Wilaya ya Sengerema katika mwalo wa Kijiweni, Kisiwa cha Juma na maeneo mengine kutoa elimu kwa kushirikiana na Tasac, Polisi na Ofisa Uvuvi Mkoa," alisema Muchunguzi.

Alisema, kila miezi mitatu wanapaswa kutoa elimu kwa watu kuhusu suala zima la maboya licha ya kuwa vifaa hivyo vimekuwa vikizeeka na kupoteza ubora wa kusaidia kuokoa watu hivyo yanapaswa kubadilishwa kila mwaka.

Mmoja wa wakazi wa Jiji la Mwanza Rosemary Lukinga, alisema elimu ya uvaaji maboya bado haijawafikia watu kwa usahihi, hivyo aliiomba mamlaka husika kutilia mkazo kwa kuhakikisha kila chombo kabla ya kuanza safari kinatenga nusu saa kwa ajili ya kuelimisha abiria.



Fundi sanifu wa maabara ya Hospitali ya Halmashauri ya Kasulu, Tiracy Mbombo ambaye anakabiliwa na mashtaka kadhaa, akiwa amefícha uso wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma juzi. **PICHA: JOCTAN NGELLY.**

# Fundi sanifu akutwa na kesi ya kujibu

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Kigoma, imemwona mshtakiwa Tiracy Mbombo (42) mkazi wa Heru Chini, Wilaya ya Kasulu kuwa anakesi ya kujibu baada ya upande wa mashtaka kufunga ushahidi wao.

Mshtakiwa huyo ni fundi sanifu wa maabara ya Hospitali ya Halmashauri ya Kasulu Mji.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Flora Mtarania, kwa ajili ya uamuzi mdogo ambapo mahakama hiyo baada ya kuangalia ushahidi uliyotolewa na upande wa mashtaka umeonyesha kuwa mshtakiwa huyo ana kesi ya kujibu na mahakama hiyo ilimtaka mshtakiwa huyo ajitetee.

Mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashtaka mawili ya wizi wa vitu mbalimbali vya Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kasulu vyenye thamani ya Sh. 47,314 pamoja kughushi sahihi ya geti la kuingilia wageni kwamba aliyetakiwa kusaini hayupo wakati akijuwa ni uongo.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Antia Julius, alieleza kuwa upande wa mashtaka umefunga ushahidi wao na kusubiri uamuzi mdogo wa mahakama hiyo kama mshtakiwa huyo ana kesi ya kujibu au la.

Baada ya upande wa mashtaka kumaliza kutoa ushahidi wao, Hakimu Mtarania alitoa uamuzi mdogo kuwa baada ya Mahakama kusikiliza mashahidi saba wa upande wa mashtaka pamoja na vielelezo vitatu, imeona mshtakiwa huyo anayo kesi ya kujibu, na kumtaka mashtakiwa huyo ajitetee.

Wakili wa utetezi, Ignatus Kagashe, alidai kuwa mteja wake atajitetea kwa kiapo pia atakuwa na vielelezo viwili.

Hakimu Mtarania aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 25, mwaka huu kwa ajili ya kusikiliza utetezi wa mshtakiwa huyo.

# NIDA yapewa somo utoaji vitambulisho

**Na Elisante John,** SINGIDA

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imetakiwa kuboresha huduma zake sambamba na kutoa elimu kwa jamii, ili kuondoa majibu yenye utata yanayotolewa na baadhi ya wasimamizi wake.

Baadhi ya malalamiko ya wananchi dhidi ya baadhi ya watumishi wa mamlaka hiyo ni kupewa majibu kuwa vitambulisho vimechelewa kuwafikia wananchi kunatokana na picha walizopigwa awali kuungua.

Majibu hayo yamedaiwa kuwasababisha viongozi usumbufu, na hata msongamano usiokuwa wa lazima katika ofisi za Nida.

Hayo yalielezwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Singida, pamoja na mambo mengine, kuzungumzia kero za wananchi kutumia muda mwingi, kwa ajili ya kufuatilia na kuulizia vitambulisho vyao, katika ofisi za Nida.

Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, Justine Monko na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Eliya Dighah, walisema kupitia mikutano waliyoifanya vijijini, jamii imeonyesha kukerwa na hali hiyo, hivyo Nida kutakiwa kulimaliza suala hilo. Alisema maelekezo yanayotolewa na watendaji wa vijiji na kata vijijini, inadhihirisha wazi baadhi yao hawaelewi maelekezo ya Nida, hivyo kutoa majibu yenye utata kwa wananchi, jambo ambalo limekuwa linazalisha majibu yasiyo sahihi.

"Taarifa za wananchi tayari Nida wanazo, hili suala hata mimi lilinisababishia usumbufu nikalazimika kuwasiliana na katibu tawala wa wilaya, akanipa watu wa Nida wakanieleza vizuri tu...nadhani maelezo haya ni mazuri, naomba tukawaelekeze wananchi, ili wasiendelee kupata usumbufu," alisema Monko.

Ofisa wa Nida Mkoa wa Singida, Edigar Faraja, alisema mamlaka hiyo ingependa kuwa na ofisi kila kata na tarafa, lakini kutokana na suala hilo kuwa la kisheria zaidi, inawawia vigumu kufungua.



# Polisi wakusanya mil. 500/- siku tatu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

POLISI Mkoa wa Arusha wamekusanya faini zaidi ya Sh. milioni 500 kwa siku tatu, zinazotokana na ubovu wa magari 1,900 katika operesheni maalum ya kukagua magari ya kubeba abiri na wanafunzi.

Operesheni hiyo ni utekelezaji wa agizo la Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, alilolitoa Agosti 16, mwaka huu, alipozungumza na polisi wa kikosi wa usalama barabarani na maofisa wa jeshi hilo mkoani hapa.

Katika agizo hilo, Gambo alitoa siku 14 kwa polisi kufanya operesheni maalum ya kukagua magari ya abiria na yale yanayobeba wanafunzi na usajili wa madereva wa pikipiki na teksi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, Mary Kipesha, alisema operesheni hiyo ilianza Agosti 17 kwa mabasi yanayokwenda mkoani pamoja na daladala.

Kipesha alisema katika operesheni hiyo, walibaini mabasi mengi yanayokwenda mikoani yalikuwa na kasoro mbalimbali lakini pia daladala, maarufu kama Haice, nyingi walizozikagua zilikuwa hazina sifa ya kubeba abiria.

Alisema katika operesheni hiyo, pia walibaini kwamba magari mengi yalikuwa yametozwa faini kutokana na makosa mbalimbali, lakini wamiliki walikuwa hawajalipa wala kurekebisha kasoro kwenye magari yao, hali iliyowalazimu kuwaamuru kulipa faini hizo mara moja.

"Agizo la mkuu wa mkoa limekuwa na tija kubwa kwa sababu tumebaini kwamba magari mengi ya kubeba abiria yalikuwa mabovu, hali ambayo ingeweza kuhatarisha maisha ya abiria wanaotumia vyombo hivyo vya moto," alisema na kuongeza:

"Kutokana na kasoro hizo, magari hayo tumeyapiga faini lakini pia tumewataka wamiliki kulipa faini hizo mara moja na madereva kuendelea kutii sheria za barabarani ili kuepuka ajali zisizo za lazima," alisisitiza.

Kuhusu ukaguzi wa magari ya wanafunzi, Kipesha ambaye ana wiki mbili tuu jijini hapa, baada ya kuchukua nafasi ya Joseph Bukombe, ambaye uteuzi wake ulitenguliwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alisema magari mengi ya wanafunzi yanabeba idadi kubwa ya wanafunzi kinyume cha sheria, lakini pia ni mabovu hali ambayo inaweza kuhatarisha maisha ya wanafunzi.

Kutokana na hali hiyo, Kipesha amepiga marufuku magari ya wanafunzi kubeba idadi kubwa ya wanafunzi na kwamba dereva atakayebainika kufanya hivyo, atachukuliwa hatua za kisheria.

"Operesheni hii ni endelevu tutaendelea kuwakamata madereva wote wanaokiuka sheria za barabarani, haswa wa daladala wanaokatisha safari walizosajiliwa nazo (ruti). Askari wa usalama barabarani hatuko tayari kuona dereva anavunja sheria wakati amebeba abiria. Tutahangaika naye ili iwe fundisho kwa madereva wengine," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya madereva wa mabasi yanayokwenda mikoani, Juma Rashid alipongeza hatua hiyo ya polisi kufanya ukaguzi maalum kwa kuwa kuna baadhi ya mabasi hayana sifa za kubeba abiria, kutokana na ubovu na wakati mwingine huharibikia njiani na abiria kupata usumbufu mkubwa, huku wakiwa hawarudishiwi nauli zao.




Mwendesha guta akiwa amepumzika kwenye makutano ya Barabara ya Sam Nujoma na Igesa, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuendelea na safari ya kusafirisha mzigo wa mkaa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# DC Simanjiro atoa onyo kali mangariba

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro, Mhandisi Zephania Chaula, ametoa onyo kali kwa wanawake mangariba katika wilaya hiyo, wanaondelea na mchezo wa kukeketa watoto wa kike.

Amesema mangariba wote watakaobainika kuendelea na tabia hiyo ambao kwa sasa wameanzisha mbinu mpya ya kuwakeketa wakiwa na umri mdogo kabla ya kuanza shule, watachukuliwa hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa mangariba wengine wenye tabia kama hiyo.

Chaula alitoa onyo hilo jana, wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Terrat wilayani humo na kudai kwamba hataki tena kusikia taarifa za matukio ya kukeketa watoto wa kike katika wilaya hiyo.

"Kuanzia sasa sitaki tena kusikia taarifa za ukeketaji kwa watoto wa kike. Wafikishieni salamu hao mangariba kwamba tumeshabaini mchezo wao wa kukeketa watoto wadogo. Mangariba tutakaowabaini tutawachukulia hatua kali za kisheria, ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia kama hizo," alisema.

Kwa mujibu wa Chaula, ukeketaji ni shughuli haramu ambayo haipaswi kufanyika kabisa hapa nchini, lakini kuna baadhi ya wazazi wanashirikiana na mangariba kwa madai ya kudumisha mila potofu ambazo hazikubaliki kisheria.

Chaula alitumia fursa hiyo kuwataka mangariba hao kuachana na shughuli za ukeketaji na badala yake wajiunge kwenye vikundi na kufanya shughuli za ujasiriamali, ili wabaki salama kwa sababu kwa sasa serikali inafuatilia kwa karibu ili kukomesha vitendo hivyo ambavyo ni ukatili wa kijinsia.

Aidha, aliwataka mangariba hao kusalimisha visu na zana zote wanazotumia katika shughuli hiyo haramu, kwa kuwa serikali itaanza mpango maalum wa kuwabaini mangariba hao wanaofanyia watoto wa kike vitendo vya ukatili.

"Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro inatoa mikopo kupitia vikundi vya wanawake na vijana na watu wenye ulemavu. Ninyi mngariba acheni biashara haramu ya kukeketa watoto jiungeni kwenye vikundi na kuvisajili, ili mpate mikopo isiyo na riba kwa sababu tukiwakamata hamtabaki salama," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya ambaye alionekana kukerwa na vitendo hivyo, alisema hizo ni mila potofu ambazo zimepitwa na wakati na zinasababisha watoto wengi wa kike kutokwa na damu nyingi, wakati wakukeketwa na wakati mwingine kupoteza maisha.

Diwani wa Terrat, Jackson Ole Materi, alisema katika kata hiyo wakati wa mikutano mikuu ya vijiji, wamekuwa wakitoa elimu kwa mangariba hao kuacha kukeketa watoto wa kike na madhara ya ukeketaji.

Ole Materi alisema kupitia kauli ya mkuu wa wilaya hiyo, anatarajia wanawake hao, wataachana na tabia hiyo ambayo ilikuwa imekithiri kwa jamii hiyo ya kifugaji.

# Upelelezi kesi ya uhujumu dhidi ya hakimu wakamilika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

UPELELEZI wa kesi ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi inayowakabili washtakiwa watano, akiwamo Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Bernad Nganga, Mwanasheria wa Hifadhi za Taifa (Tanapa), Maneno Mbunda, na Mwanasheria wa Serikali Fortunatus Mhalila, umekamilika.

Licha ya tuhuma hizo, washtakiwa pia wanakabiliwa na mashtaka mengine tisa. Mbali na washtakiwa hao, wengine ni Nelson Kangero na Tumaini Mdee.

Akizungumza jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Abiud Bwegogwe, Mwanasheria wa Serikali Upendo Msuya, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na anaomba terehe nyingine kwa ajili ya kuwasomea maelezo ya awali.

Baada ya maelezo hayo, mawakili wa utetezi wakiongozwa na Elibariki Maeda akisaidiwa na Valentine Nyalu na Fridolin Bwemelo, waliiomba mahakama hiyo kuondoa mahakamani hapo hoja walizokuwa wameziwasilisha.

Agosti Mosi, mwaka huu, mawakili hao walidai mahakamani hapo kuwa notisi ya serikali namba 296/2012 inaelekeza kesi zisifunguliwe kabla ya upelelezi kukamilika, hivyo ni vyema upande wa Jamhuri ukaondoa mahakamani hapo mashtaka yanayowakabili wateja wao ambayo upelelezi haujakamilika.

Walidai hivyo kwa madai kwamba wateja wao wamekaa mahabusu zaidi ya siku 60 na watatu kati yao ni watumishi wa serikali ambao wanaendelea kulipwa mishahara na kula chakula cha bure gerezani na kuisababishia serikali hasara ya kupokea mishahara bila kufanya kazi yoyote.

Baada ya maombi hayo, Hakimu Bwegogwe alikubali ombi hilo kuiondoa hoja hiyo kisha kuahirisha kesi hiyo hadi Septemba 3, mwaka huu, ambapo washtakiwa watasomewa maelezo ya awali.

Mapema, washtakiwa hao walipofikishwa mahakamani hapo Mei 6, mwaka huu, Mwanasheria Mwandamizi wa Serikali, Javelin Rugahuruza, akisaidiana na mawakili waandamizi wa Shedrack Kimaro na Theophil Mutakyawa, waliwasomea washtakiwa hao mashtaka 11 yakiwamo ya kujihusisha na rushwa, kughushi na kujipatia mali kwa njia ya rushwa kati ya Juni Mosi, 2018 na Aprili 15, mwaka huu katika maeneo mbalimbali.

Mashtaka mengine waliosomewa waliyotenda katika kipindi hicho ni kuchukua rushwa ya Sh. milioni 31.5 toka kwa Kangero, utakatishaji wa Sh. milioni 31.5, kughushi nyaraka za uongo za nyara ya serikali za kilo 15 za meno ya tembo ya Sh. milioni 9.8.

# Ukaguzi fedha za vijiji waiva

**Na Godfrey Mushi,** SAME

SERIKALI imempa siku 14 Mkaguzi wa Ndani wa Halmashauri ya Wilaya ya Same, kuanza operesheni maalum ya ukaguzi wa fedha za umma kwenye vijiji vyote, kabla ya wenyeviti wa vijiji kuachia ngazi kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, aliagiza juzi kuwa hadi Agosti 30, mwaka huu, vijiji ambavyo havijasoma taarifa ya mapato na matumizi viwe vimekamilisha ili kusubiri ukaguzi rasmi wa serikali.

"DED (Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri), naagiza mkaguzi wa ndani akafanye ukaguzi katika vijiji vyote na nipate ripoti yake ndani ya wiki mbili kuanzia sasa. Lakini pia elekeza kwa barua, vijiji vyote visome mapato na matumizi kabla ya tarehe 30.

"Nataka hilo lifanyike kabla wenyeviti hao hawajatoka madarakani ili wasijeondoke na fedha au michango ya wananchi. Nasema hilo kwa sababu nimekutana na kero nyingi zinazohitaji utatuzi wa haraka, baada ya kwenda kuzungumza na wananchi katika Kijiji cha Mhero kule Kata ya Chome," alisema.

Alisema tabia ya kusomwa kwa taarifa hizo kwa wananchi kila kipindi cha robo ya mwaka, kuna sababisha migogoro ambayo huwafanya wananchi wakati mwingine kugoma kushiriki shughuli za maendeleo kama kuchangia miradi mbalimbali kwa kuhofia fedha zao kutafunwa.

Alisema migogoro mingi ya kifedha katika serikali za mitaa imekuwa ikijitokeza kutokana na viongozi wao kutowasomea wananchi mapato na matumizi.

Alipotafutwa mtaalamu wa mradi wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS) katika mkoa wa Kilimanjaro kutoa ushauri wake kuhusiana na zoezi hilo, Veronika Shao alisema ipo haja kwa serikali kufanya tathmini ya thamani ya fedha kwenye shughuli mbalimbali zinazofanywa kwenye vijiji kwa kutumia rasilimali za umma.

Shao ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kiraia la Kinshai, alisema ili kupata ufumbuzi wa kudumu utakaoondoa kasumba hiyo, ni lazima kufanyika kwa tathmini ili kuongeza kasi ya kuheshimiwa kwa utawala bora na uwajibikaji.

# Chadema yawajibu madiwani wa CCM

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VIONGOZI wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ambalo linaongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), wamejibu mapigo kuhusu shutuma zinazoelezwa na wapinzani wao, CCM, kwamba kuna mpango wa kutumia mamilioni ya shilingi kwa ajili ya ununuzi wa kompyuta ndogo za mkononi maarufu kama 'Ipad' ili kuwafurahisha madiwani.

Akitoa ufafanuzi kuhusiana na shutuma hiyo jana, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Michael Kilawila, alisema ununuzi wa 'Ipad' hizo hauepukiki.

"Kwanza kwenye kamati tunapitia na kupendekeza na mwisho hoja inakwenda kwenye Baraza la Madiwani ili kupata baraka. Mimi mwenyekiti, sina mamlaka ya kufanya ya kuhamisha fedha yoyote ya halmashauri bila kupitia baraza hilo.

"Wanaolalamika ni wale wanaopenda kujilimbikizia miradi mingi kwenye maeneo yao. Tukienda sasa kwenye uamuzi wa baraza wa kujigeuza kutoka kwenye analogia kwenda kwenye dijitali hakuepukiki," alisisitiza.

Akionyesha kutofurahishwa na shutuma hizo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Exaud Mamuya, alisema si kweli kwamba wamepanga kutumia Sh. milioni 104 kununua Ipad, bali fedha iliyotengwa kwa ajili ya kompyuta hizo ni Sh. milioni 19.8.

"Hayo malalamiko yao hayana msingi kwa sababu Ipad zitakazonunuliwa ni 66 ambazo zitakuwa ni za waheshimiwa madiwani 46 na wataalamu 20 ambazo kila moja ni Sh.300,000," alisema.

Wiki iliyopita, Madiwani wa CCM, Morice Makoi (Okaoni), Deo Mushi (Kibosho Magharibi), Kamili Mmbando (Kahe Mashariki), Bertin Mkami (Uru Shimbwe) na Anna Lyimo (Kilema Kaskazini), waliamsha zogo hilo kila mmoja akipinga ununuzi huo wa Ipad, badala ya fedha itakayotumika kuelekezwa katika ukarabati wa barabara.

Diwani wa Okaoni (CCM) na Mwenyekiti wa zamani wa halmashauri hiyo, Morice Makoi, alinukuliwa akisema: "Bado miezi 10 madiwani waondoke madarakani, katika halmashauri yetu kuna baadhi ya vyoo vimeanguka, zahanati hazina umeme, leo kuna watu wanachukua milioni 104 wanaamua kwenda kununua Ipad na kununua viti kwa ajili ya ukumbi, wakati viti vipo miaka yote tunakaa."




Meneja Mauzo wa Tigo Mkoa wa Kilimanjaro, Tryphone Kamugisha, pamoja na Kaimu Ofisa Mtendaji wa Mji Mdogo wa Mwanga, Hassan Msuya, wakikata utepe kuzindua rasmi mnara wa mawasiliano ya simu kwa huduma ya mtandao wenye kasi ya 4G Wilaya ya Mwanga, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# UWT kumpongeza JPM utekelezaji ilani

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, anatarajiwa kuongoza kongamano la Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoani Kilimanjaro, Agosti 24 mwaka huu, kwa ajili ya kumpongeza Rais John Magufuli kwa kutekeleza ilani ya chama hicho ya mwaka 2015-2020 kwa mafanikio makubwa.

Taarifa iliyothibitishwa na Katibu wa UWT mkoani Kilimanjaro, Mary Sulley, ilieleza kuwa katika uwanja wa Majengo Manispaa ya Moshi, jumuiya hiyo itakutana kumpongeza Rais Magufuli kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa ilani ya CCM katika kipindi cha miaka mitatu.

"Ni kweli, Spika wa Bunge ndiye anayekuja kunguruma katika kongamano letu la kumpongeza Rais Magufuli kwa kufanikiwa kutekeleza ilani ya uchaguzi kati ya mwaka 2015 na 2019. Watanzania ni mashahidi kwa mambo makubwa ya maendeleo kwa taifa letu yanayofanywa na serikali hii ya awamu ya tano, sasa Ndugai ndiye mgeni wa heshima siku hiyo," alisema.

Moja ya miradi mikubwa nchini inayompa heshima Rais Magufuli ya kukumbukwa ni utekelezaji wa mradi wa umeme wa maporomoko ya maji ya Mto Rufiji (RHPP) unaojengwa na Kampuni ya Arab Contractors kwa pamoja na Elsewedy Electric zote kutoka Misri. Mradi una uwezo wa kuzalisha megawati 2,115.

Mingine ni mradi wa reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, kukamilika kwa ujenzi wa jengo la tatu la abiria la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), ununuzi wa ndege mpya za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), ufufuaji wa reli ya kaskazini iliyokufa miaka 12 iliyopita, ujenzi wa miundombinu ya barabara za lami, madaraja makubwa na elimu bure.

Katika kipindi hicho, Rais Magufuli amesimamia misingi ya uchumi pamoja na changamoto kadhaa zinazoikumba uchumi wa dunia na hata ukanda wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, akieleza mafanikio hayo, alisema: "Huwezi kuongelea kukua kwa uchumi bila kuangalia vijenzi muhimu vya kuashiria ukuaji wa uchumi, mambo ambayo Rais Magufuli ameyafanya zaidi ni kuhahakikisha mapato ya serikali yanakua, ameziba mianya ya upotevu wa mapato na kuongeza ukusanyaji wa kodi ya serikali, hivyo ni lazima apongezwe.

Pia katika kuhakikisha anapambana na rushwa na ufisadi, alisema Rais Magufuli alianzisha Mahakama ya Mafisadi (makosa ya uhujumu uchumi) ambayo ilianza kazi rasmi Julai, 2017.

ama
ALHAMISI AGOSTI 22, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



**Raia Uganda ateuliwa kuongoza UNAIDS**


Ukurasa 17



MWEZI WA UNYONYESHAJI

Benki yaandaa chumba, wazazi kunyonyesha wakiwa kazini

Ukurasa 20



Ukurasa 14

**Vijana wapaa kwa kilimo 'haidroponiki'**



KOLOKOLO DOMOREFU

# NDEGE ADIMU DUNIANI, ATISHIWA KUTOWEKA

Ukurasa 16



# Chanjo ugonjwa wa zinaa yapita awamu ya kwanza

CHANJO ya kuwakinga watu dhidi ya magonjwa ya zinaa imepita uchunguzi wa kwanza wa kiusalama.

Ni ya kwanza kupita majaribio kwa binadamu.

Wataalamu wanasema chanjo hiyo ndiyo njia bora ya kukabiliana na ugonjwa wa Chlamydia, ambao unachangia karibu ya nusu ya maambukizi ya magonjwa yote ya zinaa nchini Uingereza.

Uchunguzi zaidi unapendekezwa kufanywa ili kubaini jinsi chanjo hiyo inavyofanya kazi na itolewe kwa kiwango gani, linasema jarida la Lancet la magonjwa ya kuambukiza.

Majaribio hayo yatachukua miaka kadhaa kubainishwa lakini kwa sasa wataalamu wanapendekeza njia bora zaidi ya kujikinga na maambukizi ya chlamydia ni kutumia mipira ya kondomu.

CHLAMYDIA NI NINI?

Ni ugonjwa unaoambukizwa kupitia bakteria inayomwingia mtu anayefanya ngono bila kinga (hata bila kumwingilia mtu).

Bakteria ya chlamydia huishi katika mazingira ya maji maji yanayopatikana kwenye manii ya wanaume na katika sehemu ya siri ya mwanamke.

Mara nyingi mtu aliyeambukizwa haonyeshi dalili zozote na ndio sababu watu huutaja ugonjwa huo kuwa ugonjwa wa "siri."

Usipotibiwa kwa kutumia antibiotiki, unaweza kusababisha madhara makubwa yatakayoathiri kizazi cha mwathiriwa.

Watu walio chini ya miaka 25 ambao wanapendelea kufanya ngono, wanashauriwa kufanya vipimo vya chlamydia kila mwaka.

Huduma ya Afya ya Kitaifa (NHS) nchini Uingereza, inatoa huduma ya uchunguzi bila malipo.

Watu pia wanaweza kujifanyia uchunguzi binafsi kwa kununua vifaa maalum vilivyoidhinishwa kutoka kwa maduka ya kuuza dawa. **BBC**

## MAZINGIRA

# Vijana wapaa kwa kilimo 'haidroponiki'

**Na Faustine Feliciane**

KWA miaka mingi kilimo kilifanyika kwa mazoea, tena hofu ya kulinda mazingira haikuwa kubwa kama ilivyo sasa.

Tofauti na zama hizo kilimo kilipofanyika bila tahadhari hasa kuangalia usalama wa mazingira, siku hizi changamoto mbalimbali zikiwamo mabadiliko ya tabianchi zimehamasisha wakulima kutumia teknolojia ya kisasa.

Ndiyo maana enzi hizi zinashuhudia teknolojia ya kisasa kwenye uzalishaji ambayo imeibua masuala mengi ikiwamo kulima bila kupanda mimea kwenye ardhi pamoja na kuzalisha bila kuharibu tabaka la udongo.

Kilimo hiki kiitwacho haidroponiki kinatajwa kuwa na tija zaidi na chenye walaji wengi walioko nje ya mipaka.

Hivi karibuni Nipashe ilikitembelea kikundi cha vijana wa kituo cha Green Fish, cha Kitunda jijini Dar es Salaam, hao wamejiajiri kwenye ufugaji wa samaki na kilimo cha kisasa pasipokutumia udongo.

**HYDROPONIC NI NINI?**

Kwa mujibu wa taarifa za mtandao ni utaalamu wa kuotesha mazao bora yenye tija kwa muda mfupi zaidi bila kutumia udongo, mbinu inayotumia maji na virutubisho viitwavyo hydroponic nutrients ambavyo pia ni vimiminika vinavyofyonzwa na mimea hiyo.

Kilimo hiki huanza na kuchagua mbegu ambazo hazijachipua, ambazo hulowekwa ndani ya mchanganyiko wa maji na chlorine kwa saa chache ili kuzuia zisivunde ua vimelea kuota juu yake.

Baada ya hapo mbegu hulowekwa kwenye maji, kisha kuoshwa na kulowekwa kwenye majisafi kwa siku nzima au saa 24 mchakato unaoziwezesha kufyonza maji vema.

Mbegu hizo hupandwa kwenye treyi au eneo lingine linalokubalika kitaalamu ambazo chini lina matundu kuwezesha maji kuingia na kutoka.

Katika mahojiano na Nipashe, Mkurugenzi wa kituo hicho, Ambwenisye Mwakyombe, anaweka wazi namna ambavyo ufugaji wa samaki na kilimo cha kisasa pasipokutumia udongo kinavyowapa tija.

"Uwekezaji huu umesaidia sana kutuwezesha vijana kupata elimu na mafunzo ya kilimo na stadi za kazi." Anasema Mwakyombe.

Aidha, Mwakyombe, anaeleza kuwa mbali na kufanya kilimo hicho, pia wana utaalamu na teknolojia ya kuandaa wenyewe mbegu katika maabara maalum kabla ya kuzipeleka mashambani.

> "Samaki wote tunapata masoko, na zaidi ni mboga ambazo tuna oda nyingi kiasi kwamba kampuni yetu haina uwezo wa kuzalisha kiwango kinachoitajika kwa wateja wetu," anasema Mwakyombe.

"Sisi tunafanya kilimo kisichotumia udongo huitwa hydroponic, mbegu zetu tunaziandaa kwa kutumia mabaki ya nazi baada ya kuifua na tunatumia maji, mbolea, mwanga na kishikizo (pressure) tu," anasema Mwakyombe.

Anafafanua kuwa kilimo hicho kimewapa tija kwa kuwa wanatumia eneo dogo kulima mazao mengi yanayowapatia pesa za kutosha huku pia wakitoa elimu kwa vijana wengine ambao wanakuja kujifunza namna ya kufuga samaki na kilimo hicho cha hydroponic.

Mwakyombe anasema:

"Kilimo hiki kinafaida kubwa ukilingaisha na kilimo cha kawaida cha kutumia udongo na mashamba makubwa. Vijana wana fursa nyingi za kujitengenezea pesa, kikubwa ni kujituma na kutafuta njia sahihi, hiki kilimo kina faida kubwa licha kutumia muda mfupi katika kuotesha mpaka kuvuna, pia huitaji kupalilia kama ilivyo kwenye kilimo cha kupanda mimea kwenye udongo."

Anasema kwenye kampuni yao ya Green Fish wanafuga samaki aina ya kambare na sato pamoja na kilimo cha mboga jamii ya 'letusi'.

"Samaki wote tunapata masoko, na zaidi ni mboga ambazo tuna oda nyingi kiasi kwamba kampuni yetu haina uwezo wa kuzalisha kiwango kinachoitajika kwa wateja wetu," anasema Mwakyombe.

Hivi karibuni kwa mujibu wa maelezo yake wamepata oda za kukusanya tani 20 za mboga kwa ajili ya kupeleka nje ya nchi, lakini hawajafikia uwezo wa kuzalisha kiwango hicho kikubwa cha tani hizo.

Anawahimiza vijana wachangamke fursa zipo na hiyo ni mojawapo , kutokana na kuwa na wateja wengi wameamua kutoa mafunzo kwa vijana wengine waende kuzalisha kwa sababu soko lipo kubwa tena nje ya nchi.

Aidha, mtaalamu wa ufundi na teknolojia wa kampuni hiyo, Daniel Myovela, anasema kilimo hicho kinatoa nafasi kwa mmiliki wa shamba au wafanyakazi kupata taarifa ya shamba lake kupitia simu yake ya mkononi.

Anasema mfumo huo wa kompyuta umeunganishwa kwenye shamba ambapo unatoa taarifa ya kila kinachoendelea kwenye shamba na kumpa taarifa mkulima kila wakati anapohitaji.

"Mfumo huu unamjulisha mwenye shamba taarifa mbalimbali, kwa mfano inapotokea maji yameisha au mwanga ndani ya shamba umekuwa mdogo au hata kukiwa na hali ya hewa ambayo si rafiki na mmea, taarifa inatumwa na hapo mwenye shamba anaenda kurekebisha hiyo hali," anasema Myovela.

Anaeleza kuwa zipo mboga ambazo zinahitaji baridi shambani na mwanga, hivyo kwenye shamba hilo wamefunga feni na kuweka taa.

Anasema kitu pekee ambacho kinaweza kuwa kikwazo kwenye uendeshaji wa shamba hilo ni mtaji, lakini suala la masoko ni kubwa na kilimo chake kina tija zaidi.

"Kikubwa mkulima anapaswa kuchagua zao moja na kujikita kwenye kulizalisha ataona faida yake, wakulima wengi wanakosea jambo moja, utakuta mtu anajihusisha na mazao tofauti na ya aina mbalimbali bila kujua lipi hasa ndilo zao lake la biashara, ukiwa na zao moja maalum kwa mkulima itamsaidia kuligharamia na kuona faida yake," anasema.

Mkurugenzi Mwakyombe, anaeleza kuwa kazi za kampuni yao zina mkono wa serikali na kwamba uimara wa kampuni yao umechangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ambayo imetoa mchango mkubwa kwao mpaka kufikia hatua ya mafanikio.

Anasema serikali hiyo imewapatia mkopo na kuhakikisha kuwa wanafanya uwekezaji wenye tija.



Kilimo cha mboga kinachofanyika kwenye mabomba au treyi zinazohifadhi na kupitisha maji kiitwacho hydroponiki ni teknolojia ya kisasa isiyotumia udongo kuotesha mazao. Pichani mboga jamii ya letusi zilizozalishwa kwenye bustani maalumu isiyo na udongo. **PICHA :MTANDAO.**

MAZINGIRA

Na Gaudensia Mngumi

## KOROSHO HIZI...

# Tishio afya wanawake, watoto

PENGINE mtu anaposikia utajiri wa korosho unatishia afya, atahusisha hali hiyo na matumizi ya viuatilifu na kemikali za sumu kuzalisha zao hilo.

Lakini sivyo ni unyanyasaji na ufukuzaji wanawake na kutelekeza watoto wakati wa mavuno ya korosho maarufu kama 'safisha ghala' unaofanywa na wanaume wanapouza korosho unavyowaweka wanawake na watoto katika hali mbaya kiafya ya mwili na akili.

Kwa hiyo si matumizi ya dawa wala mbolea za viwandani kukuza korosho bali ni ukatili unaofanywa baada ya wanaume kujaza fedha za korosho mifukoni kila mwaka katika maeneo mengi ya mkoa wa Mtwara.

Safisha ghala ni mambo ya siku nyingi ambayo pamoja na kuwasababisha maradhi ya kisaikolojia na kimwili wanawake, huwaumiza watoto wanaotishiwa na lishe duni na hata mimba za utotoni kwa mabinti.

Hayo yanaibuka hivi karibuni wakati wanahabari na maofisa wa Shirika la Kimataifa la Action Aid Tanzania (AATZ) walipotembelea wilaya za Tandahimba na Newala mkoani Mtwara.

AATZ inashirikiana na jamii za Newala na Tandahimba kwenye sekta za elimu, kuboresha kilimo na kuhamasisha usawa wa kijinsia na kuondoa unyanyasaji wanawake na watoto ili kuondoa umaskini.

Katika ziara hiyo wanawake wengi wamelalamikia unyanyasaji wakisema umewadhuru kiafya (akili na mwili).

### KWA VIPI?

Madhara ya unyanyasaji huo yanatajwa na waathirika kuwa yapo kisaikolojia kwa vile baadhi wanachanganyikiwa kwani hufukuzwa baada ya kuzalisha na kuuza korosho. Kwao ni kama kupokonywa tonge mdomoni au kukatazwa usiguse pesa ulizozitafuta kwa jasho lako.

Japo hawana takwimu za kutoka hospitalini wanasema wanawaona wenzao ambao pamoja na kuchanganyikiwa, huugua 'presha' ya kupanda au kushuka, hupata sonona na hata baadhi hurukwa na akili.

Amina Ali Kulaga, ni mama wa miaka 70, anayeeleza kuwa mwanawe ni mwathirika aliyeolewa na kufukuzwa muda mfupi baada ya fedha za korosho kupatikana.

Kulaga mkazi wa Kijiji cha Mnyawa Tandahimba, anasema kinachosababisha kufukuzwa ni kwa sababu wanaume wanaoa kiholela na kuacha kiholela bila udhibiti.

"Msichana anaolewa kimila hakuna hati ya ndoa. Wengi wanaoana mitaani hawaendi kufunga ndoa rasmi msikitini wala serikalini," anasema Kulaga.

Inakuwa rahisi kutimuliwa kwa vile hakuna nyaraka wala andiko la kisheria ni kimila, ndiyo ujanja wanaotumia wanaume hasa pale wanapowachoka wenza wao, anasema Kulaga, mkazi wa Kijiji cha Mnyawa kilichopo Tandahimba.

"Tunaathirika kisaikolojia kwa vile wanawake wengi wanachanganyikiwa na kufukuzwa baada ya kuzalisha ili wenzao wengine waolewe. Unaondolewa msimu huo mwenzako ale fedha ambazo ni jasho lako," anasema Mwajuma Konganika mkazi wa Mnyawa.

Aidha, anaeleza kuwa ukifika msimu huo si wanawake wala ndoa zinazothaminiwa

wanafukuzwa na wengi wanachanganyikiwa wasijue hatima, wakisumbuliwa na sonona kwa muda mrefu.

### NDOA ZA KIFURUSHI

Dharau na kejeli zinazojitokeza wakati wa mavuno ni wanaume kutamba kuwa wanaoa ndoa za kifurushi kama zilivyo vocha za simu.

"Kama wateja wa simu ndivyo na wanaume msimu wa kuuza korosho. Wanatamba kuwa huoa kwa siku, miezi au ndani ya msimu kulingana na matakwa na kutelekeza wanawake na watoto kwa jinsi wanavyotaka baada ya fedha kuisha," anasema Rukia Hamisi.

Anaungwa mkono na Mwajuma Asali, anayeongeza kuwa wanaume wakivuna ndiyo wakati wa kuwadharau wanawake mambo yanayofanyika kuanzia Oktoba hadi Januari mavuno yakiisha.

Rehema Chibwana ambaye mumewe kila akivuna korosho anahama nyumbani kwa miaka yote tangu walipofunga ndoa mwaka 1983, anasema ni jambo lililozoeleka na wanaume hawajali.

Wanawake ndiyo wanaopalilia, kufagia chini ili kuokota korosho na kuzipeleka sokoni hawagusi fedha.

### WATOTO

Athari kubwa zinazoambatana na matendo hayo ni pamoja na watoto kukwama kimasomo na kusababisha kuongezeka watu wasiojua kusoma na kuandika.

Lakini pia jamii yenye watoto walio na lishe duni na wadumavu wa akili na mwili.

Anayezungumzia suala hilo ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Namedi iliyoko Tandahimba, Joseph John, anayeeleza kuwa kutokana na matatizo ya familia kuvurugika wazazi wengi wanapoachana watoto nao husambaratika.

Anaeleza kuwa mara nyingi kinamama wakiachana na waume zao, wanawake huondoka na watoto na pale wanapohama kijiji huondoka nao hivyo kukosa masomo.

Mabinti wana hali mbaya zaidi kwa vile wanakosa wasimamizi na maelezo bora na baadhi hupatikana na ndoa na mimba za utotoni, anasema Mariam Bakari, Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Mnyawa.

Pia wazazi wanapoachana mara nyingi baba ndiyo wanaowahudumia kimahitaji lakini wanapowataliki wake zao, huduma kwa watoto inaondoka hivyo hukosa sare, vitabu na daftari, chakula nyumbani na shuleni na mwisho huacha shule.

Kukana watoto ni tatizo jingine wanawake wanapofukuzwa watoto wakienda kuomba mahitaji kwa baba zao wanawakana na kuwaambia hawajui na kuwataka kuwafuata wake zao jambo linaloathiri afya ya akili.

### KUNYANYAPAA NDOA

Sharafi Mung'wara ni miongoni mwa wanaume waliozungumzia sababu za kutelekeza wanawake, akisema baadhi ya jamii za wakulima wa korosho mkoani Mtwara hazikubaliani na ndoa kudumu.

Mkazi huyu wa Kijiji cha Mnyawa, anasema ndoa inapodumu muda mrefu jamii inainyanyapaa, mwanaume akiulizwa 'unaishi na mama yako, si mkeo' kwa kuwa umeishi naye sana.

Aidha, Mung'wara anaeleza kuwa jamii inapinga kudumu katika ndoa na wakati mwingine mwanaume analaumiwa kuwa amelishwa dawa za mapenzi, (umenywesha maji ya bendera).

Anaeleza kuwa maneno kama kuwaita wanaume kakakuona yanatumiwa kwenye unyanyasaji huo na kwamba mara nyingi kakakuona ni mnyama asiyeonekana na anapoibuka ni mara chache na anakuwa na ujumbe maalumu kwenye jamii.

Hivyo wanaume hao huonekana kama wamefichwa na kukaliwa kooni na wake zao, kwa mujibu wa maelezo yake.

### AINA ZA UNYANYASAJI

Wanawake wananyanyaswa kwa kauli mfano, umekuja hapa na nini? Baba yangu kafa kanirithisha mikorosho wewe umefiwa? Hivi unang'ang'ania hapa huna kwenu? Ondoka nyumbani kwangu.'

Lakini pia wanaume wanaona kuwa vurumai hizo zinatokana na wanawake kutothamini ndo, lakini kufurahia kuolewa kwenye harusi kubwa zenye magari mengi, bodaboda kwa wingi na zawadi zinazotolewa wakati wa kutunzwa na wanandugu na familia.

### VIONGOZI WA DINI

Bakari Litongolele ni Mwenyekiti wa Msikiti wa Pachoto ulioko wilayani Newala, akizungumzia tatizo hilo anasema hakuna sheria wala imani inayoruhusu kutelekeza watoto. Ni makosa na kwamba ni jambo lililoibuka miaka ya 1990 korosho ilivyopanda bei.

Litongolele (86) anasema licha ya jamii, viongozi wa dini na asasi za kiraia kuwahimiza watu kuacha safisha ghala vijana wengi ambao ni wahusika hawashiriki ibada, mikutano wala kufuatilia maelekezo ndiyo maana tatizo huendelea.

### JUHUDI ZA AATZ

Action Aid ni moja ya asasi za kimataifa zilizowekeza kukabiliana na unyanyasaji, kwa kuwahamasisha wanawake kudai usawa wa kijinsia, ushirikishwaji, kuwainua kiuchumi na kuwaunganisha katika makundi ya umoja.

Mratibu wa AATZ, Tandahimba na Newala Dinno Celestine, anakiri kuwa kuna talaka na ndoa holela nyingi zinazoathiri afya na uchumi wa wanawake.

Aidha, anasema baada ya kuliona hilo wanawaunganisha wanawake na kuanzisha asasi za Newala Women Rights Organisation (Newora) na Tandahimba Women Rights Association (Taworo).

Anasema kupitia umoja huo wanawake wametambua haki zao, wameanzisha vikundi ushirika na uwekezaji, vyama vya kuweka na kukopa vilivyoanzishwa na kuungwa mkono na Taworo na Newora pamoja na kumiliki mali ikiwa ni pamoja na ardhi na biashara.

Baadhi ya vikundi ni Tukazane na Upendo ambavyo wanawake wanabangua korosho, kutengeneza batiki, kuzalisha uyoga na pia wanamiliki mali hasa ardhi.

Aidha, Celestine anasema AATZ imesaidia kuanzishwa kamati za haki za wanawake vijijini.

Anasema iwapo juhudi hizo zitasimamiwa na kuimarishwa unyanyasaji huo utaondoka na hicho ndicho shirika hilo linachotaka kuona.



Wanawake wa Kijiji cha Mnyawa wilayani Tandahimba wakizungumzia na kuchambua athari za operesheni 'safisha ghala' inavyoumiza uchumi na afya za wanawake na watoto. **PICHA:GAUDENSIA MNGUMI.**

MAZINGIRA

KOLOKOLO DOMOREFU

# Ndege adimu duniani, atishiwa kutoweka

## ▪Serikali na wadau wapambana kumlinda



Wanawake wa Kijiji cha Shebomeza wakipanda miti ya asili baada ya kuondoa mihesi na maotea yake katika shamba, ili kulinda makazi ya ndege jamii ya kolokolo domorefu. **PICHA: BEATRICE PHILEMON.**

**Na Beatrice Philemon**

UKIZUNGUMZIA ndege anayeitwa kolokolo domo refu si wengi wanamfahamu ndege huyu ambaye kisayansi ni Artisornis moreaui.

Sifa yake ni pamoja na umbo dogo lakini ana mdomo pamoja na mkia mrefu.

Ndege huyu yuko katika hatari ya kutoweka na kwa sasa anapatikana katika nchi za Tanzania na Msumbiji.

Akizungumza na Nipashe kuhusu ndege huyo, kwenye Hifadhi ya Misitu ya Asili ya Amani Nature Forest mkoani Tanga, Ofisa Mradi wa Shirika la Kiraia la Nature Tanzania, linalojihusisha na uhifadhi Nsajigwa Kyonjola, anasema kwa

Tanzania anapatikana katika safu ya milima ya Usambara Mashariki mkoani Tanga, wakati Msumbiji hupatikana katika safu ya milima ya Njesi.

Anaeleza kuwa anapenda kuishi katika maeneo maalumu kama vile kando kando ya misitu au katika uwazi ndani ya msitu wa asili.

> **“Kwa mfano hapo awali mfugaji alikuwa anapata lita mbili za maziwa hivi sasa anapata zaidi ya lita sita ni hatua kubwa kutokana na mafunzo bora waliyoyapata kupitia mradi wa uhifadhi wa ndege jamii ya kolokolo domorefu.”**

### KUTOWEKA

Anasema yupo katika hatari ya kutoweka kutokana na ukataji wa miti ya asili kwa ajili ya mbao na pia tishio la miti vamizi aina ya mihesi inayojulikana kitaalamu kama (Maesopsis eminii ), ambayo hupunguza uwepo wa ndege adimu akiwamo kolokolo.

“Mihesi ililetwa Tanzania katika Milima ya Usambara Mashariki kutoka Uganda na Waingereza kati ya mwaka 1930 na 1950, na imekua na kuenea kwa wingi katika safu ya Milima ya Usambara Mashariki hasa katika msitu wa hifadhi ya Amani kwa kusambazwa na ndege wakubwa kama vile hondohondo na popo wakubwa,” anasema Kyonjola.

Miti hii inakua na kuenea zaidi katika maeno ya wazi yaliokatwa miti na yenye mwaga, hivyo kitafiti mihesi inaathiri utunzaji wa bionuai ya viumbe hawa.

Ili kumlinda ndege huyu asitoweke, kuboresha uhifadhi wa bionuai katika maeneo yao katika msitu wa hifadhi ya Amani mikakati inafanyika.

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) limewekeza katika mradi mpya wa uhifadhi wa kolokolo domorefu katika safu ya Milima ya Usambara Mashariki.

“Huu ni mradi wa miezi 14 unaogharamiwa na Mfuko wa Critical Ecosystem Partnership Fund (CEPF),” anasema Kyonjola.

Ofisa miradi huyo anasema kwa sasa mradi huu ulioanza Agosti mwaka jana katika Milima ya Usambara Mashariki-Tanga kwa kushirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wakulima, Kijiji cha Shebomeza, Mbomole na kata ya Amani, katika Wilaya ya Muheza wakishirikia na Hifadhi ya Msitu wa Asili ya Amani, unaelekea ukingoni ukimalizika mwezi ujao, (Septemba mwaka huu).

Anasema wakulima katika vijiji vya Shebomeza na Mbomole wamepewa miche ya karafuu, pilipili manga, mdalasini, miti ya asili, mizinga ya nyuki, ng’ombe wa maziwa na nguruwe.

“Tulitoa mimea hii na mizinga na mifugo kwa wakulima ili wajikite katika kilimo cha viungo kuondoa miti aina ya mihesi inayoharibu makazi ya ndege huyu na kupanda viungo na miti ya asili,” anasema ofisa miradi.

### KUONDOA MIHESI

Kadhalika mkakati wa kuondoa mihesi kwa kuanzisha kilimo cha viungo katika Kijiji cha Shebomeza na Mbomole, utasaidia kuboresha uhifadhi wa baionuai katika maeneo yao.

Pia utaongeza makazi ya ndege huyu adimu kwani ukulima wa viungo ni rafiki wa mazingira, anasema.

Nature Tanzania kwa kushirikiana na TFCG wametoa miche 666 ya mdalasini, 60 ya karafuu, 2004 ya pilipilimanga na miti ya asili 2004 imepandwa katika mashamba mbalimbali ya wanachi katika vijiji hivyo.

Mbali na hilo pia Nature Tanzania imetoa mizinga ya kisasa 10 na nguruwe 10 katika Kanisa Katoliki la Amani na wananchi wengine wamepata ng’ombe wa maziwa na nguruwe, ili kusaidia uhifadhi na ulinzi wa ndege huyu aliye katika hatari ya kutoweka na pia kujiongezea kipato badala ya kutegemea misitu.

Aidha, Kyanjola alisema zaidi ya watu 300 wakiwamo wenyeviti wa vijiji, maofisa watendaji wa vijiji na kata kutoka Vijiji vya Shebomeza na Mbomole wamepatiwa mafunzo juu ya madhara ya mihesi.

Aidha, wamefunzwa faida ya baionuai kwa binadamu, jinsi ya kumlinda kolokolo domo refu na uhifadhi wa mazingira.

Anasema mpaka sasa ekari 21 zimeng’olewa mihesi na kupandwa jamii 42 za miti ya asili inayokuwa haraka na muda mfupi katika Msitu wa Usambara na kando kando ya msitu ikiwamo ile inayomvutia ndege huyo kuendelea kuishi katika safu za Milima ya Usambara Mashariki.

### USHIRIKISHAJI WATOTO

Mradi umeshirikisha watoto katika uhifadhi wa ndege, kupitia elimu ya ndege, jinsi ya kumuita ndege, kumkamata, kujua tabia zake, wanapopenda kuishi na jinsi ya kumhifadhi.

“Lengo ni kusaidia watoto wapende na kufahamu tabia zao ili baadaye wawe waongoza watalii na watafiti wa kizazi kijacho. Na pia kuwajengea ufahamu wa kujua thamani ya kuhifadhi misitu.” Anasema Kyanjola.

Mradi huu wa uhifadhi wa kolokolo umeleta mafanikio makubwa kwa wananchi kwa sababu wamepata miradi ya kujiongezea kipato.

### VIONGOZI VIJIJINI

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Shebomeza, Michael Siafu, anasema tangu amefahamu mradi huu mwaka 2018, umekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi na kijiji.

Kabla ya kuleta mradi katika kijiji hiki, Nature Tanzania walifanya utafiti kwa kushirikiana na Amani Nature Reserve na baadaye walianza kupanda miti ya asili.

“Baada ya kuona ndege hawa wameanza kuwa wachache, Nature Tanzania kwa kushirikiana na TFCG waliamua kuja na mradi wa uhifadhi wa kolokolo domorefu lakini changamoto yake kubwa ni miti ambayo si rafiki ya mihesi,” anasema Siafu.

“Kama kijiji tunashuru Nature Tanzania na TFCG kwa kuleta mradi huu kwa sababu wananchi wanajipatia kipato kutokana na kilimo cha viungo, ufugaji wa ng’ombe na nguruwe,” anaongeza Siafu.

“Sasa hivi tuna ng’ombe wa maziwa na kuku chotala wa mayai na wananchi wameendelea kunufaika na miradi hii,” aliongeza Ofisa Mtendaji wa Kijiji.

UCHUMI WA KIJIJI

Kabla ya mradi hali ilikuwa ya kawaida watu walikuwa wanalima kiasili na walikuwa wanapata mavuno machache katika Kijiji cha Shebomeza.

“Kwa mfano hapo awali mfugaji alikuwa anapata lita mbili za maziwa hivi sasa anapata zaidi ya lita sita ni hatua kubwa kutokana na mafunzo bora waliyoyapata kupitia mradi wa uhifadhi wa ndege jamii ya kolokolo domorefu.”

Shebomeza kuna wakazi 1,141 kati ya hao wanaume ni 564, wanawake 577 na nguvu kazi ni watu 521, anasema Siafu.

Kwa upande wake Ofisa Mtendaji Kata ya Amani, Hadija Nasoro, anasema, ingawa mradi unakaribia kuisha, lakini watu wataendelea kujifunza kupitia mashamba darasa ambayo yameanzishwa na Nature Tanzania kwa kushirikiana na TFCG.

“Sisi Kata ya Amani tutaendelea kuhifadhi mazingira kwa ajili ya kumlinda ndege jamii ya kolokolo domorefu na watoto wataendelea kufundishwa aina za ndege na jinsi ya kuwahifadhi na hapo baadaye wataendelea kuhifadhi mazingira,” anasema Hadija.

Anaeleza kuwa sehemu kubwa ya hifadhi ya msitu wa Amani ina vivutio vingi vya utalii, lakini bado havijulikani.

Anasema kuna miti ya asili, ndege adimu ambao hawapatikani katika nchi nyingine ulimwenguni mbali na Tanzania.

“Tunaiomba serikali iingalie zaidi Amani, itangaze vivutio vya utalii ili iweze kujulikana katika nchi mbalimbali duniani na kusaidia hifadhi ya msitu ipate kipato na asilimia 20 ya mapato iweze kurudishwa kijijini kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya wanakijiji,” anasema.

Mkulima ambaye amenufaika na mradi huu, Amiri Said, alishukuru Nature Tanzania kwa kumpatia miche 200 ya karafuu, 300 ya mdalasini na miche 100 ya pilipili manga ili kujikita katika kilimo cha viungo ili kulinda ndege kolokolo domorefu.

Anasema kabla ya kupewa miche hiyo walifanya utafiti na kubaini eneo ambalo litapandwa mazao hayo hii ili kumvutia ndege huyu. “Walitushauri kujikita katika kilimo hiki kwa sababu kuna aina ya ndege wanaotoweka kutokana na uharibifu wa mazingira na mimi nimeingia nao mkataba wa makubaliano kwa ajili ya uhifadhi wa eneo la huyu ndege, anasema Saidi.

> **“Walitushauri kujikita katika kilimo hiki kwa sababu kuna aina ya ndege wanaotoweka kutokana na uharibifu wa mazingira na mimi nimeingia nao mkataba wa makubaliano kwa ajili ya uhifadhi wa eneo la huyu ndege, anasema Saidi.**

Anaongeza: “Tunachokifanya katika kumlinda na kumhifadhi ni pamoja na kuondoa mihesi katika mashamba yetu na kupanda miche ya viungo ikiwamo miti ya asili ili kumvutia huyu ndege.”

Hivi sasa watu wengi wanaoishi kando kando ya misitu wanalima kilimo cha viungo na kwamba viungo ni biashara nzuri ukizingatia Amani ni eneo ambalo linatoa viungo ambavyo havitumii mbolea za kemikali.

Saidi anasema ni viungo vinavyolimwa kwa kilimo hai na ni biashara nzuri inayovutia wateja na walaji wengi nje na ndani ya Tanzania kwa sababu viungo havina kemikali.

# Raia Uganda ateuliwa kuongoza UNAIDS



Winnie Byanyima, Mkurugenzi Mtendaji mpya wa UNAIDS ambaye ni raia wa Uganda. **PICHA: MTANDAO**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), António Guterres, amemteua Winifred ‘Winnie’ Karagwa Byanyima wa Uganda kuwa Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Ukimwi (UNAIDS).

Uteuzi huo unafuatia utafiti na mchakato wa muda mrefu ulioongozwa na mashirika wadhamini chini ya uenyekiti wa Dk. Natalia Kanem.

Dk. Kanem ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) na mchakato ulijumuisha mahojiano na majadiliano na pande zote husika, kupitia Bodi ya Uratibu wa Programu za UNAIDS.

Byanyima anachukua nafasi ya Michel Sidibé ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii wa Mali.

Katibu Mkuu amemshukuru Dk. Sidibé kwa kuliongoza Shirika la UNAIDS tangu mwaka 2009 hadi 2019, akiwa mstari wa mbele kukabiliana na changamoto za kimataifa za HIV na ukimwi.

Byanyima atakuja na uzoefu wa muda mrefu katika masuala ya uwezo wa serikali, mashirika mbalimbali, sekta binafsi na asasi za kiraia katika kutokomeza virusi vya HIV na ukimwi kwa jamii zote duniani.

Amekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Kimataifa la Oxfam, tangu mwaka 2013.

Kabla ya hapo kwa miaka saba alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Jinsia na Maendeleo katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP).

Alianza safari yake kama mwanaharakati wa kupigania jamii zilizotengwa na wanawake, miaka 30 iliyopita alipokuwa mbunge katika Bunge la kitaifa nchini Uganda.

Na mwaka 2004, alitangazwa kuwa Mkurugenzi wa Wanawake na Maendeleo katika Tume ya Muungano wa Afrika (AU), akifanya kazi katika masuala ya mikataba na haki za wanawake barani Afrika.

Hicho ni chombo cha kimataifa cha haki za binadamu ambacho baadaye kilikuwa nyenzo muhimu katika kusababisha kupunguza athari za maambukizi ya HIV, kwenye maisha ya wanawake wengi barani Afrika.

Byanyima ana shahada ya uzamili katika masuala ya uhandisi wa mitambo akijikita kwenye uhifadhi wa nishati na mazingira kutoka kwenye taasisi ya teknolojia ya Cranfield, Uingereza.

Aidha, ana shahada ya kwanza ya uhandisi wa masuala ya ndege kutoka Chuo Kikuu cha Manchester nchini Uingereza.

Anazungumza Kiingereza, Kiswahili na Kifaransa kidogo. Ameolewa na ana mtoto mmoja wa kiume.

Katibu Mkuu amemshukuru Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Idara ya Utawala ya UNAIDS, Gunilla Carlsson kutoka Sweden, kwa huduma yake aliyoitoa kama Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa shirika hilo.

**HABARI UN**

MAZINGIRA

# Uingereza, SBL kupanda miti 1,000

Na Joseph Mwendapole

TANZANIA inatajwa kuwa na kiwango cha uharibifu wa mazingira ya misitu cha asilimia moja kwa mwaka ambacho ni sawa na hekari 400,000 za misitu, kiasi ambacho ni mara mbili zaidi ya kile cha dunia cha asilimia 0.5 kwa mwaka.

Kuiweka hii katika uhalisia, Project Gaia, shirika la kiraia linajinasibu kutoa huduma ya nishati endelevu kwa lengo la kubadilisha sura ya umaskini wa nishati, linaonyesha kwamba kati ya mwaka 1990 na 2010, Tanzania ilipoteza takribani asilimia 19.4 ya misitu sawa na hekari takribani 8,000,000.

Hali hii ya upotevu wa misitu ni ishara ya kutoa mwanga na wito kwa wadau wa mazingira pamoja na serikali kulifanyia kazi mapema tatizo hili kabla taifa halijageuka kuwa janga, kinachotisha zaidi ni kwamba tathmini juu ya misitu ya dunia iliyofanywa na Umoja wa Mataifa (UN) pamoja na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo Duniani (FAO) inaonyesha kwamba zaidi ya hekari milioni 5.8 za misitu ya Tanzania zimepotea katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi 2015, ikiwa ni sawa na asilimia 10 ya misitu yote inayopatikana nchini.

Kati ya sababu kubwa zinazosababisha upotevu wa misitu nchini, ni kuzalisha mkaa, kilimo cha kuhamahama na mbao. Hizi ndizo zinazotajwa kuwa sababu kubwa huku sababu nyingine ndogo zikitajwa kuwa ni pamoja na mmomonyoko wa udongo, kupotea kwa wanyama pori na ufyekaji wa misitu ovyo.

Hii inaweza kuwa moja ya sababu kwamba, serikali inawajibika kutambua fika kwamba vita dhidi ya uchafuzi wa mazingira haiwezi kufanikiwa kwa kutegemea juhudi za serikali pekee bali jamii ina wajibu wa kuja na sera za mazingira zinazoweza kuboresha na kuimarisha maeneo yanayojihusisha moja kwa moja na uhifadhi wa mazingira, kwa kuhusisha sekta muhimu, mikakati pamoja na maamuzi yanayoweza kusaidia kutokomeza janga hili.

Ni katika hali hiyo kwamba mashirika na kampuni mbalimbali ni miongoni mwa wadau wanaolichukulia suala la uhifadhi wa mazingira kwa uzito unaostahili kwa kujishughulisha moja kwa moja na jitihada hizo katika jamii zinazoendesha shughuli zake.

Katika kuitikia wito huo, kampuni ya bia ya Serengeti Breweries Limited (SBL) iliendesha kampeni ya upandaji miti katika moja ya kiwanda chake kilichoko Moshi pamoja na wilayani Mwanga mkoani Kilimanjaro, na kuotesha miti 1,000.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, mpango huu wa upandaji miti umelenga kuongeza jitihada za uhifadhi wa mazingira kwa kuongeza ukijani juu ya ardhi. Swali ni kwanini suala la uhifadhi wa mazingira limeigusa kampuni binafsi ya uzalishaji bia?



Uteketezaji misitu kama huu unasababisha hekari takribani 300,000 za misitu kuangamizwa kila mwaka, ndiyo mashirika ya kijamii na kampuni kama SBL, zimejitosa kuokoa mazingira kwa kupanda miti 1,000. **PICHA; MTANDAO.**

> “SBL imejipanga kupanda miti 1,000 mkoani Kilimanjaro kama sehemu ya kuendeleza mpango wetu wa kuziunga mkono jamii zinazotuzunguka katika masuala mbalimbaali likiwamo hili la uhifadhi wa mazingira,” anasema Ocitti.

Hata sasa uchafuzi wa mazingira linabaki kuwa suala nyeti nchini kutokana na hali halisi iliyopo ikiwa ni taifa kupoteza zaidi ya hekari milioni 5.8 za misitu ya Tanzania zimepotea katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi 2015 ikiwa ni sawa na asilimia 10 ya misitu yote inayopatikana nchini.

Kwa mujibu wa SBL, suala la uhifadhi wa mazingira linachukua nafasi kubwa katika muundo wake wa uendeshaji wa shughuli zake za uzalishaji wa bia. Uhifadhi wa mazingira ni suala linalopewa kipaumbele kati ya masuala manne ya kijamii ambayo kampuni hiyo inayatekeleza kwa jamii. Masuala mengine matatu ni pamoja na mradi wa usambazaji wa maji safi na salama kwenye jamii hitaji, kutoa ufadhili wa kulipia wanafunzi kwa masomo ya elimu ya juu pamoja na kuielimisha jamii juu ya unywaji pombe kistaarabu na kutoendesha vyombo vya moto baada ya kunywa pombe.

Ni kwa muktadha huo kwamba SBL, wazalishaji hawa wamezindua kampeni ya upandaji miti 1,000 katika wilaya za Moshi na Mwanga mkoani Kilimanjaro.

“SBL imejipanga kupanda miti 1,000 mkoani Kilimanjaro kama sehemu ya kuendeleza mpango wetu wa kuziunga mkono jamii zinazotuzunguka katika masuala mbalimbaali likiwamo hili la uhifadhi wa mazingira,” anasema Ocitti.

Mkurugenzi huyu anaongeza kuwa, mpango huu umekuja katika kipindi ambacho kumekuwa na wito kutoka jumuiya ya kimataifa juu ya kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa kwa kuongeza juhudi za uhifadhi wa misitu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi na hivyo kuyaweka mazingira katika hali ya usalama kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Anafafanua zaidi faida za muda mrefu zitokanazo na upandaji miti, anataja baadhi kuwa ni kutengeneza mazingira mazuri ya kuishi viumbe hai kama binadamu na wanyama, kupunguza mabadiliko ya tabia ya nchi, kusafisha hewa, kutengeneza makazi ya wanyama, kuboresha udongo, kuhifadhi vyanzo vya maji, kupunguza mmomonyoko wa udongo pamoja na faida nyinginezo nyingi.

Juhudi za SBL za kulenga kuinua uhifadhi wa mazingira zinaenda sambamba na mradi mwingine wa usambazi wa majisafi na salama katika mkoa wa Kilimanjaro pamoja na mikoa mingine nchini, ambapo kuna uhitaji mkubwa wa huduma za visima vya maji ambavyo pia hutumiwa katika kilimo cha umwagiliaji. Mradi huu wa SBL umesaidia kuwainua wakulima wakubwa ambao hulima nafaka ambayo baadaye hutumika kama malighafi katika utengenezaji wa bia.

Zoezi hili la upandaji miti lilishuhudiwa na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Sarah Cooke ambaye aliambatana na Mwakilishi wa Waziri Mkuu wa Uingereza katika masuala ya biashara, Andrew Rosindell.

Akizungumza mara ya kupanda mti, Balozi Cooke alisema kuwa Uingereza imekuwa ikiunga mkono juhudi za uwekezaji pamoja na biashara nchini Tanzania, huku akiipongeza SBL kuwa imekuwa ni mfano mzuri wa uwekezaji. “Pamoja na uwekezaji wetu hapa nchini, tunachangia karibia asilimia tano ya mapato yetu kama ushuru kwa serikali, hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi.” Anasema Balozi.

SBL ni miongoni mwa kampuni zilizoko chini ya umiliki wa Diageo Plc, kampuni ya kimataifa ya Uingereza inayojihusisha na uzalishaji wa vinywaji kama bia, ikiwa na makao yake makuu jijini London na ofisi katika mabara sita.

Kwa upande wake, Rosindell, aliipongeza SBL kwa kuanzisha kampeni ya upandaji miti na kuongeza kuwa ushiriki wake katika zoezi hilo unadhihirisha uhusiano mzuri uliyopo kati ya Tanzania na Uingereza.

AFYA



Baadhi ya wakazi wa Mara wanaodaiwa kukataa vyoo na badala yake hujisaidia ufukweni kwenye visiwa vya Ziwa Victoria. Pichani ni kisiwa kilichomo kwenye ziwa hilo. **PICHA: MTANDAO.**

# Ni aibu karne ya 21 Mara inapokataa choo

**Na Sabato Kasika**

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inaendesha kampeni ya 'usichukulie poa, nyumba ni choo' kwa ajili ya kumlinda binadamu dhidi ya magonjwa au hatari yoyote ya kiafya inayotokana na kuzagaa kwa vinyesi vya binadamu.

Kampeni hizo zilianza tangu mwaka 2012 baada ya utafiti na kubaini kuwa asilimia 20 ya kaya hazikuwa na vyoo, lakini kupitia kampeni hiyo, asilimia imepungua hadi kufikia 5.1.

Hiyo ni kwa mujibu wa mratibu wa kampeni ya taifa ya usafi wa mazingira yenye kauli mbiu 'usichukulie poa nyumba ni choo', kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anyitike Mwakitalima.

Hata hivyo, anasema katika kutekeleza kampeni hiyo, kumejitokeza changamoto kadhaa ikiwamo za kiutamaduni kwani baadhi ya watu wenye mila za kutotumia choo kwa kile wanachodai ni laana katika familia.

Mara ni miongoni mwa mikoa yenye changamoto kwenye suala zima la vyoo bora na matumizi yake, hali ambayo inawaweka wakazi wake kwenye hatari ya kukumbwa na magonjwa ya mlipuko.

Wakati akihitimisha kampeni hizo katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, Agosti 18 mwaka huu, Mwakitalima alisema mkoa ni wa 24 kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara, kwa kuwa na usafi duni wa mazingira.

Uduni huo pia ni wa ujenzi wa vyoo bora na kutovitumia ipasavyo, hali inayoweza kuchangia magonjwa ya mlipuko, ikiwamo kipindupindu, homa ya matumbo na kuhara.

Anabainisha kuwa mkoa wa Mara una asilimia 46.6 ya kaya zenye vyoo bora, na kwamba watu wanaoishi vijijini ndio wanaofikiriwa kuwa katika hatari kubwa ya kupata magonjwa hayo yatokanayo na uchafu wa mazingira.

Ofisa Afya wa Mkoa wa Mara, Dk. Bumija Mhando, anasema asilimia 93 ya wananchi mkoa huo wanaongoza kwa kutokuwa na vyoo bora na zaidi ya kaya 22,700 sawa na asilimia saba ya makazi ya watu hawana choo.

Katika hitimisho la kampeni hizo wilayani Bunda, Mhando anasema asilimia 94 ya wananchi hawanawi mikono kila wanapotoka chooni kujisaidia.

"Takwimu zinaonyesha ni asilimia sita pekee ya wananchi wa mkoa huo wananawa mikono kila wanapotoka chooni, pia changamoto zinazosababisha kutojenga vyoo bora ni wananchi kutumia Ziwa Victoria kujisaidia haja kubwa na pia madereva wanatajwa kushusha abiria njiani ili wajisaidie porini," anasema Mhando.

Aidha, anatoa wito na kuwaomba wakazi wa mkoa wa Mara na kusema: "Naomba wananchi waelewe kuwa vyoo bora ni vyenye kuta nne, paa, sakafu, kifaa cha kunawia mikono chenye maji na sabuni."

Kwa upande wake Ofisi ya Afya wa Wilaya ya Bunda, inasema lengo la kampeni hiyo ni kuhakikisha kila kaya inatumia choo bora ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko.

Inafafanua kuwa kwa kipindi cha Aprili hadi Juni mwaka huu, takwimu zinaonyesha kuwa kaya zenye vyoo bora ni 31,725 ambazo ni sawa na asilimia 57 kati ya kaya 55,702 na 2,239 sawa na asilimia nne hazina vyoo.

Wakati ofisi hiyo ikitoka na takwimu hizo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Lidya Bupilipili, anatoa wito kwa jamii kubadilika na kuachana na vitendo vya uharibifu wa mazingira kwa kujenga vyoo bora na kuvitumia inavyotakiwa.

Mkuu wa Wilaya anawakumbusha na kuwataka wanawake na wasichana kuacha urembo wa kufuga kucha ndefu au kuweka kucha bandia kwa sababu zinaficha uchafu unaoweza kusababisha magonjwa hayo.

> **"Takwimu zinaonyesha ni asilimia sita pekee ya wananchi wa mkoa huo wananawa mikono kila wanapotoka chooni, pia changamoto zinazosababisha kutojenga vyoo bora ni wananchi kutumia Ziwa Victoria kujisaidia haja kubwa na pia madereva wanatajwa kushusha abiria njiani ili wajisaidie porini," anasema Mhando.**

### MKUU WA MKOA AKEMEA

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima, anakemea baadhi ya tabia mbaya zinazotia dosari mkoa huo kama vile ukatili dhidi ya wanawake, ubakaji wa watoto na magomvi ya kijamii kutokana na mitafaruku mbalimbali hasa ardhi na ulevi.

Anasema ukeketaji na tatizo la wananchi kuchafua mazingira kwa kujisaidia vichakani, kwenye miamba na Ziwa Victoria na kuwataka wananchi kuacha vitendo hivyo vinavyoaibisha hasa zama hizi ambazo Watanzania wengi wanafahamu kusoma na kuandika.

Mkuu huyo wa mkoa anaagiza kila mtendaji kwenye halmashauri zote za mkoa huo, kutimiza wajibu wake kuhakikisha anafikisha elimu ili kila kaya inakuwa na choo na kukitumia kikamilifu.

"Mimi kama mkuu wa mkoa siwezi kukubali kuendelea kuwa na aibu hii ya kuchafua mazingira kwa kujisaidia vichakani, kwenye miamba na ziwani achaneni na vitendo hivyo vinavyoaibisha," anasema Malima.

Malima anatoa siku 60 kwamba kila kaya iwe na choo, na baada ya hapo ataiomba timu ya hamasa ifike tena mkoani Mara kuangalia utekelezaji wake.

Aidha, anawataka wakazi wa mkoa huo kuachana na mila potofu, ambazo ni miongoni mwa sababu zinazochangia matumizi hafifu ya vyoo ikiwamo za baba mzazi kutotumia choo kimoja na watoto.

Mkuu wa mkoa anaitaka jamii ijue kuwa choo bora ni kile kinachozuia kuenea kwa kinyesi katika mazingira ya binadamu, kuwa na sakafu inayosafishika kwa maji, kiwe na usiri, mlango na paa, wasiishie kujua tu bali na kukitumia.

Anawataka viongozi kuwa mfano wa kuigwa kwa wananchi wao kwa vile baadhi ya viongozi wa vijiji kwenye baadhi ya maeneo hawana vyoo, hali inayosababisha ugumu kwa baadhi ya wananchi kuwa na vyoo bora.

AFYA



Wanawake wanahimizwa kunyonyesha watoto wachanga kwa miezi sita bila kuwapa chochote lakini inawazekanaje kama hawatasaidiwa? Kujenga vyumba mahususi kazini kwa ajili ya huduma hiyo ni moja ya mikakati ya kukamilisha azma hiyo. **PICHA MTANDAO.**

MWEZI WA UNYONYESHAJI

# Benki yaandaa chumba, wazazi kunyonyesha wakiwa kazini

**Na Mary Geofrey**

UNYONYESHAJI watoto ni moja ya uwekezaji muhimu kiafya ambao huokoa maisha, huboresha afya, kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa zima.

Ndiyo maana kila mwaka kuanzia Agosti 1 hadi 7 ni Wiki ya Unyonyeshaji Duniani, inayolenga kuhamasisha wanawake kuwalisha na kuwapa watoto wao maziwa kikamilifu ili kulinda afya zao.

Hapa nchini takwimu za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, zinaonyesha kuwa ni asilimia 40 tu ya watoto wenye umri chini ya miezi sita wananyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kulishwa chochote. Aidha, zinaeleza kuwa ni asilimia 45 wanaoendelea kunyonyeshwa maziwa ya mama mpaka wanapofikisha miezi 24 au miaka miwili.

Kwa mujibu wa takwimu hizo kupanua huduma za kuendeleza unyonyeshaji kwa kufuata taratibu sahihi za unyonyeshaji wa maziwa ya mama huzuia vifo takribani 823,000 vya watoto.

Aidha, unyonyeshaji huzuia vifo 20,000 vya wanawake vinavyotokea wakati wa kujifungu kila mwaka.

CHA KUFANYA

Moja ya changamoto inayotajwa na Wizara ya Afya inayosababisha mama kushindwa kunyonyesha mtoto wake inavyotakiwa ni kukosekana msaada kwa mzazi au mama anayenyonyesha katika mazingira ya kazi.

Benki ya NMB kwa kutambua umuhimu huo, mwaka huu imezindua chumba maalum kwa ajili ya wafanyakazi wanaonyonyesha na wajawazito.

Lengo la kuazisha chumba hicho katika ofisi za makao makuu jijini Dar es Salaam ni kuwasaidia wafanyakazi wanawake wa benki hiyo, kutekeleza kwa vitendo sera ya serikali ya kunyonyesha watoto kwa miezi sita bila kulisha chochote.

Linda Teggisa ni Mkuu wa Kitengo cha Fedha cha NMB, anasema kuzinduliwa kwa chumba hicho mapema mwezi huu, kutawasaidia wafanyakazi wanawake wanaonyonyesha kuwa na muda wa kunyonyesha bila kuathiri utendaji kazi wao.

Anasema waliona mama anayenyonyesha ili atimize vyema matakwa ya Wizara ya Afya ya kumnyonyesha mtoto wake kwa miezi sita bila kumpa chochote ni vyema akatengenezewa mazingira wezeshi.

"Tunatambua wafanyakazi wanawake wanakaa mbali na mahali pa kazi, wanatoka nyumbani mapema kuwahi kazini, tukafikiri ni namna gani tunaweza kumwezesha kumpa mtoto wake huduma anayostahili bila kuathiri utendaji kazi wake au kufanya kazi kwa wasiwasi wakati anapokuwa mbali na mtoto wake," anasema Teggisa.

"Tunaushukuru uongozi wa NMB ambao wanatambua mchango wa wanawake wa NMB na wa taifa hili, ndiyo sababu wamekubali ombi letu la kuanzisha chumba hiki maalum kwa ajili ya wazazi wanaonyonyesha na wajawazito," anaongeza.

### CHIMBUKO

Teggisa ambaye pia ni Mwenyekiti Mtandao wa Wafanyakazi Wanawake wa NMB, anasema wazo la kuanzisha chumba hicho maalum ambacho kinakuwa kama sehemu ya huduma ya kwanza kwa mama mjamzito na anayenyonyesha, lilianzia kwenye vikao vya wanawake.

Anasema waliangalia ni changamoto zipi zinazowakabili wanawake hasa kwa kuzingatia kuwa benki hiyo ina wafanyakazi wanawake takribani 1,500 nchi nzima, wakaona ni kumwezesha kufanya kazi kwa uhuru wakati anapokuwa katika kipindi cha uzazi.

"Haikuwa rahisi kueleza uongozi na kukubali kuhusu wazo hili na changamoto ilikuwa, je, vipi kwa wanawake wengine ambao wapo katika matawi mengine watanufaika vipi? Lakini tuliweza kujenga hoja ambayo kwa miaka mitatu imefanikisha leo kuwa na chumba hiki," anasema Teggisa.

### CHANGAMOTO NYINGINE

Tegissa anasema kati ya changamoto kubwa ambazo zinakabiliwa na wafanyakazi wengi wanawake ni kushindwa kujiendeleza, hivyo serikali ingewapa kipaumbele ili wajiendeleza na kuweza kushika nafasi kubwa za uongozi ndani na nje ya ofisi.

Taggisa anasema NMB inatambua kuwa kunyonyesha ni afya ya mtoto mchanga hivyo wameanzisha kitengo hicho, ili kumrahisishia mama anayenyonyesha kutoa huduma hiyo kwa mtoto wake bila kikwazo.

Teggisa anasema waliona wafanyakazi wanawake wanahitaji huduma hiyo ya kunyonyesha watoto wao, kuletewa kazini na kuwanyonyesha na kukamua maziwa kwa ajili ya watoto wao wakiwa katika eneo la kujisitiri.

Kadhalika, anasema baada ya kukamilika chumba hicho, wanatarajia kuanza kujenga vyumba kama hicho katika ofisi za matawi yote ya NMB katika kuhakikisha huduma hiyo inawafakiwa wanawake wote.

Anasema pia mbali na huduma hiyo, kupitia mtandao huo wamekuwa wakitumia kuangalia changamoto zinazowakabili wafanyakazi wanawake wa benki hiyo.

Anataja moja kubwa kuwa ni kukosa ujasiri wa kuwania nafasi za juu za uongozi kwa kuwa hawajiamini kuwa wana uwezo wa kufanya kazi hizo.

"Hivyo kupitia mtandao huu tumekuwa tukizungumza na wanawake na kuwapa ujasiri wa kuwania nafasi mbalimbali za uongoz, lakini pia kuwajenga kuwa na ujasiri wa kuweza kuongoza wengine ili inapotokea fursa hiyo wasiogope," anasema kiongozi wa mtandao huo.

### KUTIMIA LENGO

Mkuu wa Kitengo cha Ubunifu wa NMB, Josina Njambi, anasema walianzisha chumba hicho kumwezesha mama anayenyonyesha kumlisha mtoto au kumkamulia maziwa bila vikwazo na kwamba ili kupata huduma katika chumba hicho, wafanyakazi wataingia humo kwa zamu.

Anasema chumba hicho kina sehemu ya kubadilishia mtoto nguo, jokofu la kuhifadhia maziwa yanayokamuliwa, sehemu ya kukaa mama na kabati la kuhifadhia vifaa vya mama.

"Tumehakikisha mama anafanya kazi kwa weledi bila kuwaza mtoto wake, lakini pia kuhakikisha chumba hiki kinatumika kwa kazi iliyokusudiwa tunapanga ratiba ya watu kuingia na kwenda kufanya kile anachokusudia," anasema.

Njambi anasema mfanyakazi wa NMB anayenyonyesha anaweza akaletewa mtoto kazini, akamnyonyesha na kurudishwa nyumbani bila kuathiri utendaji kazi wake. Anasema pia kuwapo kwa chumba hicho kutapunguza ruhusa za wanawake wanaonyesha na kitatumiwa na wajawazipo ambao watajisikia vibaya wawapo kazini kwa ajili ya kupata huduma ya kwanza.

"Tumekuwa tukiona wafanyakazi wanaonyonyesha wanakuwa wanaomba ruhusa ya kwenda kunyonyesha au kuhangaika kukamua maziwa katika ofisi za watu au kwenye magari, lakini sasa wanaweza kuwa na uhuru wa kupata huduma hiyo," anasema.

Anaeleza kuwa kabla ya kuanzishwa kwa huduma hiyo mama alilazimika kufanya kazi kwa wasiwasi akimuwaza mtoto endapo maziwa yatakuwa yameisha na yeye hajarudi nyumbani, lakini sasa wanaweza kuwa na kufanya kazi kwa amani.

# Waaswa kuacha kuchanganya kifafa na ushirikina

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wameshauriwa kuepuka kuuhusisha ugonjwa wa kifafa na imani za kishirikiana na kuwapeleka kwa waganga wa jadi na badala yake wawapeleke hospitalini mapema ili watibiwe kabla ya ugonjwa huo haujawa sugu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Mbeya ya Ifisi, Dk. Hamis Ally, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa huo, huku akisema watu wengi wamekuwa wakidhani kuwa wagonjwa wa kifafa wamelogwa.

Alisema ugonjwa huo unasababishwa na vitu mbalimbali ikiwamo ulevi wa kupindukia, matumizi ya dawa za kulevya na mtoto kuminywa na mama wakati wa kujifungua na kwamba unatibika endapo mgonjwa atawahishwa hospitalini.

"Kuna baadhi huwa wanawaleta wagonjwa wa wao wakiwa katika hali mbaya na ukifuatilia unakuta wana imani zao ambazo si za kweli. Sasa tunawashauri wananchi wote kuwawahisha wagonjwa wanapowabaini kuwa wana tatizo hilo ili watibiwe mapema," alisema Dk. Ally.

Alisema ugonjwa huo usipotibiwa mapema, husababisha vifo kwa wagonjwa, hivyo akawataka wananchi kuachana na imani potofu na badala yake wawapeleke hospitalini.

Naye Muuguzi Mkuu wa Hospitali ya Teule ya Ifisi, Sella Mhina, aliwataka wananchi hasa vijana kuacha tabia ya unywaji wa pombe kupita kiasi kwa kuwa ni miongoni mwa sababu zinazosababisha ugonjwa wa kifafa.

Alisema baadhi ya wagonjwa wanaotibiwa kifafa hospitalini hapo, wameupata kutokana na ulevi uliopindukia. Alisema unywaji huo huathiri ubongo na kusababaisha mtu kupata ugonjwa huo.

# Miundombinu Ziwa Ngosi kuboreshwa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imeanza kuboresha miundombinu ya barabara kwenda katika Ziwa Ngosi lililopo katika Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya ili kuwezesha kivutio hicho cha watalii kufikiwa kirahisi.

Aidha, TFS inakusudia kujenga vyoo ndani ya Msitu wa Uporoto unaozunguka ziwa hilo, ili kurahisisha huduma hiyo kwa watalii wanaotembelea kivutio hicho pamoja na watumishi wanaofanya kazi kwenye maeneo hayo.

Ziwa Ngosi ni miongoni mwa vivutio bora vya utalii katika mkoa wa Mbeya na lina mwonekano wa ramani ya Bara la Afrika na lina sifa za aina yake ikiwamo kutokuwa na mto unaoingiza maji wala unaotoa na linadaiwa kuwa lilitokana na mlipuko wa volkano.

Kaimu Meneja wa TFS Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Ebrantino Mgiye, alisema jana kuwa katika Bajeti ya mwaka 2019/20, wametenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo, muhimu ili kuwezesha kufikika kwa urahisi na wageni wanapata huduma muhimu.

Alisema kwa sasa eneo hilo linafikika kwa shida kutokana na magari kutokufika, hivyo watalii wanalazimika kuyaacha na kutembea umbali mrefu mpaka kulifikia ziwa hilo.

"Lakini pia tunatarajia kuongeza 'Forest Range' (maeneo ya ulinzi wa raslimali zilizomo ndani ya msitu). Lengo la serikali ni kuhakikisha kivutio hiki kinawanufaisha wananchi na rasilimali zingine zinakuwa salama," alisema Mgiye.

Alisema wataendelea kuboresha huduma zingine ndani ya eneo hilo kadri bajeti itakavyoruhusu ili watalii wengi wavutiwe kutembelea kivutio hicho.

Mhifadhi wa Hifadhi ya Mlima Rungwe, Yusuph Tango, alisema maji ya ziwa hilo ni tofauti na ya maziwa mengine kwa madai kuwa yanabadilika rangi kulingana na hali ya hewa, hivyo kuwa na hali ya mvuto.

Alisema kwa sasa wanafanya kila linalowezekana kuhakikisha rasilimali zilizomo ndani ya Mlima Uporoto zinakuwa salama kwa ajili ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

"Watalii wanaokuja kutembelea ziwa hili huwa wanashangaa kutokana na sifa zake, kwanza lipo juu ya milima tofauti na yalivyo maziwa mengine, mwonekano wake ni wa pekee kabisa maana ni kama ramani ya Bara la Afrika ilivyo pamoja na visiwa vyake," alisema Tango.

Nao baadhi ya wananchi wanaoishi jirani na ziwa hilo, walisema miaka ya nyuma ziwa hilo lilikuwa linahusishwa na baadhi ya imani hali iliyokuwa inawafanya baadhi ya watu kuogopa kwenda kutembelea tofauti na ilivyo sasa.

Amos Mwamgobole alisema kulikuwa na imani kuwa endapo mtu akiwa jirani na ziwa hilo na akazungumza lugha ya Kinyakyusa anapotea lakini kwa sasa imani hiyo haipo tena.



Wageni kutoka mataifa mbalimbali wakigawa zawadi zilizotolewa na Taasisi ya Time to Help, kwa wanawake wa Kijiji cha Kikale, wilayani Kisarawe mkoani Pwani juzi, kama sehemu ya mpango wa taasisi hiyo wa kusaidia watu wasiojiweza wenye mahitaji mbalimbali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Vyuo sasa kufundisha lugha za alama

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WADAU wa elimu mkoani Mbeya, wameishauri serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuvilazimisha vyuo vyote vya ualimu nchini kufundisha lugha ya alama ili kuwa na idadi ya kutosha ya walimu wa lugha hiyo kwa ajili ya wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia (viziwi).

Wadau hao waliiomba pia wizara kuandaa mtaala maalumu kwa ajili ya kufundishia lugha ya alama kwa madai kuwa kukosekana kwa mtaala huo kunasababisha viziwi kukosa baadhi ya huduma muhimu kutokana na watoa huduma kutokuwa na uelewa wa lugha hiyo.

Walitoa ushauri huo juzi, wakati wa utambulisho wa Chuo cha Wakalimani wa Lugha ya Alama kijulikanacho kwa jina la Amani kilichoanzishwa katika eneo la Iwambi jijini hapa na mmoja wa wadau wa elimu maalumu mkoani Mbeya.

Mmoja wa wadau hao, Thomas Mwanga, ambaye ni Ofisa Elimu wa Kata ya Mbalizi Road, alisema endapo vyuo vyote vya walimu vitafundisha lugha hiyo, itakuwa rahisi hata kutekeleza elimu jumuishi kwa vitendo.

Alisema kwa sasa wapo walimu maalumu kwa ajili ya kufundiha wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia na kwa mwalimu ambaye hajasoma lugha hiyo inakuwa vigumu hata kuelewana na mwanafunzi mwenye changamoto hiyo.

"Lugha hii si ya viziwi pekee bali na ya kwetu sote. Ikitokea mzazi mwenye ulemavu huo akaenda shuleni kuzungumza na walimu kuhusu mtoto wake, inatakiwa walimu wote waelewane naye na si kwenda kumtafuta mwalimu ambaye ni maalumu na hiyo inachelewesha huduma," alisema Mwanga.

Naye Michael Ilanga, mkazi wa Jiji la Mbeya, alisema wakati wa kuandikisha watoto wa darasa la kwanza, baadhi ya wazazi wenye watoto viziwi wanaogopa kuwapeleka shuleni wakiamini kuwa kutakuwa na changamoto ya mawasiliano.

Alisema hali hiyo huwalazimu kutafuta shule maalumu kwa ajili ya walemavu hali ambayo alidai kuwa inazaa changamoto nyingine kuwa wakati mwingine shule hizo zinakuwa mbali na makazi ya wananchi hao.

Alisema uwapo wa chuo hicho unaleta matumaini mapya kwa wazazi na watu wote wenye changamoto hiyo kupata huduma kwa urahisi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mkurugenzi wa Chuo hicho, Philemon Mwansansu, alisema aliamua kuanzisha chuo hicho baada ya kubaini kuwa kuna changamoto ya upatikanaji wa huduma za kijamii kwa watu wenye ulemavu wa kusikia kutokana na idadi ndogo ya wakalimani.





## Sera ya kilimo kubadilishwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Mathew Mtigumwe, amesema mchakato wa kuipitia upya Sera ya Kilimo ya mwaka 2013 umeanza ili kuleta tija kwa wakulima.

Mtigumwe alitoa kauli hiyo jana katika warsha kuhusu kuongeza tija na faida kwa kukabiliana na changamoto za kilimo cha umwagiliaji iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii (ESRF).

Alisema mwezi Desemba mwaka huu, watakuwa wameshakaa vikao vya kimaamuzi ili kuipitisha sera hiyo ya mwaka 2019.

Alisema kuna mambo wanataka kuyabadilisha, ambayo yanayohitaji kupata msukumo mkubwa zaidi.

"Kwa mfano tulikuwa na Sheria ya Kilimo kwa hiyo tumeona kwamba tuje na sera mpya ili tuwe na sheria mpya, lakini pia tulikuwa tumepitia utendajii wa ujumla wa bodi zetu za mazao, tuna bodi tisa na kila bodi imeanzishwa kwa sheria yake," alisema Mtigumwe.

Vile vile, alisema umefika wakati mwafaka wa kuangalia mfumo mpya wa bodi ili kuwa na taasisi ambazo zitasimamia kilimo na mazao ya kimkakati.

"Badala ya kuwa na bodi nyingi ambazo kila mmoja inafanya kimfumo wake kuna mambo mengi ambayo yote wameyaingiza kwenye sera kwa mfano kulinda ardhi ya kilimo ambayo yatawekwa kwenye sera mpya ambayo yamekuja baada ya kuwa na malengo tofauti na yale waliyokuwa nayo siku za nyuma," alisema.

Alisema lengo ni kuzalisha zaidi na kila zao wameweka malengo mapya ili yaendane na malengo la kitaifa ya kuhakikisha wanaingia kwenye nchi ya uchumi wa kati 2025 na uchumi wa viwanda.

Naye, Mkurugenzi wa Taasisi ya Makazi ya Binadamu kutoka chuo Kikuu cha Ardhi, Makarius Mndemu, alisema utafiti uliofanywa kwenye kilimo cha umwagiliaji mikoa ya Iringa na Mbeya, umebaini kuna tija kubwa kwenye kilimo cha umwagiliji wa kisasa ikiwamo uzalishaji mkubwa wa mazao.

"Hii ni kutokana na teknolojia ya kisasa ya umwagiliaji mkulima anaweza kupima kiasi cha unyevu kilichopo kwenye ardhi na kuendelea na shughuli nyingine za kiuchumi badala ya kushinda shambani anamwagilia mazao hata kama ardhi bado ina unyevu wa kutosha," alisema.

# 'Masimango ni ukatili wa kisaikolojia'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amesema kitendo cha kumsimanga mtu au kumshambulia kwa maneno ni ukatili wa kisaikolojia kwa kuwa unamfanya mtu kukosa thamani.

Dk. Ndugulile alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza kuhusu kampeni ya kitaifa ya 'Twende pamoja ambayo inalenga kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto itakayoendeshwa mikoa mbalimbali Tanzania Bara.

Alisema vitendo vya kumshambulia mtu kwa matusi, maneno, masimango vina muathiri mtu kisaikolojia na vimekuwa vikifanyika majumbani, sokoni, shuleni na maeneo mengine.

"Kumsimanga mtu ni ukatili wa kijinsia, unamsimanga mtu anakaa bure, kulala bure vyote hivyo ni ukatili unamuathiri mtu kisaikolojia," alisema.

Dk. Ndugulile alisema kitendo hicho kinamfanya mtu kukosa thamani kwenye nyumba na jamii.

"Kwa mfano mtu kaolewa amekaa mwaka mmoja hajapata mtoto anaanza kusimangwa, umekaa ndani ya nyumba unajaza choo mara nini huo ni ukatili wa kijinsia na kisaikolojia,"alisema.

Pia alisema: "Kitendo cha baba kufariki mtu anaanza kunyanyaswa hakuna kutoka na chochote, toka kama ulivyokuja, inamfanya mtu kukosa thamani matusi, maneno maneno, masimango haya."

Akizungumzia kuhusu ukubwa wa hali ya ukatili nchini, Naibu Waziri huyo alisema kwa mwaka 2017 inaonyesha kuwa jumla ya watu 41,416 walifanyiwa ukatili wa kijinsia na walitoa taarifa kwenye vituo vya polisi ikilinganishwa na watu 31,996 waliofanyiwa mwaka 2016.

"Baadhi ya matukio yaliyotolewa taarifa ni pamoja na ubakaji, vipigo, matusi, ulawiti, kutupa watoto, ukeketaji na kuwapa mimba wanafunzi,"alisema.

Alifafanua kuwa kati ya matukio 41,416 yaliyotolewa taarifa mwaka 2017, matukio 27,703 sawa na asilimia 67 yalifanywa dhidi ya wanawake na watoto.

Kadhalika, alisema taarifa ya utafiti wa idadi ya watu na afya inaonyesha kwamba asilimia 40 ya wanawake wa umri kati ya miaka 15-49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili au kingono mara moja au zaidi katika kipindi hicho cha maisha.

Vile vile, alisema asilimia 20 ya wanawake wa umri kati ya miaka 15-49 wamefanyiwa ukatili wa kimwili katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

"Asilimia tisa ya wanawake umri kati ya miaka 15-49, wameingiliwa kimwili bila ridhaa yao, ukatili huu unafanyika zaidi kwa wanawake walioolewa," alisema.

Vile vile, alisema utafiti umebainisha kwamba nusu ya wanawake walioolewa wamefanyiwa ukatili wa kimwili kwa asilimia 39, ukatili wa kihisia kwa asilimia 36 na ukatili wa kingono kwa asilimia 14.

"Kwa upande wa watoto takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 27 ya watoto wa miaka 15-19 wamezaa na watoto wawili kati ya watano wameolewa kabla ya umri wa miaka 18," alisema.

Dk. Ndugulile alisema takwimu hizo zinaonyesha ukubwa wa tatizo linaloendelea kutishia amani kwa jamii hususan wanawake na watoto.

"Hivyo, ni matumaini yangu kupitia kampeni za aina hii kila mmoja atakuwa balozi wa kuzuia na kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imechukua hatua mbalimbali kukabiliana na hali hiyo ikiwamo kufungua vituo vya kutoa huduma kwa waathirika wa matukio hayo (one stop centre), kwenye mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Mwanza, Mbeya, Iringa na Shinyanga.




Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua mpango kazi wa kuendeleza miji hapa nchini, uliofanyika jijini Dodoma jana. Wengine ni Naibu Waziri wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH** .

# Jafo: Jiji la Dar liko ovyo ovyo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, amesema mji wa Dar es Salaam haujapangwa vizuri huku akiwataka wakuu wa mikoa kuhakikisha wanasimamia mpango kazi wa kuendeleza miji Tanzania ili isitokee kwenye miji mingine.

Jafo alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizindua mpango huo jijini hapa.

Alisema kwa sasa ongezeko la watu ni kubwa hususan katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam, hivyo mpango huo umekuja wakati muafaka licha ya Jiji la Dar es Salaam kupangwa ovyo.

"Dar es Salaam ule mji upo ovyo, hata moto ukitokea hauwezi kuokoa tujiulize ni majanga mangapi yametokea tumeshindwa kuokoa sababu ya upangaji mbaya?" Alihoji.

Alisema hatua zimechelewa kuchukuliwa kwa Jiji la Dar es Salaam. "Yaani unatamani uchukue greda uvunje nyumba kwa kuwa zimekaa vibaya nawapongeza Dodoma angalau jiji limekaa vizuri," alisema Jafo.

Akizindua, Jafo aliwataka Wakuu wa Mikoa nchini kuusimamia mpango huo ikiwa ni pamoja na kuainisha maeneo.

Alisema bila mpango kazi inawezekana kuishi maisha yasiyo mazuri. "Mabadiliko haya ambayo yanafanywa sasa hivi ni muhimu sana katika upangaji wa miji," alisema.

Jafo alisema lazima miji ipangwe vizuri kwa kuwa kwa sasa ile ambayo imepangwa vizuri imesababisha kuongezeka kwa mapato kutokana na serikali kufanikiwa kukusanya kodi.

"Kuna maeneo gari la zimamoto haliwezi kupitia, kupitisha jeneza shida, msiba unakuwa nyumba ya tatu sababu kwenye msiba hakufikiki, kuna vijana wana magari mazuri, lakini yanakaa kwa jirani wanapokaa hakufikiki," alisema.

Naye, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, alisema mpango huo ni muhimu na utasaidia katika ujenzi wa miji iliyopangika pamoja na kuongeza thamani ya ardhi.

"Serikali imetayarisha mipango kabambe 30 kwa mwaka 2018/19 na 20 imekamilika huku 10 ikiwa katika mipango mbalimbali," alisema.

Kadhalika, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Adolf Ndunguru, alisema kwa sasa miji inakuwa hivyo mpango huo umekuja kusaidia kuwapo na mpango mzuri kwenye maeneo nchini.



# UN kuiunga mkono Z'bar miradi ya maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UMOJA wa Mataifa (UN) umeahidi kuendelea kuiunga mkono Zanzibar kwa kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inayosimamiwa na mashirika yake inatekelezwa kikamilifu na kupata mafanikio kwa azma ya kuwasaidia walengwa ambao ni wananchi wa Zanzibar.

Mwakilishi Mkazi na Mratibu wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa (UN) Tanzania, Alvaro Rodriguez, alisema hayo wakati alipofika Ikulu kwa ajili ya kuaga na kufanya mazungumzo na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Alieleza kuwa Umoja wa Mataifa (UN), unapongeza sana juhudi hizo za Rais Shein na unaahidi kuendelea kushirikiana naye, huku akieleza kuwa mashirika yote ya (UN) yana matumaini makubwa ya kuona matokeo endelevu yatakayotokana na juhudi hizo katika miaka ijayo.

Pia kiongozi huyo alieleza azma ya mashirika hayo ya UN kuendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuimarisha miradi ya maendeleo ikiwamo elimu, afya, upatikanaji wa majisafi na salama, utawala bora, uimarishaji wa haki za binadamu, uwezeshaji, mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto uhifadhi wa mazingira pamoja na mambo mengineyo.

Alisema mafanikio yanayopatikana ambayo yamepewa kipaumbele katika utekelezaji wa 'Programu ya pamoja ya Zanzibar ya mwaka 2018-2021' iliyozinduliwa Agosti mwaka jana, yakiwamo kupunguza vifo vya uzazi, ukatili dhidi ya wanawake na watoto, uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake kupitia zao la mwani pamoja na uratibu wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG).

Alieleza kuwa licha ya kupangiwa majukumu mengine ya kikazi, lakini anaamini kwamba kiongozi atakayechukua nafasi yake ataendeleza uhusiano na mashirikiano mema yaliopo kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na UN.

Naye Rais Shein kwa upande wake alitoa pongezi kwa umoja huo, chini ya mratibu wake, Alvaro Rodrigues, ambaye amemaliza muda wake wa kazi nchini kwa kuendelea kushirikiana na kuiunga mkono Zanzibar katika kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mapema, Rais Dk. Shein, alifanya mazungumzo na Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (Unfpa), Jacqueline Mahol, aliyefika Ikulu Mjini Zanzibar kwa ajili ya kuzungumza naye.

Katika maelezo yake Rais Shein, alilipongeza Shirika la Unfpa kwa kuendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuhakikisha huduma za jamii zinaimarika zikiwamo huduma za afya.

Alisema kuwa Unfpa limekuwa na uhusiano na ushirikiano na serikali kwa muda mrefu na tangu wakati huo limekuwa likifanya juhudi katika kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Alieleza kuwa juhudi kubwa zimechukuliwa na mafanikio yanaonekana katika kupunguza vifo vya kinamama na watoto kwa ushirikiano wa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na washirika wa maendeleo likiwamo Shirika la Unfpa.

Kwa upande wake Mohan aliahidi kuwa shirika lake litaendelea kuziunga mkono juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kupambana na umaskini, kuwaletea maendeleo wananchi wake sambamba na kutekeleza malengo na mikakati yake iliyoiweka kwenye Mkuza III.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi ambaye pia ni mlezi wa CCM Mkoa wa Shinyanga, akimsisitiza mwanafunzi Leticia Tungu (15) anayesoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Ulowa, Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, kuwa asome kwa bidii hasa masomo ya Sayansi na kushangazwa na udogo wa umbile lake. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vitendo vya udhalilishaji vinapoteza usalama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VITENDO vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia vilivyokithiri Zanzibar vinapoteza mwelekeo wa taifa na kukosesha amani na usalama wa watoto na jamii kwa ujumla.

Naibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mwanajuma Majid, alisema hayo wakati akifungua mkutano wa kuwasilisha takwimu za vitendo hivyo kwa mwaka 2018.

"Sote ni mashuhuda hakuna siku hata moja ambayo itapita bila ya kusikia matukio ya vitendo vya udhalilishaji na ukatili mjini na vijijini," alisema.

Alisema ili kushughulikia mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji, serikali imezindua mpango wa kitaifa unaowahimiza wadau kuchukua hatua za kukinga vitendo hivyo visitokee na kufanyia kazi sababu zinazochangia kadhia hiyo.

Alisema miongoni mwa sababu zinazochangia kuendelea kwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji ni udhaifu katika malezi na mmomonyoko wa maadili.

"Nawaomba wadau wanapotekeleza shughuli zao kulitilia mkazo suala zima la wazazi, walezi na jamii kulipa uzito suala la malezi yaliyo bora na kuwa karibu na watoto wao kama ilivyohimizwa katika dini zetu," alisema.

Alisema katika utekelezaji wa mpango huo kuna haja ya wizara yake kushirikiana na ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kutathmini pamoja na kukusanya takwimu sahihi za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto, ili ziweze kutoa taswira halisi ya ukubwa wa tatizo na kusaidia katika kupanga mikakati madhubuti ya kudhibiti vitendo hivyo.

"Katika kulifanikisha hili wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imechukua juhudi za kutosha za kuhakikisha uimarishaji wa upatikanaji wa takwimu halisi ya tatizo hili."

Alieleza miongoni mwa juhudi hizo ni kuandaa nyenzo ya kukusanyia takwimu kwa taasisi zinazosimamia na kushughulikia vitendo hivyo pamoja na kuzipatia mafunzo taasisi hizo namna ya kuzitumia.

Alisema kupitia nyenzo hizo tayari taasisi hizo zimeanza kukusanya takwimu hizo na kuziwasilisha Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa serikali kwa ajili ya uchambuzi na kusambazwa kwa wadau kwa ajili ya matumizi.

Alisema mbali na juhudi hizo bado kunachangamoto za upatikanaji wa takwimu kwa baadhi ya taasisi zinazoshughulikia vitendo hivyo.

# Waziri avunja Bodi ya Bandari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Sira Ubwa Mamboya, ameivunja Bodi ya Shirika la Bandari kwa kushindwa kulisimamia shirika hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, alisema ameivunja bodi hiyo kwa mujibu wa kifungu namba 6(4)(c) Sheria namba moja ya mwaka 1997.

Alisema uamuzi wa kufanya hivyo umekuja kutokana na ripoti ya kamati ya mawaziri iliyoundwa na Rais wa Zanzibar na kuonekana kuwa bodi hiyo imeshindwa kusimamia na kusababisha shirika hilo kutotekeleza majukumu yake.

"Kuliundwa kamati ya kuiangalia bodi hiyo kuhusu utendaji wake na kuonekana imeshindwa kulisimamia shirika hilo, kitendo ambacho kimesababisha kutotekeleza majukumu yake ipasavyo," alisema Mamboya.

Alisema katika kufatilia iligundulika kuwa hata ule utendaji mbovu wa shirika unafanyika kutokana na kukosa usimamizi.

Alieleza kuwa wamepokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara kucheleweshewa utoaji wa mizigo yao bandarini hali inayowafanya kupata hasara.

Bodi hiyo iliyovunjwa ilikuwa chini ya Mwenyekiti wake marehemu Salmon Senga, aliyefariki mwezi uliopita.

# Biteko ambana mwekezaji madini kuingia ubia kinyume cha sheria

**Na Issa Mtuwa,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Doto Biteko, ameibana kampuni ya madini ya Ngwenda Ltd kwa hoja tatu zilizoifanya kampuni hiyo, kuingia makubaliano na kampuni nyingine kinyume cha sheria.

Hatua ya Biteko inafuatia ziara aliyofanya mkoani Lindi na Mtwara katika Wilaya ya Nachingwea na kuibua sintofahamu kuhusu ushirika wa kampuni hiyo na Kampuni ya Indiana kutoka Australia.

Suala hilo limefanya uongozi wa Kampuni ya Indiana kupitia Mkurugenzi wake, Bob Adam, kuja nchini kukutana na Waziri wa Madini ili kujadili kuhusu ushirika wao na Ngwena Ltd.

Juzi, Waziri Biteko alikutana na kuzungumza na mkurugenzi huyo kuhusu ushirika wao wa kuunganisha kampuni hizo bila kuijulisha wizara.

Waziri Biteko alimbana mwekezaji huyo kwa hoja tatu zilizosababisha kutopatikana majibu kwa kutokuwapo kwa mwakilishi wa upande wa pili wa Kampuni ya Ngwena Ltd.

Hoja hizo ambazo Waziri Biteko alitaka kufahamu kutoka kwa Kampuni ya Indiana ni; mosi, makubaliano kati ya Indiana na Ngwena, ambayo wizara haina taarifa, uamuzi wa kuunganisha bila kuijulisha wizara wakati kampuni moja ni ya kitanzania na nyingine ni ya kigeni.

Suala la pili ni; wizara inataka kuona makubaliano yao ya kimaslahi baina ya pande zote ili pia wizara ijue serikali inafaidikaje, na suala la tatu ni kampuni husika zinatunzaje shehena kubwa ya sampuli za madini bila kuijulisha Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) ambayo ndio yenye dhamana ya utunzaji.

Waziri Biteko aliendelea kuibana kampuni ya Indiana kupitia mkurugenzi wake huyo kwa kumuuliza uhusika wake katika Kampuni ya Ngwena Ltd., huku Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Wizara ya Madini, Edwin Igenge, akimhoji ni lini ushirika wake na Ngwena ulianza, kabla au baada ya marekebisho ya Sheria ya mwaka 2017.

Akitoa majibu kwa baadhi ya hoja na maswali, Bob Adam, alisema Indiana ndio inayomiliki Ngwena Ltd na kuifadhili kifedha na masuala mengine. Kuhusu kabla au baada ya marekebisho ya Sheria ya 2017, Adam hakuwa na uhakika na kuahidi mpaka arejee kwenye nyaraka ili ajiridhishe.

"Kampuni yetu ndio inayomiliki Ngwena Ltd kwa maana Indiana inamiliki asilimia 60 ya hisa zote na ndio maana ninasema Indiana inamiliki Ngwena," alisema Adam.

Kutokana na hoja tatu za msingi kutopatiwa majibu ya kuridhisha kwa kukosekana kwa uongozi wa Ngwena Ltd., katika kikao hicho, Waziri Biteko ametaka kupangwa kwa tarehe nyingine huku akimtaka Adam kurudi tena nchini akiwa na uongozi wa Ngwena Ltd., ili kufahamu kiundani makubaliano yao kwa kuwa mpaka sasa kampuni inayotambuliwa na wizara ni Ngwena Ltd na siyo Indiana.

Wiki iliyopita Waziri wa Madini alifanya ziara mkoani Lindi, Wilaya ya Nachingwea na kutembelea eneo la Nditi ambalo Kampuni ya Ngwena Ltd., imewekeza, moja ya mambo aliyokutana nayo ni uwapo wa makubaliano kati ya kampuni hiyo na Indiana kutoka Australia, kinyume cha sheria na uwapo wa shehena kubwa ya sampuli za madini zilizohifadhiwa kinyume cha sheria.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene (wa kwanza kulia), akishiriki zoezi la kurejeleza vyura wa kihansi alipofanya ziara ya kutembelea maporomoko ya bonde la Mto Kihansi kujionea namna mazingira yanavyotunzwa kulinda ekolojia wilayani Kilombero jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Kaya 6,459 hazina vyoo Mkoa Simiyu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MKOA wa Simiyu umetajwa kuwa ni miongoni mwa mikoa isiyokuwa na vyoo bora, licha ya kupiga hatua za kimaendeleo ikiwamo ujenzi wa nyumba za kisasa na makazi bora.

Licha ya kuwa na vyoo bora 97,536 ambayo ni sawa na asilimia 46.7, lakini kaya 6,459 zimegundulika kutokuwa na vyoo kabisa kwa asilimia 3 ambapo jumla ya kaya 215,316 zenye vyoo visivyo na ubora 208,856 ni sawa na asilimia 97.

Hayo yamebainishwa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, wakati akizungumza kwenye uzinduzi wa kampeni ya 'Nyumba ni Choo' iliofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na kusema mkoa umejipanga kuhamasisha ujenzi wa vyoo bora kila kaya.

Aidha, Sagini alisema katika kuhakikisha suala hilo linatiliwa mkazo, ni vyema sera za usafi wa mazingira zikatiliwa maanani ili kuwezesha uwapo wa vyoo bora katika jamii na vinavyotumika.

Mratibu wa Kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anjitike Mwakitalima, alisema kuwa uzinduzi wa kampeni hiyo umefanyika katika mikoa 10 ikiwamo Simiyu ambayo imeelezwa kufanya vibaya katika kipindi cha nyuma kwani ilikuwa na idadi ya vyoo vichache.

Mwakitalima alisema kampeni hiyo imelenga kuongeza uwapo wa vyoo bora kwa kipindi kifupi ili kuboresha hali ya afya katika nchi sambamba na kuukabili uchafu kwa njia zote ikiwamo kuhakikisha ujenzi wa vyoo bora kwenye ngazi ya kaya na taasisi.

"Kipindi cha nyuma mkoa huu ulikuwa unafanya vibaya kwenye eneo hili kwani kulikuwa na idadi ya vyoo vichache na kwa kupitia kampeni hii tumelenga kukabiliana na uchafu kwa njia zote ikiwamo ujenzi wa vyoo bora na matumizi ya vyoo hivyo kwenye jamii," alisema Mwakitalima.

Awali Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema tatizo hilo la kutokuwa na vyoo bora linasababishwa na baadhi ya tamaduni, ambapo katika baadhi ya jamii baba mkwe hatumii choo kimoja na mkwe.

# Maonyesho ya viwanda Mwanza kuleta nchi tisa

**Na Rose Jacob,** MWANZA

KATIKA kuunga mkono juhudi za Rais John Magufuli kwa dhamira yake ya kuifanya Tanzania ya viwanda na uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, nchi za Kenya, Uganda, Burundi, Indonesia, China, Rwanda, India, Syria na Tanzania zitafanywa maonyesho ya biashara katika Jiji la Mwanza.

Maonyesho hayo ya 14 yameandaliwa na chemba ya wafanyabiashara wenye viwanda na kilimo Tanzania (TCCIA) yatakayowakutanisha wafanyabiashara na wadau kutoka nchi zinazounda Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Maonyesho hayo yataanza rasmi Agosti 30 hadi Septemba 8, mwaka huu, katika viwanja vya Rock City Mall mkoani hapa, yakiwa na kaulimbiu isemayo 'Kuongeza ubunifu katika uzalishaji na biashara katika kukuza uchumi wetu' ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa TCCIA Mkoa wa Mwanza, Dk. Elibariki Mmari, alisema maonyesho hayo yamelenga kutoa fursa kwa kampuni za Tanzania kujifunza na kupanua wigo wa biashara za nje kwa kutumia fursa zilizopo za makubaliano ya kibiashara kati ya Tanzania na nchi nyingine.

"Maonyesho hayo yatasaidia jumuiya ya wafanyabiashara kuimarisha mtandao wa masoko na usambazaji wa bidhaa zao, kutengeneza ushirikiano wa kibiashara na ushirikiano baina ya wafanyabiashara pamoja na kampuni kujitangaza," alisema.

Alitaja washiriki wa maonyesho hayo ni kampuni binafsi na umma, idara za serikali pamoja na mifuko ya hifadhi za jamii, na kuwa wataonyesha bidhaa za kilimo, chakula, vinywaji, nguo, bidhaa za ngozi, bidhaa za viwandani pamoja na bidhaa za ujenzi.

Bidhaa zingine ni za urembo, mbao na samani, pembejeo za kilimo, vifaa vya umeme, huduma za kibiashara, mashine na bidhaa za kiuhandisi.

Dk. Mmari aliwasihi washiriki wa maonyesho hayo kufuata sheria na taratibu zote ikiwamo kutoa risiti halali za malipo baada ya kuuza bidhaa zao kama sheria inavyoelekeza.

HABARI KIMATAIFA

# Maduro akiri kufanya mazungumzo ya siri na Marekani

**CARACAS, Venezuela**

RAIS wa Venezuela, Nicolás Maduro amesema yupo kwenye mazungumzo na utawala wa Rais wa Marekani, Donald Trump kwa miezi kadhaa sasa, licha ya kuwapo kwa vikwazo vipya vya Marekani kwa taifa hilo.

Mgogoro unaoedelea wa kisiasa na kiuchumi umeifanya Venezuela kuwa na marais wawili waliojitangazia uhalali wa kuongoza. Ambao ni Maduro na kiongozi wa bunge la nchi hiyo, Juan Guaidó

Marekani ni moja ya mataifa 50 ambayo hayamtambui Maduro kama rais halali wa Venezuela.

Utawala wa Washington ulitangaza vikwazo vipya dhidi ya Venezuela mwanzoni mwa mwezi kama njia ya kumuongezea Rais Maduro shinikizo la kung'atuka.

Hata hivyo, jana Rais Maduro amethibitisha kuwa amekuwa kwenye mazungumzo na maofisa waandamizi wa serikali ya Rais Trump kwa miezi kadhaa sasa.

Akizungumza kupitia runinga, Rais Maduro alisema: "Kama nilivyofanya mazungumzo ndani ya Venezuela, pia nimetafuta namna ya kumfanya Rais Trump aisikilize Venezuela."

Kwa upande wake Rais Trump pia alithibitisha kuwa utawala wake umekuwa kwenye mazungumzo na wawakilishi wa Venezuela.

"Sitaki kusema nani, lakini tunazungumza na watu wa ngazi ya juu kabisa," alisema Rais Trump.

Taifa hilo limekabiliwa na mgogoro wa uongozi kati ya Rais Maduro na kiongozi wa bunge la Venezuela, Juan Guaidó.

Guaidó alijitangaza mwenyewe kuwa Makamu Rais Januari, akidai kwamba uchaguzi uliomleta Maduri uongozini kwa muhula wa pili ulikumbwa na udanganyifu.

Huku Guaido akiungwa mkono na mataifa 50, ameshindwa kumng'oa madarakani Rais Maduro.

Mazungumzo kati ya pande hizo mbili yalioandaliwa mjini Barbados na kuongozwa na Norway yaligonga mwamba baada ya Rais Maduro kuupinga upinzani kwa kuunga mkono vikwazo vilivyowekwa na Marekani.

Taifa hilo linakumbwa na mdororo mbaya zaidi wa kiuchumi huku robo ya idadi yake ya watu milioni 30 ikihitaji msaada kulingana na Umoja wa Mataifa (UN).

Zaidi ya raia milioni nne wa Venezuela wameondoka katika taifa hilo katika kipindi cha miaka iliopita. **BBC**

# Uganda yafuta hukumu ya kifo

**KAMPALA, Uganda**

BUNGE la Uganda limepitisha sheria inayopinga hukumu ya adhabu ya kifo kwa baadhi ya uhalifu, na kufanya marekebisho katika sheria nne tofauti ikiwamo sheria ya kupambana na ugaidi.

Endapo sheria hiyo itasainiwa na Rais Yoweri Museveni , marekebisho hayo yatasitisha hukumu ya kifo kwa uhalifu mkubwa zaidi, kwa maelekezo ya Jaji.

Watunga sheria wanasema kuwa hiyo ni hatua kubwa inayoweza kukomesha hukumu hiyo, jambo ambalo mahakama iliwahi kupigia kelele.

Hadi sasa kuna wafungwa 133 ambao wamehukumiwa kunyongwa lakini imeshapita miaka 20 tangu wahukumiwe.

Kumekuwa na kampeni mbalimbali za kutokomeza hukumu hilo nchini Uganda, kufuatia hukumu ya mwaka 2009 ya mfungwa Susan Kigula ambaye alihoji juu ya hukumu ya kifo kuwa kinyume na katiba.

Mahakama baadae ilitaka hukumu ya kifo isiwe lazima kwa kesi za mauaji, kuwasisitiza watu kuwa mtu hapaswi kuwekwa jela kwa miaka mitatu wakati amehukumiwa kunyongwa muda huo ukipita mfungwa huyo ni sawa kuwa amepewa hukumu ya kifungo cha maisha.

Mara ya mwisho Rais Museveni kuidhinisha hukumu ya kifo itekelezwe ilikuwa mwaka 1999 na watu 27 katika gereza la Luzira mjini Kampala.

Kadhalika, aliidhinisha mahakama ya kijeshi kutekeleza hukumu ya kifo mwaka 2005.

Ripoti ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu hukumu ya kifo imewasilishwa katika tume ya haki za binadamu Septemba mwaka huu na kusema kuwa kuna mataifa 170 wameachana na adhabu hiyo ya kifo kisheria na utekelezaji au hajauliwa mtu kwa zaidi ya miaka 10.

UN ambayo ina wanachama 193, hivyo ni mataifa 23 tu ndio ambayo hayakutoa hata hukumu moja ya kifo katika muongo uliopita.

Kwa kihistoria, Kanisa limekuwa likizuia adhabu ya kifo, ikiwa ni pamoja na katika karne ya 20.

Nchini Kenya wahalifu wamekuwa wakihukumiwa kifo lakini hakuna aliyewahi kuuawa tangu miaka ya 1980.

Watetezi wa haki za binadamu wamekuwa wakipigania kuondolewa kwa hukumu hiyo.

Baadhi ya wafungwa hata hivyo wamekuwa wakilalamika kwamba hakuna tofauti ya hukumu ya kifo na ile ya maisha jela kwani mfungwa huwa anaishi jela hadi kifo chake. **BBC**



Kardinali George Pell akiongozwa na askari polisi mjini Melbourne baada ya kuhukumiwa. **PICHA: ALLIANCE**

# Mahakama yamtia hatiani Kardinali kuwabaka watoto

**CANBERRA, Australia**

KARDINALI wa Kanisa Katoliki, George Pell, amerejeshwa gerezani baada ya mahakama ya Australia kutupa rufani yake dhidi ya hatia inayomkabili ya dhuluma za kingono dhidi ya watoto.

Kardinali Pell alitiwa hatiani kwa kosa la kuwabaka wavulana wawili.

Imeelezwa kuwa Kardinali Pell ataendelea kutumikia kifungo chake cha miaka sita kwa kuwashambulia kingono wavulana wawili wenye umri wa miaka 13 waliokuwa wanaimba kwaya kwenye kanisa mjini Melbourne katika miaka ya 1990.

Kardinali Pell (78) alikuwa amevaa suti nyeusi na mara kwa mara alikuwa akiinamisha kichwa chake wakati Jaji Mkuu, Anne Ferguson akisoma hukumu yake huku kundi la watu lililokusanyika nje ya mahakama hiyo likishangilia.

Jaji Ferguson alisema Kardinali Pell atakuwa atastahili kupewa msamaha baada ya miaka mitatu na miezi minane, ingawa Kardinali huyo anaweza bado kuiomba mahakama ya juu ya Australia kusikiliza rufaa zaidi.

Kardinali Pell ndiye kiongozi wa juu zaidi wa Kikatoliki kutiwa hatiani kwa makosa ya udhalilishaji wa watoto kingono, na kuifanya kesi yake pamoja na hukumu wakati wa uthibitisho kwa waumini na makundi ya wahanga kote duniani.

Aliwahi kushiriki katika mchakato wa kuwachagua mapapa, Pia aliwahi kusimamia hazina ya Vatican na alishiriki katika uitikiaji wa Kanisa la Australia juu ya madai ya udhalilishaji wa kingono dhidi ya watoto.

Pam Stavropoulos, kutoka kundi la watoto walioathirika, alisema kuthibitishwa kwa hatia dhidi ya mkosaji mashuhuri na aliewahi kuwa na mamlaka makubwa, kunatilia mkazo imani katika mchakato wa kisheria na uwezekano wa kuzungumza waziwazi.

Mawakili wa Kardinali Pell waliainisha vipingamizi 13 dhidi ya hatia zake, na kutilia mashaka kila kitu kuanzia uwezekano wa kimwili wa mteja wao kuvua majoho yake kumbaka mvulana, hadi kwenye uaminifu wa shahidi mkuu.

Kesi hiyo haikuwa ya kawaida kwa sababu ilitegemea zaidi ushahidi wa waathirika pekee aliesalia hai.

Wawili kati ya majaji wamemuelezea mwathirika kama shahidi mwenye heshima ambaye hakuwa muongo, asiye na njozi na shahidi wa ukweli.

Mmoja wa waathirika wa tukio hilo alitoa maoni yake katika taarifa iliyosomwa na wakili wake Vivian Waller, baada ya hukumu ya mahakama.

"Nimetulizwa na uamuzi wa mahakama ya rufaa. Ni miaka minne sasa tangu niliporipoti polisi. Mchakato wa jinai umekuwa wa kuchekesha. Safari hiyo imenipeleka maeneo mengi, ambayo nilihofia kwamba nisingeweza kurejea. Lakini nashukuru kwamba mahakama imempa Kadinali Pell fursa ya kupinga mashtaka, na kila fursa ya kusikilizwa. Natumai tu kwamba sasa yote yameisha."

Mwathirika wa pili wa tukio hilo alifariki mwaka 2014 baada ya kumeza dawa.

Waziri Mkuu wa Australia, Scott Morrison ameelezea huruma kwa waathirika hao na kusema mahakama imefanya kazi yake,

Amesema Kardinali Pell atanyang'anywa nishati yake ya heshima baada ya kushindwa rufani yake. **DW**

# Ofisa matatani madai ya rushwa

**Na Paul William, MOSHI**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kilimanjaro, inamshikilia Ofisa Utumishi Mwandamizi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Julius Kimaro, kwa tuhuma za kudai na kupokea rushwa ya Sh. 100,000.

Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kilimanjaro, Holle Makungu, alisema jana kuwa ofisa huyo alikuwa amepewa majukumu ya kusimamia makusanyo ya maduhuli katika halmashauri hiyo.

Makungu alisema Kimaro alikamatwa na maofisa wa Takukuru juzi maeneo ya baa iitwayo Forest katika Manispaa ya Moshi baada ya kupokea rushwa ya Sh. 100,000 kutoka kwa mfanyabiashara wa vinyago.

Alisema awali Kimaro alimkadiria mfanyabiashara huyo kuwa katika biashara yake ya vinyago anatakiwa kulipa kodi ya Sh. milioni nne kwa mwezi na kumwahidi kumpunguzia hadi Sh. milioni mbili endapo angetoa rushwa ya kiasi hicho.

Mkuu huyo alisema baada ya mazungumzo na makubaliano hayo, ndipo mfanyabiashara huyo alipotoa taarifa Takukuru iliyosababisha kukamatwa kwa Kimaro.

Alitoa rai kwa wananchi wote kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa kwa kutoa taarifa ili hatua ziweze kuchukuliwa kwa wahusika bila kujali wadhifa wa mtu au hadhi yake katika jamii.

"Nitoe wito kwa wananchi ambao wamekuwa wakiomba kutoa rushwa na watumishi wa umma wasisite kuja kwetu kutoa taarifa ili watumishi hao waweze kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria kwani jukumu lao ni kuwatumikia wananchi na sio kuomba rushwa," alisema Makungu.

**Alisema awali Kimaro alimkadiria mfanyabiashara huyo kuwa katika biashara yake ya vinyago anatakiwa kulipa kodi ya Sh. milioni nne kwa mwezi na kumwahidi kumpunguzia hadi Sh. milioni mbili endapo angetoa rushwa ya kiasi hicho.**

# Tanga yapania ushindi ukusanyaji mapato

**Na Boniface Gideon, TANGA**

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga imesema itaendelea kuimarisha mifumo yake ya ukusanyaji wa mapato ili kulifanya jiji hilo, kufanya vizuri katika nafasi za kiushindani zinazoshirikisha majiji sita.

Majiji hayo ni pamoja na Tanga, Dar es Salaam, Mbeya, Arusha, Dodoma na Mwanza.

Kauli hiyo imetolewa na Meya wa Jiji la Tanga, Mustafa Selebos, wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu namna walivyojipanga kukusanya mapato na kwamba wataendelea kutembelea miradi ya vyanzo vyake katika kuhakikisha wanafanya vizuri.

Meya Selebos alisema, Halmashauri ya Jiji la Tanga inaendelea kuimarisha vyanzo vyake vya mapato ikiwa ni pamoja na kubuni vyanzo vipya kama sehemu ya kulifanya jiji hilo kufanya vizuri zaidi.

Alisema katika taarifa ya Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo, hivi karibuni ya kuzitaja halmashauri zilizofanya vizuri, anasikitishwa kuona Halmashauri ya Bumbuli iliyopo wilayani Lushoto kutofanya vizuri. Alisema atatumia nafasi yake kama Makamu Mwenyekiti wa Alat Mkoa kuwakumbusha watendaji.

Alisema lengo si migogoro ni kufanya kazi kwa mshikamano kwa kuwasaidia watendaji, kuwakumbusha, kuwasimamia na hata kuwaelekeza, lakini pia kuwasaidia kupitisha bajeti katika kutoa ushauri mzuri wa vyanzo vipya vya mapato.

"Mimi binafsi kwa niaba ya Halmashauri ya Jiji la Tanga napenda kumpongeza mheshimiwa Rais kwa jitihada zake binafsi za kuiangalia Tanga kama jiji na ninaomba nikiri kwamba awamu hii imetimiza mambo ya msingi kwa mfano juzi tumepokea Sh. bilioni nane za miradi ya kimkakati na tumeelekeza katika stendi ya mabasi, lakini tunatarajia kupokea zaidi ya Sh. bilioni 17 katika ujenzi wa soko la kisasa Mgandini," alisisitiza Meya Selebosi.

Alisema anachokifanya Rais John Magufuli ni kuzizowezesha halmashauri kubuni fikra mpya baada ya vyanzo vingine kurudi TRA au kwenda Serikali Kuu.

Aliipongeza Halmashauri ya Jiji la Tanga baada ya kuibuka na kupata ushindi wa nafasi ya kwanza katika majiji yaliyoshiriki katika sherehe za wakulima za Nanenane, mkoani Morogoro.

Diwani wa Kata Usagara, Carlos Hiza, alisema wataendelea kuwawakilisha vyema wananchi wao kwa kuwa jukumu walilowapa ni kuhakikisha maendeleo yanapatikana ipasavyo.




Fundi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) Mkoa wa huduma wa Tegeta, akichomelea bomba kudhibiti uvujaji wa maji katika njia panda ya Kunduchi, jijini humo jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Watoto 67 wapatiwa bima ya afya

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Time To Help imewakatia bima ya afya watoto 67 wanaolelewa kwenye kituo cha kulelea watoto cha Dogodogo Center cha jijini Dar es Salaam.

Meneja Uhusiano wa taasisi hiyo, Mbwana Kitendo, alisema uamuzi wa kufanya hivyo ni kuwaondolea usumbufu wanapoumwa.

Alisema taasisi hiyo pia imewapa bima zaidi ya watoto 50 visiwani Zanzibar ambao wanalelewa kwenye vituo mbalimbali vya yatima ili wasisumbuke wanapoumwa.

Kitendo alisema mpango wa taasisi hiyo kwa sasa ni kuwapatia wafadhili wa kudumu watoto hao ambapo mtu mmoja mmoja atakuwa anachagua mtoto ambaye atakuwa anamfadhili. Kuhusu mpango wa taasisi hiyo kusaidia wahitaji kupitia Sikukuu ya Eid el Hajj kila mwaka, Kitendo alisema imezifikia Watanzania wengi visiwani Zanzibar na Tanzania Bara kwa kuwapa nyama.

Kitendo alisema kwa mara ya kwanza mwaka huu, huduma za Eid al Hajj za kuchinja ng'ombe na kuwagapa nyama wahitaji kupitia wahudumu wa kujitolea wa hapa nchini na kutoka nje ziliwafikia walengwa katika maeneo ya Singida, Tabora, Kikale na Kigoma.

Alitaja maeneo mengine yaliyokwishafikiwa na huduma hiyo kuwa ni Dar es Salaam, Zanzibar, Pwani, Tanga, Morogoro, Dodoma, Moshi, Arusha, Mwanza na visiwa vya Pemba na Mafia.

Alisema idadi ya familia zinazonufaika na huduma hii zinatarajiwa kuongezeka kutoka 20,000 za mwaka jana hadi 33,000 mwaka huu ambapo ng'ombe wanaochinjwa wakiongezeka kutoka 635 hadi 730.

Alisema kuna wahudumu wa kujitolea walioshiriki mwaka huu wanaopata 250, miongoni mwao wakiwemo 55 kutoka Ujerumani, Uswizi, Azerbaijan, Malaysia, Uholanzi, Denmark, Austria, na Uingereza.

Alisema sherehe ya Eid al Adha nchini Tanzania inaratibiwa kwa pamoja na taasisi dada za Time To Help, ambazo ni Shule za Feza, Kilimanjaro Dialogue na Muungano wa Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wachuuzi wa Tanzania (ABITAT).

Kitendo alisema kupitia taasisi hiyo wamekuwa wakijenga na kukarabati madarasa machakavu kwenye shule mbalimbali nchini ikiwa ni jitihada za kuunga mkono serikali kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu.

"Mfano shule ya Kawe B ilikuwa na nyufa sana kwasababu ilijengwa zamani sana kwa hiyo tumeifanyia ukarabati mkubwa, shule za Boko, Temboni, Kifuru wilayani Kisarawe, shule ya Idris Abdulwakil ya Mpiji Majohe na Golani Kimara," alisema.

Aliongeza kuwa shule nyingi zina shida ya maji hivyo taasisi hiyo imekuwa ikichimba visima vingi vya maji kwa shule mbalimbali nchini ili kuwaondoa wanafunzi kwenye hatari ya kupata maradhi kutokana na adha ya maji.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

**WACHIMBAJI VISIMA:** Visima Tanzania,tunachimba visima virefu na vifupi kwa gharama nafuu,na ofa ya pampu ya bure simu:0623528465/0658910584.

**Pata Ramani** za majengo mbalimbali kama Nyumba na Shule Simu: 0744113969


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA CHETI




xxxxxx

**ERAD MISRIWAY MUSHI** Amepotelewa na cheti cha elimu ya kidato cha sita alichosomea katika Shule ya Sekondari ya Mzumbe chenye index namba S.140/563 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1985. Cheti hicho kimepotea Jijini Dar es Salaam

**Yeyote atakaekiona anaombwa atpe taarifa katika kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: DAR/CEN/RB/226920/2019**

### KUPOTEA KWA PASPORT



215384001

**PRISCUS ANDREA NGOWI**

Mtajwa hapo juu amepotelewa na passport yenye no, **TAE 077905** iliyotolewa na ofisi ya uhamiaji mwaka 2019.

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**RB NO MKR/RB/3735/19**

### KUPOTEA KWA CHETI



215383902

**Catherine Jumanne Mavere** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Kilichotolewa kwa mtahiniwa **namba S.0250** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2011 katika shule ya sekondari wasichana Murigha

yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi taarifa ya polisi

**Taarifa ya polisi RB. Namba RUV/RB/4073/2019**

### KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI YA KUSAFIRIA



**Joline Joely Chief Senge** anatangaza kupotea kwa Hati ya kusafiria/Passport yenye **namba AB836426** iliyotolewa na ofisi za wizara ya Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2016.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/KIJ/RB/227751/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



115379802

**Pastory Charles** anatangaza kupotelewa nne cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1498/0103** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika Shule ya Sekondari Lugeye .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: MAB/RB/876/018

### KUPOTEA KWA CHETI



**Chelsea Daniel** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.1523/0013** kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari Mbagala Agape.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

215383402

**Polisi Taarifa: DAR/MBA/RB/225577/2019**

### KUPOTEA KWA CHETI



**Albina B. Kitona** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0401/0004** kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 1994 katika shule ya Sekondari Namfua .

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

115383502

**Polisi Taarifa: WMB/RB/5532/19**


Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

NEWSPAPER

CLASSFIED ADVERTISEMENT

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la

Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# BAILLY
## KUONGEZEWA MKATABA MAN UTD

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inapanga kumuongezea mkataba beki wake, Eric Bailly licha ya kuwa majeruhi ikihofia kwamba huenda akaondoka bure mwishoni mwa msimu huu mkataba wake ukimalizika.

Gazeti la Daily Mail limeandika kwamba, United inataka kuongeza mkataba huo ili iweze kumuuza kwa bei nzuri.

Bailly amekuwa hana nafasi ya kucheza mara kwa mara katika kikosi hicho tangu alipotua hapo akitokea Villarreal ya Hispania miaka minne iliyopita na kipindi cha majira ya joto alitajwa kwamba ataondoka.

United haina mpango wa muda mrefu na mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, lakini inataka kupata fedha katika dirisha lijalo la usajili wa kipindi cha majira ya joto.

Kuwasili kwa beki wa kimataifa wa England, Harry Maguire, kutoka Leicester City kumemaliza kabisa nafasi ya Bailly huku Kocha, Ole Gunnar Solskjaer akitaka kutengeneza upatina na Victor Lindelof.

United imevunja rekodi ya uhamisho kwa mabeki duniani kwa kumsajili Maguire kwa Pauni milioni 85. Rekodi hiyo ilikuwa ikishikiliwa na beki wa Liverpool, Virgil van Dijk aliyetoka Southampton.

# PSG WAIKATA MAINI BARCELONA

**PARIS, Ufaransa**

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Ufaransa, PSG, wameikataa rasmi ofa iliyowekwa mezani na Barcelona kwa ajili ya kumchukua Neymar kwa mkopo wa muda mrefu.

Pamoja na PSG kuwa tayari kumruhusu mshambuliaji wao huyo kuondoka klabuni hapo, lakini wanachotaka wao ni dau la maana litakalofikia lile la pauni milioni 203 walizotoa kumpata nyota huyo akitokea Barcelona.

Hata kama Barca watamalizia dau lote hadi kufikia mwaka ujao kama inavyodaiwa ili kumchukua jumla, lakini PSG hawaamini kama mabingwa hao wa La Liga watakamilisha malipo hayo kitu ambacho kimewafanya wasite kumwachia nyota huyo.

Neymar amekuwa akihusishwa na kurudi Barcelona, pia akitakiwa kwa nguvu na Real Madrid ambayo kwa sasa imeonekana kulegeza kamba kutokana na ujio wa Eden Hazard kutoka Chelsea.

Neymar amekuwa na hamu ya kurudi Barcelona ambako alicheza kwa kiwango kikubwa sambamba na Lionel Messi na Luis Suarez.



## SALAH: SINA MPANGO WA KUONDOKA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amesema hana mpango wa kuihama klabu ya Liverpool kama anavyoshauriwa na kwamba anataka kumalizia soka lake hapo kwenye dimba la Anfield.

Nyota wa zamani wa Manchester United, Gary Neville mapema wiki hii alikunukuliwa na vyombo vya habari akimshauri Salah kuihama klabu hiyo na kwenda kutafuta changamoto sehemu nyingine.



Neville alimtaka Salah kuondoka kwa mabingwa hao wa Ulaya kujiunga na klabu nyingine ili kupata mafanikio zaidi katika soka.

Lakini, nahodha huyo wa Misri amemjibua Neville akiwambia ana amani ndani ya moyo wake hapo Liverpool.

"Nina furaha Liveropool, nina furaha na jiji hili na mashabiki wake kwa ujumla,"alisema Salah akinukuliwa na Daily Mail.

Mchezaji huyo amekuwa kinara wa mabao Liverpool na miaka miwili iliyopita, alitwaa tuzo ya mfungaji bora.

Katika kuthibitisha ubora wake, Salah alifunga bao katika mchezo dhidi ya Norwich City msimu huu.

Salah amekuwa mfalme wa mabao Liverpool tangu alipojiunga na klabu hiyo ya Anfield akitokea AS Roma mwaka 2017.

Neville ambaye ni kocha na mchambuzi, alimtaka nyota huyo kuondoka Liverpool baada ya kuibuka tetesi za kutakiwa na Real Madrid ya Hispania.

Mshambuliaji huyo mwenye miaka 27, amefunga jumla ya mabao 55 katika mechi 76 alizocheza Liverpool.

HABARI MICHEZO



# POGBA

## AMWIBUA NEVILLE, ATAKA MITANDAO KUSUSIWA

**LONDON, England**

KOCHA wa timu ya Taifa ya Wanawake England, Phil Neville amesema wachezaji wanapaswa kususia mitandao ya kijamii ili kutuma ujumbe mzito kwamba ubaguzi wa rangi hautakubaliwa.

Matamshi ya Neville yanajiri baada ya kiungo wa Man United, Paul Pogba kupokea machapisho ya ubaguzi wa rangi mitandaoni kufuatia kukosa penalti wakati wa mechi waliyotoka sare ya 1-1 dhidi ya Wolves Jumatatu usiku.

"Lazima tuchukue hatua muafaka sasa kama jamii ya soka. Tumeona na wachezaji wameona katika mitandao ya kijamii," alisema Neville.

"Sijui kama jamii ya soka tunafaa kususia mitandao ya kijamii, kwa sababu Twitter haitachukua hatua yoyote, instagram haitafanya lolote - wanakutumia barua pepe wakisema kwamba watachunguza lakini hakuna kinachofanyika."

"Nimepoteza imani na yeyote anayeendesha idara za mitandao hii, hivyo basi tutume ujumbe mzito. Tususie mitandao ya kijamii kwa miezi sita. Tuone athari yake kwa kampuni hizo za mitandao ya kijamii."

Jumanne, Twitter ilitoa taarifa ikisema kuwa inashutumu kwa nguvu matusi na sasa imepiga marufuku baadhi ya akaunti kwa kukiuka sera yake ya chuki.

# Aubameyang: Arsenal itabeba ubingwa EPL

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, amesema wako tayari kupigania ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu.

Aubameyang alisema Arsenal imejiandaa kutoa upinzani katika Ligi Kuu baada ya kuanza vema katika mechi mbili za mashindano.

Mchezaji huyo alisema wamejiandaa kushinda kila mchezo baada ya kuilaza Newcastle United bao 1-0 kabla ya kuigagadua Burnley mabao 2-1.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon, alisema matokeo hayo ni salamu kwa wapinzani msimu huu.

Awali, Kocha wa Arsenal, Unai Emery alisema wataishangaza England msimu huu kwa kuwa ana kikosi bora.

**"Nadhani tangu mwanzo nilisema mapema tu mefanya usajili mzuri na utakuwa na manufaa kwetu,"alisema Aubameyang.**

Nyota huyo alisema msimu uliopita Arsenal haikuwa mbali kukata tiketi kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini msimu huu ni zamu yao.

"Najua lolote linaweza kutokea mbele ya safari, lakini ukweli ni kwamba tunataka ubingwa msimu huu,"aliongeza kinara huyo wa mabao Arsenal.

Aubameyang alifunga mabao yote ya ushindi katika mechi hizo mbili na matumaini yake ni kuipa mafanikio klabu hiyo inayotumia dimba la Emierates.

# Baba sababu Pulisic kutotua United

**LONDON, England**

SABABU ya mchezaji Christian Pulisic kukataa kusaini na Klabu ya Manchester United na kutua Chelsea, imetajwa kuwa ni Jose Mourinho.

Pulisic alinaswa na Chelsea msimu uliopita kwa dau la pauni milioni 58, kisha akaachwa kwenye klabu yake ya zamani ya Borrusia Dortmund na msimu huu ameanza rasmi kuitumikia klabu yake mpya.

Awali, Chelsea ilikuwa ikipambana na Man United katika kuwania saini ya kinda huyo wa Dortmund, na iliaminika kabisa kwamba angetua zake Old Trafford, lakini ghafla tu mambo yakabadilika.

Mourinho aliliweka jina lake kwenye orodha ya juu na mabosi wake walikuwa tayari kuweka ofa nono mezani, lakini kinda huyo alikataa.

Imebainika kuwa uamuzi wa Pulisic kugomea kutua Old Trafford ulitokana na baba yake kutovutiwa na sera ya Mourinho ya kuwanyima nafasi makinda kuonyesha vipaji vyao.

"Baba yake hakuwa upande wake kwenye dili la kutaka kwenda Man United. Sera za Mourinho kutopenda kuwatumia na kuwaendeleza vijana wenye vipaji zilimtisha," amefichua mmoja wa makocha wa zamani wa kinda huyo mwenye miaka 20, Robin Walker.



Walker alimnoa Pulisic tangu akiwa mdogo kwenye klabu ya Brackley Town na amebainisha kwamba yeye ni shabiki mkubwa wa Chelsea kwa kuwa amekulia na kuishi jijini London.

**"Hakutaka kuchezea Man United kwa sababu wakati huo ilikuwa ikiongozwa na Jose Mourinho. Baba yake Pulisic si mfuasi wa Mourinho, kwa sababu ya kutopenda kuwapa nafasi vijana. Sababu ilikuwa hiyo tu vinginevyo angekuwa yuko Old Trafford kwa sasa," alisema Walker.**

Mbali na Pulisic, Man United pia iliwakosa wachezaji wengi mastaa iliokuwa ikiwasaka kutokana na kutovutiwa na sera za Mourinho hasa za kuwakosoa hadharani.

Desemba mwaka jana, mabosi wa Man United walifikia uamuzi wa kumfuta kazi Mourinho na nafasi yake kuchukuliwa na Ole Gunnar Solskjaer, ambaye amekuwa akiwaamini vijana uwanjani.

Katika utawala wa Mourinho, makinda wenye vipaji kama Andreas Pereira, Scott McTominay, Tahith Chong, Gomes na Mason Greenwood hawakuwa wakipewa nafasi kuonyesha uwezo wao, lakini sasa Ole ameanza kuwaibua.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO NA KIGUGUMIZI CHA KUTUNDIKA DALUGA

Labda ninaweza kustaafu kazi yangu mwaka ujao ... lakini ninaweza kucheza hadi nikiwa na miaka 40 ama 41...

**TURIN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo bado hana uhakika lini atatundika rasmi daluga, akisema inaweza kuwa mapema mwaka ujao au anaweza kucheza hadi miaka 40.

Ronaldo, 34, aliendelea kuwa nyota baada ya kujiunga na Juve mwaka jana, akifunga mabao 28 katika mechi 43 kwenye mashindano yote na kuisaidia miamba hiyo ya Italia kutwaa ubingwa wa Serie A kwa msimu wa 2018-19.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] hana uhakika wa lini atastaafu rasmi kucheza soka, ingawa nyota huyo amesema haitakuwa muda mrefu kutoka sasa.

"Sifikirii kuhusu hilo," Ronaldo aliiambia TVI juzi, Jumanne.

"Labda ninaweza kustaafu kazi yangu mwaka ujao ... lakini pia ninaweza kucheza hadi nikiwa na miaka 40 ama 41.

"Sijui. Ninachoweza kusema mara zote ni kufurahia wakati wangu. Zawadi hiyo ni bora na lazima niendelee kuifurahia. "

Mbali na tuzo nyingi binafsi, Ronaldo ana rekodi ya kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tano[mara nne akiwa na Real Madrid na moja akiwa na Manchester United], ubingwa wa Ligi Kuu England mara tatu na wa La Liga mara mbili.

Ronaldo bado anaonekana anahamasika kutaka kuweka rekodi.

"Kuna mchezaji wa soka mwenye rekodi nyingi kuliko mimi?" aliuliza.

"Sidhani kuwa kuna mwanasoka mwenye rekodi nyingi zaidi yangu."

Ronaldo na Juventus wataanza mbio za kutetea ubingwa wao wa Serie A kwa kuifuata Parma Jumamosi.

## KWA UFUPI

**SANCHO AULA ZAIDI DORTMUND**

Borussia Dortmund imempa ofa nyota wa kimataifa wa England, Jadon Sancho - anayewindwa na Manchester City na Manchester United - mshahara wa pauni 190,000-kwa wiki , ambapo sasa mshahara wake utakuwa umeongezeka na kufikia karibu pauni milioni 10 kwa mwaka. ***(Mail)***

**ROJO ANUKIA MKOPO FENERBAHCE**

MIAMBA ya Uturuki, Fenerbahce inataka kumsajili beki wa Manchester United, Muargentina Marcos Rojo, 29, kwa mkopo. ***(A Spor, via Manchester Evening News)***

**SUAREZ ATEGWA JUVENTUS**

Juventus inavutiwa kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Uruguay, Luis Suarez, 32, kama mabingwa hao wa Hispania watamsajili kwa mara nyingine straika Mbrazil Neymar, 27, kutoka Paris St-Germain. ***(Tuttosport, via Sun)***

**KLOPP ATANGAZA KUSTAAFU**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema anaweza kustaafu ndani ya "miaka miwili ama mitatu" - baada ya mkataba wake na Wekundu hao kumalizika mwaka 2022. ***(Gianluca di Marzio, via Sun)***

**CAMAVINGA AVUTA VIGOGO EPL**

MIAMBA ya Ligi Kuu England, Manchester City, Tottenham na Arsenal inamfuatilia kiungo kinda wa Rennes, Muangola Eduardo Camavinga, ambaye alikiongoza kikosi chake kushinda dhidi ya Paris St-Germain kwenye mechi ya Ligue 1 Jumapili. ***(Mail)***

**JOVIC KUSEPA MAPEMA REAL**

STRAIKA wa Real Madrid, Luka Jovic, 21, anaweza kujiunga na AC Milan kwa mkopo- ikiwa ni miezi miwili tu baada ya Mserbia huyo kujiunga na miamba hiyo ya Bernabeu kwa pauni milioni 62. ***(Gazzetta - in Italian)***

**GUENDOUZI KUFUNGWA ARSENAL**

Arsenal inafikiria kumpa ofa mpya ya mkataba wa miaka mitano kiungo Mfaransa Matteo Guendouzi, 20, ambao utamfanya kulipwa mara mbili ya kiasi cha pauni 70,000 anachopokea sasa kwa wiki. ***(Mail)***

**LEMINA YAMNASA LEMINA**

Monaco imekubali dili la kumsajili kiungo wa Southampton, Mgabon Mario Lemina, 25, kwa mkataba wa mkopo wa muda mrefu kwa sharti la kuwa na kipengele cha kumnunua jumla. ***(RMC - in French)***

**WANYAMA ATAKIWA CLUB BRUGES**

MIAMBA ya Ubelgiji Club Bruges inataka kuipata saini ya kiungo wa Spurs, Mkenya Victor Wanyama, 28. ***(Express)***

**CAN CHAMBO YA RAKITIC JUVE**

Juventus ipo tayari kumjumuisha kiungo wa zamani wa Liverpool, Mjerumani Emre Can, 25, kama sehemu ya dili la kuipata saini ya kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 31. ***(Tuttosport, via Mail)***

**LLORIS ATOA WITO SPURS**

KIPA wa Tottenham, Mfaransa Hugo Lloris, 32, ametoa wito kwa miamba hiyo ya kaskazini mwa London kuwa wavumilivu wakati huu wakipania kutwaa ubingwa wao wa kwanza msimu huu tangu mwaka 2008. ***(Standard)***

**N'KOUDOU KWA MKOPO BESIKTAS**

Besiktas imekubaliana dili la mkopo wa muda mrefu na winga wa Tottenham, Mfaransa Georges-Kevin N'Koudou, 24. ***(TRT Spor - in Turkish)***

## HABARI MICHEZO

# KMC YAMWAGIWA BILIONI, YAITANGAZIA VITA AS KIGALI

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI ikielekea kuivaa AS Kigali katika mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika, timu ya KMC FC, imeongezewa morali kufuatia kulamba dume la udhamini wa Sh. bilioni moja kutoka Kampuni ya M-Bet, imeelezwa jijini Dar es Salaam jana.

Kocha Mkuu wa timu ya KMC FC Jackson Mayanja, hakusita kuitangazia vita AS Kigali wakati wa kutangazwa kwa udhamini huo jana kulikoenda sambamba na kueleza maandalizi ya mechi yao ya marudiano na uzinduzi wa jezi mpya zitakazoanza kutumika kesho katika mechi hiyo ya marudiano.

Akizungumzia mchezo huo, Mayanja alisema wataingia kwa tahadhari kubwa kuhakikisha wanatoka na matokeo mazuri.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunashinda katika mchezo huo lengo letu ni kuingia hatua ya makundi," alisema Mayanja.

Hata hivyo, alisema licha ya kukosa baadhi ya nyota wake katika mchezo huo, hakuna kitakachoharibika kwa kuwa wamesajili wachezaji wengi wazuri.

"Tumesajili wachezaji wengi wazuri hata wengine wasipocheza naamini waliopo watafanya juhudi uwanjani," alisema kocha huyo.

Akizungumzia udhamini huo, Meneja Masoko wa M-Bet, Allen Mushi, alisema mkataba huo una thamani ya Sh.bilioni moja na utakuwa ukiambatana na motisha kila timu inapofanya vizuri.

"Tumeamua kuchagua kuidhamini KMC kwa sababu tumeona ni timu ambayo imekuja kwa kasi, vile vile ilijitahidi msimu uliopita kwa kushika nafasi nzuri (ya nne) na inamafanikio makubwa," alisema Allen.

Aidha, alisema timu hiyo ina uongozi mzuri na kuahidi endapo ikipata ubingwa msimu ujao watawapa zawadi kubwa zaidi wachezaji na uongozi mzima.

Naye Mwenyekiti wa timu hiyo ambaye pia ni Meya wa Kinondoni, Benjamini Sita, alisema nafasi zipo wazi kwa mdhamini yeyote anayehitaji kuiunga mkono timu yao.

"Nafasi bado zipo kama kuna anayehitaji kutuongezea nguvu nafasi zipo," alisema Benjamini.

Kufuatia sare tasa katika mechi ya awali nchini Rwanda, mshindi wa mechi ya kesho atakutana na mshindi wa jumla kati ya Masters Security Services ya Malawi na Proline FC ya Uganda anapotokea kocha wa wa KMC, Mayanja.



Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Michael Mwita, akichezesha droo ya michuano Sprite Bball Kings 2019 jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Rais wa Mpira wa Kikapu Dar es Salaam (DBB), Okale Emessu. **MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania yazinduka Cecafa U-15 Eritrea

**Na Somoe Ng'itu, ASMARA**

TIMU ya soka ya Taifa ya vijana ya umri chini ya miaka 15, imeipa kichapo cha bila huruma yosso wenzao kutoka Sudan Kusini katika mechi ya Kundi B iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea kwa kuwafumua mabao 6-0.

Tanzania sasa imefikisha pointi tatu na inahitaji kupata ushindi katika mechi zake mbili zilizobaki dhidi ya Rwanda itakayochezwa kesho na Ethiopia hapo Jumapili ili kuweza kusonga mbele, wakati Uganda ambao wana pointi sita wako katika nafasi nzuri ya kuongoza kundi hilo.

Yosso wa Tanzania walienda mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 3-0 katika mchezo huo uliochezwa saa 8:00 mchana na kuchezeshwa na mwamuzi Idriss Mohammed kutoka Eritrea.

Bao la kwanza la Tanzania lilifungwa na Hashimu Kiambe katika dakika ya 26 wakati Rabin Sanga alifunga la pili dakika 10 baadaye na Fundumo Joseph alifunga la tatu dakika 40 ya mchezo huo.

Tanzania iliendelea kuwanyanyasa Sudan Kusini ambayo jana ilipoteza mechi yake ya tatu mfululizo katika mashindano hayo kwa kufunga bao la nne dakika ya 55 kupitia kwa Fundumo huku Sanga akifunga goli la tano na nahodha Ladaki Juma akikamilisha ushindi wa mabao sita katika mchezo huo.

Kocha wa Tanzania, Maalim Saleh, alisema amefurahishwa na ushindi huo ambao umetokana na wachezaji wake kufuata vema maelekezo aliyotoa katika mazoezi waliyofanya juzi.

Hata hivyo, Saleh, alisema kuwa vijana wake wamepoteza nafasi nyingi zaidi za kufunga mabao katika mchezo huo na anaamini watatulia zaidi ili wafanye vema katika mchezo unaofuata dhidi ya Rwanda.

# Kipenga Sprite Bball Kings 2019 chapulizwa

**Na Philip Nyiti**

KIPENGA cha mashindano ya Sprite Bball Kings 2019 kimepulizwa rasmi baada ya droo ya kinyang'anyiro hicho kinachoshirikisha jumla ya timu 43 kupangwa jijini Dar es Salaam jana.

Mashindano hayo ambayo yanaandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite, yataanza kutimua vumbi Jumapili katika viwanja vya JK Park, ambapo bingwa ataibuka na kitita cha Sh. milioni 10 huku mshindi wa pili akijinyakulia Sh. milioni tatu na mchezaji bora Sh. milion mbili.

Akizungumza wakati wa droo ya michuano hiyo na upangaji ratiba, Msemaji wa mashindano hayo, Goza Chuma, alisema hatua ya kwanza itashirikisha timu 43 kabla ya kupatikana 16 zitakazotinga 16-bora na kisha robo fainali, nusu fainali na fainali.

"Mashindano haya yanafanyika kwa msimu wa tatu mfululizo, ila kwa mwaka huu tumeyaboresha kwa kuongeza zawadi na kanuni mbalimbali ili kuleta tofauti na miaka mingine ya nyuma, hivyo tunaomba mashabiki kujitokeza kwa wingi siku ya ufunguzi," alisema Chuma.

Aidha, alisema kaulimbiu ya mashindano hayo kwa mwaka huu ni 'Sprite Bball Kings 2019 Noma Kweli'.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), Michael Mwita, aliwapongeza East Africa Televisheni na East Africa Radio pamoja na kinywaji cha Sprite kwa kuandaa mashindano hayo kwa kuwa yanaleta tija na manufaa katika kuendeleza mpira wa Kikapu Tanzania.

"Tunawaomba vijana kujitokeza kushiriki na kushuhudia mashindano hayo kwa sababu yanafungua fursa mbalimbali za kimichezo na kuwajenga kiafya," alisema.

Naye kiongozi wa timu ya Mchenga ambao ni mabingwa watetezi, Mohamed Yusuf, akizungumza kwa niaba ya timu shiriki alisema wanaamini michuano ya mwaka huu itakuwa migumu na yenye ushindani mkubwa, lakini kwa upande wao wamejipanga vizuri kutetea ubingwa wao kama ilivyokuwa misimu miwili iliyopita.

## Malindi kukosa wa3 ikiivaa Mogadishu

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Malindi itawakosa wachezaji wake wawili kuelekea mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho barani Africa (Caf) Jumamosi dhidi ya Mogadishu City ya Somalia kutokana na kukabiliwa na majeraha.

Katika mchezo huo ambao utapigwa pia katika Uwanja wa Amaan kama ulivyokuwa ule wa awali wakati zikitoka sare tasa, safari hii Malindi watakuwa wenyeji.

Mogadishu City ilitumia uwanja huo kama wake wa nyumbani kutokana suala la kiusalama nchini kwao, hivyo mchezo wa kesho Malindi itakuwa mwenyeji na mshindi wa jumla ndiye atakayesonga mbele.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Makipa wa Malindi, Saleh Machupa, aliwataja majeruhi hao kuwa ni mshambuliaji Amour Janja, nahodha Ali Khani pamoja mlinda mlango namba moja, Salula Salum.

Alisema Janja na Khani wanasumbiliwa na maumivu ya misuli ya paja huku Salula ambaye anaweza kucheza kutokana na kutokuwa na majeraha makubwa, akisumbuliwa na maumivu ya nyonga.

Akizungumzia mchezo huo, Machupa alisema hawatarajii kupoteza mchezo huo ambao una umuhimu mkubwa kwao kushinda ili kuweza kusonga mbele.

Michezo

Alhamisi Agosti 22, 2019

Nipashe



Ronaldo na kigugumizi cha kutundika daluga

HABARI UK 30



Baadhi ya wachezji wa Kikosi cha Yanga. **PICHA: MTANDAO**

# CAF YACHOMOA YANGA KUPELEKWA MACHINJONI

● ● ● Yabaini pia ujanja wa Township Rollers, yajifua na jua kali la saa tisa alasiri, Zahera asema...

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA si Shirikisho la Soka barani Afrika (Caf), kugomea ombi la Township Rollers la kuhamisha uwanja, Yanga ingeweza kukutana na dhahama kubwa katika mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa itakayopigwa Jumamosi nchini Botswana, imefahamika.

Township Rollers mapema wiki hii ilituma maombi Caf ikiomba mechi hiyo isichezwe Uwanja wa Taifa, Gaborone na badala yake ikachezwe Uwanja wa University of Botswana (UB), ambao unachukua tariban watazamaji 10,000.

Hata hivyo, Caf iliwakatalia Township Rollers kwa kile ilichoeleza kuchelewa kutuma maombi hayo ya mabadiliko ya uwanja, hivyo ikaelekeza mchezo huo upigwe katika Uwanja wa Taifa, Gaborone ambao ni wa nyasi bandia inapofanya mazoezi Yanga kwa sasa.

Ally Kimrume, Mtazania anayeishi Botswana, aliliambia Nipashe jana kuwa, kama mechi hiyo ingekubaliwa kuchezwa Uwanja wa UB, ingekuwa ni vigumu Yanga kuweza kuchomoza na ushindi hasa ukizingatia ni mdogo halafu ungefurika mashabiki na kuipa presha kubwa timu hiyo ya Tanzania.

"Aise hapa ni kama wametolewa 'machinjoni', sidhani kama pale wangenusurika kipigo maana presha ingekuwa kubwa sana halafu ndipo walipojichimbia wakijifua, lakini hata hivyo hii timu huku ina mashabiki wengi na ndiyo inayojulikana kwa kucheza soka la kiwango cha juu.

"Unaweza kuwa mchezo mgumu kwa Yanga, sema sijui kwa sasa usajili wa timu hiyo ya Tanzania na namna walivyojipanga," alisema Kimrume.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, akizungumza na Nipashe jana, alisema wamefurahi mechi hiyo kupigwa katika Uwanja wa Taifa ambao wenyeji wao wamewapangia kufanya mazoezi hapo.

"Waliomba mechi kupelekwa Uwanja wa UB, lakini Caf imewakatalia kwa sababu walichelewa kupeleka maombi yao, hivyo mechi yetu itachezwa hapa tunapofanya mazoezi kama ilivyopangwa awali," alisema Mwakalebela.

Alisema Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera amependekeza wachezaji kufanya mazoezi saa tisa mchana lengo likiwa ni kuzoea mazingira ya jua kali kutokana na aina ya uwanja wa nyasi bandia watakaoutumia katika mchezo huo.

"Wote tunafahamu mazingira ya uwanja wa nyasi bandia, siku zote unashika joto kwa sababu ya jua kali linalopiga uwanjani hapo, hivyo benchi la ufundi kwa kushirikiana na viongozi tumeshauriana kufanya mazoezi saa tisa alasiri," alisema.

Yanga inahitaji sare ya kuanzia mabao mawili ama ushindi ili kusonga mbele kufuatia mechi ya awali Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kumalizika kwa sare ya bao 1-1 Timu itakayoibuka na ushindi itakutana na mshindi wa mechi kati ya Green Mamba ya Eswatini na Zesco ya Zambia katika raundi inayofuata.

## Kahata: Lazima tushinde J'pili

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akijawa na furaha ya kupokea tuzo ya Kiungo Bora wa Mwaka nchini Kenya, winga wa Simba Francis Kahata amefunguka kuwa mechi yao ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya UD Songo ya Msumbiji Jumapili, "we must win" (lazima tushinde).

Kahata ambaye alikuwa akiichezea Gor Mahia ya Kenya msimu uliopita, ametangazwa kuwa Kiungo Bora wa Msimu na Chama cha Waandishi wa Habari za Michezo nchini Kenya wakati kipa wa Yanga, Farouk Shikalo aliyekuwa akiidakia Bandari ya nchini humo, naye akitwaa tuzo ya Kipa Bora wa Msimu.

Hata hivyo, kuelekea mechi ya Simba dhidi ya UD Songo waliyolazimisha sare ugenini nchini Msumbiji, Kahata juzi alisema anaamini kwa ushirikiano mkubwa na wachezaji wenzake wataibuka na ushindi katika mchezo huo na kusonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, Caf.

"Nina furaha sana kushinda tuzo hii, kwani malengo ya kila mchezaji ni pamoja na kushinda tuzo binafsi, ninaamini mafanikio haya nimeyapata kutokana na ushirikiano wa wachezaji wenzangu, hivyo hata hapa Simba kwa ushirikiano huo inawezekana," Kahata alisema.

Akizungumzia mechi ya Jumapili, Kahata alisema: "Hii ni mechi ambayo 'we must win' (lazima tushinde), na tofauti na Kenya na hapa Tanzania, timu inapata sapoti kubwa kutoka kwa mashabiki jambo ambalo linaongeza morali kwa wachezaji.

"Kenya mashabiki hawahudhurii kwa wingi uwanjani kama Tanzania, hilo pia linaongeza sana morali, hivyo kwa sapoti kubwa tunayoipata tunaweza kushinda na ninaomba mashabiki waendelee kuisapoti timu."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002